

JARIDA LA FAHARI YA KISWAHILI (JAFAKI)



ISSN: 2799 - 2187

**JUZUU 01
2022**

**TOLEO 01
2022**

**KITIVO CHA SANAA NA SAYANSI ZA JAMII
CHUO KIKUU KATOLIKI RUAHA**

BODI YA WAHARIRI

Mhariri Mkuu

Prof. A. K. Mutembei - Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania

Mhariri Msaidizi

Dkt W. Migodela - Chuo Kikuu Katoliki Ruaha, Tanzania

Mhariri Mshauri

Timoth Mapunda - Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania

Bodi ya Washauri

Prof. C. S. Momanyi - Africa Translingual Translators, Kenya

Prof. E. S. Mohochi - Chuo Kikuu cha Kibabii, Kenya

Dkt M. Hans - Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania

Dkt M. Juma - Baraza la Kiswahili Zanzibar, Tanzania

Dkt P. Ntawigira - Chuo Kikuu cha Rwanda

Dkt Y. Mgogo - Ofisi ya Rais TAMISEMI, Dodoma Tanzania

Kamati ya Wahariri

Dkt A. Sote - Chuo Kikuu Kishiriki Katoliki Mbeya, Tanzania

Dkt C. Simon - Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Tanzania

Dkt F. L. Ilomo - Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania

Dkt G. Kawonga - Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa, Tanzania

Dkt J. Kisanji - MS Training Centre for Development Cooperation in Eastern and Southern Africa, Tanzania

Dkt J. M. Kavoi - Chuo Kikuu cha Mt. Agustino, Mwanza Tanzania

Dkt M. Kanigi - Chuo Kikuu cha Mzumbe, Tanzania

Dkt M. Kibiki - Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam, Tanzania

Dkt M. L. Kahaika - Chuo Kikuu cha Makerere, Uganda

Dkt N. Nturo - Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira, Tanzania

Dkt R. Gaudioso - Chuo Kikuu cha Naples L'Orientale, Italia

Dkt R. Sekile - Chuo Kikuu Kishiriki Katoliki Mbeya, Tanzania

Dkt S. Faustine - Chuo Kikuu cha Dodoma, Tanzania

Dkt W. K. Mlaga - Chuo Kikuu cha Rwanda

Dkt Z. Philipo - Chuo Kikuu cha Dodoma, Tanzania

Sekretarieti

Dkt A. Nyamahanga - Chuo Kikuu Katoliki Ruaha

Dkt G. Mwangosi - Chuo Kikuu Katoliki Ruaha

YALIYOMO

BODI YA WAHARIRI.....	i
MAELEZO KWA WAANDISHI	iii
Matumizi ya Lugha Yanavyoibua Dhamira katika Ushairi wa Kiswahili.....	1
Charles Mbiu	
Uchimuzi wa Fikra za Kijaala katika Ushairi wa Kiswahili: Mifano Kutoka <i>Tungizi za Mnyagatwa na Diwani ya Midulu.....</i>	17
Hassan R. Hassan na Athuman Ponera	
Nyimbo za Asili Zinavyoimarisha Mafunzo ya Jadi nchini Tanzania.....	34
Deus Gracewell Seif	
Ufutuhi kama Mbinu ya Kuwasilisha Dhamira za Kisiasa katika Katuni za Mtandaoni za Masoud Kipanya	54
Majuto Kapaya Manyuka	
Usawiri wa Lugha ya Ishara Iliyotafsiriwa katika <i>Shetani Msalabani.....</i>	66
Birigitha Ngwano John	
Utata katika Ufasiri wa Maana za Sitiari za Kiswahili.....	77
Mofart Onyoni Ayiega	
Utelezi wa Uainishaji wa baadhi ya Maneno ya Kiswahili: Kigezo cha Kimofosintaksia.....	92
Elishafati J. Ndumiwe	
Utandawazi wa Kiswahili: Kuimarika na Kulegalega kama Lugha Rasmi ya Afrika	105
Mohamed Omary Maguo	
Mapungufu ya Kiutamaduni Yanayoathiri Ustawi wa Mwanamke katika Jamii: Mifano kutoka Riwaya ya <i>Sikujua</i>	115
Ndimyake Mwakanjuki	
WAANDISHI WA MAKALA	131

MAELEZO KWA WAANDISHI

Jarida la Fahari ya Kiswahili (JAFAKI) ni jarida la kitaaluma lililopo chini ya Idara ya Lugha, Kitivo cha Sanaa na Sayansi ya Jamii, Chuo Kikuu Katoliki Ruaha, Iringa Tanzania. Jarida lilisajiliwa na Maktaba Kuu ya Taifa 2021. Jarida linachapishwa mara moja kwa mwaka na limejikita katika uchapishaji wa makala za Fasihi, Isimu na Utamaduni wa Kiswahili. Mojawapo ya majukumu yake ni kuwasaidia wataalamu wa lugha ya Kiswahili kupata fursa ya kuchapisha matokeo ya tafiti zao walizofanya katika nyanja za Fasihi, Isimu na Utamaduni wa Kiswahili. Waandishi, watafiti na wapenzi wa Kiswahili wanakaribishwa kuchapisha makala zao.

Tunapokea makala yanayohusu Fasihi, Isimu na Utamaduni wa Kiswahili. Makala yaandikwe kielekroniki na kuacha nafasi moja na nusu baina ya mistari kwa kutumia vipimo vya karatasi za A4. Mwandishi atumie programu ya word, window 7 na kuendelea. Ukurasa wa kwanza wa makala uoneshe jina la makala, jina kamili la mwandishi na anuani ya barua-pepe. Ikisiri iwe fupi, isizidi maneno 300. Unapotaja marejeleo katika matini unataja tu jina la mwisho la mwandishi likifuatiwa katika mabano, tarehe ya chapisho lake. Kwenye marejeleo, majina ya waandishi yapangwe kialfabeti. Makala ziandikwe kwa lugha ya Kiswahili, ziwe na maneno kati ya 3000 – 6000 na urejeleaji ufanywe kwa kutumia mtindo wa APA Toleo la 6. Makala zote zitumwe kwa Mhariri Mkuu kupitia baruaapepe jafaki@rucu.ac.tz.

Kwa maelezo zaidi, wasiliana na Mhariri Mkuu kupitia:

Mhariri Mkuu,
Jarida la Fahari ya Kiswahili,
S. L. P 774,
Iringa.
Baruaapepe: jafaki@rucu.ac.tz

Matumizi ya Lugha Yanavyoibua Dhamira katika Ushairi wa Kiswahili

Charles Mbiu
Chuo Kikuu Huria cha Tanzania

mbiu91@gmail.com

Ikisiri

Makala hii imechunguza matumizi ya lugha yanavyoibua dhamira katika ushairi wa Kiswahili. Utafiti huu umefanywa kwa kurejelea diwani mbili, yaani *Wasakatonge* (2003) na *Chini ya Mwembe* (2017). Data za msingi za makala hii zilipatikana maktabani kwa mbinu ya usomaji makini na uchambuzi wa nyaraka. Matokeo ya utafiti uliozaa makala hii yameonesha jinsi kipengele cha lugha kinavyoibua dhamira katika diwani teule. Vipengele vya lugha vilivyowasilishwa vilikitwa katika mazingira, historia na utamaduni wa jamii iliyomkuza na kumlea mwandishi. Pia, imeonesha kuwa lugha na dhamira ni vipengele vinavyotegemeana na kukamilishana katika kazi ya fasihi. Makala hii inapendekeza kuwa serikali itunge kanuni na sheria kali ili kudhibiti matumizi ya lugha ya fasihi za kigeni zisizoendana na uhalisia wa mazingira ya Tanzania na Afrika kwa ujumla.

Istilahi za Msingi: Matumizi ya Lugha, Dhamira na Ushairi wa Kiswahili.

1.0 Utangulizi

Makala hii imechunguza jinsi matumizi ya lugha yanavyoibua dhamira katika ushairi wa Kiswahili. Utafiti huu umefanywa kwa kurejelea diwani ya *Wasakatonge* (2003) na *Chini ya Mwembe* (2017). Matumizi ya lugha ni mojawapo ya vipengele vinavyopewa nafasi kubwa katika kutekeleza, kuongoza na kutoa mafunzo kuhusu tabia, falsafa, mila na desturi za jamii (Mahenge, 2009). Hali hiyo husaidia kujenga na kuimarisha misingi imara ya mazingira na utamaduni wa jamii nyingi hapa nchini. Matumizi ya lugha yanaambatana na utendaji thabiti na hubadilika kulingana na muktadha. Jambo hilo linawafanya

MAKALA HALISI HISTORIA YA MAKALA

Kupokelewa: 08 Machi

2022

Kurekebishwa: 30 Juni

2022

Kukubaliwa: 29 Julai

2022

Kuchapishwa: 20

Septemba 2022

ISSN: 2799 – 2187

Juzuu 1,

Toleo 1,

uk. 1 – 16.

NUKUU

Mbiu, C. (2022). Matumizi ya Lugha Yanavyoibua Dhamira katika Ushairi wa Kiswahili. *Jarida la Fahari ya Kiswahili*, 1(1), 1 – 16.

baadhi ya wanazuoni kuitalii fasihi na kuikita katika muktadha mpana wa kijamii na kihistoria katika kuuelewa utamaduni na mazingira yake.

Muunganiko wa jamii na lugha yake huweza kuthibitishwa kihistoria na kiutamaduni. Jambo hilo linatokana na ukweli kwamba, kila utamaduni unaofahamika katika jamii za dunia una lugha yake (Jesse, 2017). Matumizi ya lugha hutazamwa kama matendo ya msingi ya binadamu. Kuna muunganiko mkubwa kati ya lugha na maisha halisi ya kila siku ya binadamu wa sasa na wa tangu hapo kale. Matumizi ya lugha yanatawaliwa na kuchukuliwa kama chombo muhimu cha kupambana na harakati za maisha ya kila siku katika jamii. Makala hii iliitazama lugha kama sehemu kamili ya mfumo wa asili wa kupitisha maarifa katika jamii teule.

Ndani ya lugha yoyote kuna mengi yaliyo bora kulingana na misingi ya kiasili ya jamii inayohusika. Matumizi ya lugha ni matokeo ya yale yaliyomo katika jamii kwa kuwa hakuna tukio lolote katika maisha ya kiutamaduni ya Waafrika ambalo si zao la jamii inayohusika (Wambua, 2001). Fasihi hutazamwa kama chombo cha kijamii kinachodhibitiwa na mahitaji ya wakati ya jamii inayohusika. Hoja hii ilitumika kama mwongozokatika uchunguzi wa matumizi ya lugha katika diwani ya ya *Wasakatonge* (2003) na *Chini ya Mwembe* (2017). Jamii iliyoandikiwa ilichunguzwa kwa undani kwa kuwa ina nafasi kubwa iliyofungamana kikamilifu na fasihi yake. Uchunguzi wa matumizi ya lugha ulijikita katika misingi ya utamaduni wa maisha ya kila siku ya jamii hiyo.

2.0 Mbinu za Utafiti

Makala hii imechunguza namna matumizi ya lugha yanavyoibua dhamira katika ushairi wa Kiswahili. Utafiti huu umefanywa kwa kurejelea diwani za *Wasakatonge* (2003) na *Chini ya Mwembe* (2017). Data za msingi za makala hii zilipatikana maktabani kwa mbinu ya usomaji makini na uchambuzi wa vitabu teule. Vitabu hivyo viliteuliwa kwa sababu vina mawanda mapana yaliyosheheni data zilizokidhi mahitaji ya makala hii. Mapitio ya nyaraka zilizotumika kuthibitishadata za msingi katika makala hii zilipatikana kwa kudurusu nyaraka za kimaktaba na kieletroniki. Maktaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania iliteuliwa kwa kuwa ina data za kutosha zinazohusiana na mada iliyoshughulikiwa.

3.0 Matumizi ya Lugha Yanavyoibua Dhamira katika Ushairi wa Kiswahili

Diwani teule zilizochunguzwa katika makala hii zina utajiri mkubwa uliojilimbikiza katika vipengele vya lugha. Lugha ni chombo cha mawasiliano yanayohitilafiana kulingana na muktadha wa matumizi na uwasilishwaji wake (Okemwa, 2017). Katika makala hii, mjadala ulilenga kubaini namna vipengele vya lugha vilivyosaidia kuibua dhamira katika diwani teule. Vipengele vya lugha vilivyochunguzwa ni tashihisi, sitiari, methali, tashibiha na misemo.

3.1 Tashihisi

Tashihisi ni tamathali ya usemi ambayo vitu visivyo na sifa walizonazo binadamu hupewa sifa hizo. Tashihisi ni aina ya tamathali ambayo hutoa maelezo ambayo hukipa kitu sifa alizo nazo mwanadamu (Ali, 2005). Vitu au wanyama hao, baada ya kupewa sifa hizo, hufanya na kutenda kama binadamu. Mfano, Mbayumbayu waliruka huko na huko angani, wakimtukuza Muumba wao kwa anga zuri lililotandaa kila mahali (Madumulla, 2009). Tashihisi ni mbinu inayojulikana pia kama uhaishaji au uhuishi. Pia, hutumiwa sana katika mashairi au lugha ya kishairi, ingawa inaweza pia kupatikana katika mazungumzo ya kila siku (Wamitila, 2016). Mbinu hii hutumiwa na msanii ili kuibua dhamira fulani ambayo ameikusudia kuifikisha kwa jamii yake.

Katika diwani ya *Wasakatonge*, msanii ametumia tashihisi kuonesha matatizo ya ukabila na udini katika jamii. Kwa muda mrefu, Bara la Afrika limekuwa likisumbuliwa na masuala ya ukabila na udini na wakati mwingine kusababisha machafuko endelevu katika baadhi ya mataifa. Jamii hizo zimekuwa katika maisha ya uhasama na chuki miongoni mwao kutokana na kukumbatia masuala ya ukabila na udini. Ukabila ni dhana inayohusu utamaduni na njia ya maisha. Ukabila unaweza kuonekana katika lugha, dini, mavazi, chakula na bidhaa za kiutamaduni kama vile muziki na sanaa. Ukabila mara nyingi ni chanzo kikuu cha migogoro ya kijamii (Khatibu, 2003). Jamii katika nchi nyingi zimeangamia kutokana na masuala ya ukabila. Udini ni kile kitendo cha kuwabagua, kuwatenga, kuwanyanyasa na kuwatesa watu wa dini fulani, wengine wakiendelea kuneemeka (Rangimoto, 2013). Matatizo ya ukabila na udini huzorotesha maendeleo katika nchi nyingi katika Bara la Afrika. Katika shairi la *Afrika*, msanii anaeleza:

Lini?

Afrika utakuwa,
 Bustani ya amani,
 Ukabila kuuzika,
 Udini kuufyeka,
 Ni lini? (Uk. 6).

Katika shairi hili, msanii ametumia tashibiha ‘Afrika’ na kuuliza kuwa lini atauzika na kuufyeka ukabila na udini? Tashibiha hii imetumiwa kuonesha matatizo ya ukabila na udini yanayoliandama bara la Afrika. Msanii anatamani Afrika kuwa bara lenye amani na kuondokana na masuala ya ukabila na udini. Suala la udini huudhoofisha umoja na mshikamano wa kitaifa na kikanda. Katika nchi yetu, hisia za udini zilianza kupenya na kuenezwa na wanasiasa wasio waadilifu mara tu mfumo wa vyama vingi vya siasa vilipoanza mapema miaka ya 1990 (Jesse, 2008). Jitihada kubwa na za makusudi zinapaswa kuchukuliwa kuondoa ukabila na udini katika jamii. Tatizo la ukabila na udini litaondoka kwa viongozi kuwahamasisha wananchi wao kuishi pamoja, kusaidiana na kuaminiana (Bishop, 2007). Ukabila huchochea ubaguzi na kuondoa umoja na mshikamano miongoni mwa wanajamii.

Katika diwani ya *Wasakatonge*, msanii ametumia tashihisi kuonesha hali ngumu inayowakabili Waafrika. Hali ngumu ya maisha husababisha kuongezeka kwa hali ya umaskini. Kwa kiasi kikubwa, hali ngumu ya kimaisha kwa jamii huchangiwa na kukosekana kwa utawala bora (Bjuremalm na wenzake, 2016). Baadhi ya viongozi wamekuwa chanzo kikuu cha hali ngumu katika jamii kutokana na kukiuka maadili na utawala uliojengwa katika misingi ya sheria na katiba ya nchi. Maamuzi mengi na sera zinazopitishwa ni zile zenye kuwanufaisha watu wachache na kuwaacha wananchi walio wengi katika wimbi kubwa la umaskini. Hatua za haraka zinapaswa kuchukuliwa ili kuondoa masuala yanayosababisha hali ngumu katika Bara la Afrika. Katika shairi la *Tiba Isotibu*, msanii anaeleza:

Twajua,
 Inaumwa Afrika,
 Sana inatilika,
 Taabani yateseka,
 Roho yake yakatika,
 Yataka tiba (uk. 18).

Msanii ametumia tashihisi inayosema, ‘Inaumwa Afrika’ akimaanisha kuwa matatizo yaliyopo Afrika yanajulikana. Afrika inakabiliwa na hali ngumu ya maisha, maradhi pamoja na ujinga uliokithiri miongoni mwa wananchi wanyonge. Viongozi wameshindwa kunusuru jamii kuondokana na matatizo yaliyopo. Kutokana na ujinga uliopo miongoni mwa Waafrika, baadhi ya wananchi na viongozi wanadhani kuwa dawa ya kuondokana na matatizo ni kuwakaribisha wageni kutoka nje ya Bara la Afrika. Hakuna umaskini mbaya kama umaskini wa mawazo (Nyerere, 1967). Jamii inapaswa kutambua kuwa matatizo ya Waafrika yatatatuliwa na Waafrika wenyewe.

3.2 Sitiari

Sitiari ni mbinu ambayo haina tofauti na tashibiha kwani mbinu zote mbili hufanya kazi ya ulinganisho wa vitu au watu. Sitiari hulinganisha vitu viwili visivyoyo na uhusiano wa moja kwa moja bila kutumia viunganishi vya *mithili ya, mfano wa, sawa na, kama* na kadhalika. Sitiari ni maelezo yanayolinganisha na kuhusisha vitu vilivyo tofauti kitabia na kimaumbile, maana na hisia ya kitu kingine (Jilala, 2008). Kwa kawaida, sitiari huwa na sehemu tatu: kizungumzwa, kifananishi na kiungo. Makala hii inaitazama sitiari kama chombo muhimu kinachobeba dhamira mbalimbali za mtunzi zenye kuuelimisha umma.

Katika diwani ya *Chini ya Mwembe*, msanii ametumia sitiari kuonesha umuhimu wa usafi katika jamii. Usafi ni neno lenye asili ya Kiarabu lenye maana ya kuwa safi pande zote. Usafi unaweza kuwa unahusu mazingira, mwili, matendo na roho. Usafi wa kimwili ni kitendo cha kuwa safi kimwili, ingawa si lazima usafi huo uendane na ule wa kiroho na kimatendo. Pamoja na hayo, usafi wa mwili ni muhimu katika kulinda afya (Kibiki, 2011). Jamii haina budi kuzingatia suala la usafi kwa kuwa ni muhimu ili kulinda afya pamoja na kuyaendeleza mazingira rafiki ya kuishi. Katika shairi la *Madaha ya Kitanzania*, msanii anaeleza:

Mguu chupa ya bia, mavazi hauchagui,
Ardhi waitifua, wachafuka maadui,
Madaha ya Kitanzania, urembo ulio adimu (uk. 48).

Msanii ametumia sitiari iliyosema, ‘Mguu chupa ya bia’ kusifia uzuri alio nao mhusika. Msanii ametumia sitiari kuhamasisha jamii hususani wanawake kujitunza na kuzingatia usafi wakati wote. Usafi umekuwa ni moja ya nguzo muhimu katika kudumisha mahusiano katika jamii na katika ndoa. Usafi ni ujuzi wa kujifunza. Jamii inapaswa kujibidiisha katika kupata maarifa ya usafi (Khatibu, 2003). Usafi humfanya mtu kuheshimika katika jamii.

Pia, katika diwani ya *Chini ya Mwembe*, msanii ametumia sitiari kuonesha umuhimu wa ubunifu katika kufanya kazi mbalimbali. Ubunifu kutenda jambo kwa namna yenye kuongeza ufanisi tofauti na utendaji wa awali uliozoeleka. Ubunifu katika utendaji wa kazi huleta manufaa yenye tija kubwa katika uzalishaji mali na uchumi. Kwa kiasi kikubwa, kupungua kwa ubunifu katika shughuli za uzalishaji mali na uchumi kumechangia umaskini katika ngazi ya familia, jamii na taifa. Kutokana na ubunifu kuwa mdogo, zaidi ya 40% ya Watanzania wanatumia chini ya shilingi 2000 kwa siku (Dongier, 2015). Katika shairi la *Mkangafu*, msanii anaeleza:

Abiria wameshuka, watathmini safari,
Shauku imewatoka, ima faima si ari,
Gari lao mkangafu, limetititia topeni.

Halirudi haliendi, ni ngoma ya kimasai,
Isobadili ufundi, yachosha na kukinai,
Gari lao mkangafu, limetititia topeni (uk. 22).

Katika beti hizo, msanii ametumia sitiari inayosema ‘Gari lao mkangafu... ‘na’ ... Ni ngoma ya Kimasai’ kulinganisha gari lililochakaa na ngoma ya Kimasai. Ngoma ya Kimasai haina kawaida ya kubadilishwa midundo ama namna ya kucheza. Hupigwa na kucheza kwa namna moja wakati wote. Kutokana na kukosekana kwa ubunifu, jamii inashindwa kupiga hatua yoyote ya kimaendeleo. Hata hivyo, hali hiyo inasababishwa na wasimamizi kukosa maono, kushindwa kuthubutu kufanya mambo mapya, uzito wa viongozi kutoa maamuzi na taasisi kuwa ulazima wa kutoa maamuzi. Pia, kukosekana kwaushirikiano imara, ubunifu na motisha kwa wafanyakazi na hakuna bajeti kufanikisha ubunifu (Fungavyema, 2019). Ubunifu ni silaha kubwa ya kutatua changamoto mbalimbali zinazoikabili jamii. Pia, nikichocheo cha maendeleo

endelevu katika jamii (Kibiki, 2011). Ubunifu unapokosekana huchangia kwa kiasi fulani jamii kuishi katika maisha ya umaskini.

3.3 Tashibiha

Tashibiha ni neno lenye maana ya kufanana au kulingana na kuwa sawasawa na kulandana (Kuhenga, 1977). Tashibiha ni mtindo wa kiuneni wa kifani ambapo kitu kimoja au zaidi hulinganishwa au kufananishwa na kitu au vitu vingine tofauti. Tashibiha ni aina ya tamathali ya ufananisho au mlinganisho wa vitu viwili au zaidi. Katika tashibiha, kuna vitu vitatu vinavyofananishwa ambavyo wataalamu wameviita kizungumzwa, kifananishi na kiungo. Tashibiha ni usemi unaolinganisha vitu viwili kwa kutumia viunganishi kama vile kama mithili ya, kana kwamba na mfano wa. Tashibiha ni tamathali ya semi ambayo huunganisha vitu viwili au zaidi kwa kutumia viunganishi (Wamitila, 2003). Hii ni mojawapo ya nyenzo zinazotumiwa kupitisha dhamira.

Katika diwani teule, waandishi wametumia tashibiha ili kumwelekeza msomaji na jamii kwenye uhalisi wa masuala mbalimbali. Mojawapo ya masuala hayo ni pamoja na uozo uliopo katika jamii. Uozo huu umesababishwa na kukosekana kwa maadili yanayokubalika katika jamii (Barasa, 2015). Uozo unasababisha jamii za nchi maskini hususani katika Afrika kuishi kwa chuki na uhasama mkubwa miongoni mwao. Uozo huu, kwa kiasi kikubwa, umechangiwa na baadhi ya tabia za viongozi wasiotimiza wajibu wao kwa jamii. Uozo uliopo katika jamii unasababisha Waafrika kuishi kwa roho mbaya baina yao na hata kudhulumiana. Baadhi yao wananyang'anyana vitu vyao kwa nguvu na kusababisha jamii kuishi kwa visasi visivyoisha kila siku. Katika diwani ya *Wasakatonge*, msanii anaeleza katika shairi la *Kansa*:

Imekuwa ni donda, donda lisolitibika,
Limeanza kuvunda, kuvunda kupasuka,
Lanuka kama ng'onda asokauka.

Ni ndwele kama kansa, kansa isiyo tiba,
Kutibu kwake hasa, hasa chuma cha shaba,
La sivyo itatesa si haba (uk. 4).

Katika beti hizi, msanii ametumia tashibiha mbili aliposema 'Lanuka kama ng'onda asokauka' na 'Ni ndwele kama kansa isiyo tiba'. Mshairi ametumia

tashibiha hizi kuonesha uozo uliopo katika jamii. Msanii anaiona jamii namna ilivyogubikwa na masuala mengi yanayokosa maadili. Uozo mwingi unaotokea Afrika kutokana na kukosekana kwa utu na ukiukwaji wa maadili yanayohitajika katika jamii zetu (King'ei, 2002). Uozo mkubwa uliopo katika jamii yetu ni pamoja na rushwa, ubaguzi, uzembe, ubadhilifu na kukosekana kwa haki. Viongozi wa kisiasa, kidini hata wa kimila wanayo nafasi kubwa ya kuondoa uozo uliopo katika jamii. Jamii yenye mpasuko wa kutokupendana haiwezi kupiga hatua yoyote kimaendeleo.

Katika diwani ya *Chini ya Mwembe*, tashibiha imetumika kusisitiza jamii kuishi kwa upendo na kuacha tabia za kusengenyana. Tabia ya kusengenyana imesababisha jamii kuishi kwa uhasama. Kusengenyana ni kumsema mtu kwa mabaya wakati hayupo. Kusengenyana ni kumzungumza vibaya mtu asiyekuwepo hata kama hayo yanayozungumzwa juu yake ni kweli (Ambrose, 2017). Tabia ya kusengenyana aghalabu husababishwa na watu kukaa bila kufanya kazi. Kusengenyana ni tabia ambayo hufanywa na wanawake na wanaume, ingawa wanawake ndiyo huongoza kwa usengenyaji zaidi (Masoud, 2018). Ili kupata ufanisi mkubwa katika nyanja mbalimbali za maendeleo, jamii inapaswa kuishi kwa upendo na kudumisha mshikamano miongoni mwao kwa kujiepusha na masengenyano. Katika shairi la *Maneno*, msanii anaeleza:

Mashavu yamewatuna, kama chura mwenye mimba,
Midomo inagongana, kama ngoma ya sindimba,
Ndimi zinadanadana, maneno kuumbaumba,
Kama maneno ni sumu, ningeshakufa zamani (uk. 46).

Katika shairi hili, msanii ametumia tashibiha 'Mashavu yamewatuna kama chura mwenye mimba' na 'Midomo inagongana kama ngoma ya sindimba'. Tashibiha hizi zinatoa rai kwa jamii kuacha tabia ya kusengenyana. Tabia ya kusengenyana imejikita kila mahali, kuanzia nyumbani, mitaani, ofisini, shuleni na vyuoni (Ngugi, 2018). Tabia hii ya kusengenyana inaweza kuachwa kwa jamii kujikita zaidi katika kufanya kazi. Jamii inapaswa kutumia muda mrefu katika kufanya kazi badala ya kukaa vibarazani na kuzushiana maneno ya fitina.

3.4 Methali

Methali huelezea wazo fulani lililokusudiwa kwa jamii kwa kifupi na kwa muhtasari. Kimuundo, methali huwa na pande mbili, upande mmoja huanzisha

jambo au wazo fulani na upande wa pili hujibu au kukamilisha sehemu ya kwanza. Kwa kawaida, methali ni utanzu tegemezi ambao kutokea kwake hutegemea tanzu nyingine kama maongezi, majadiliano na hadithi (Hussein, 2018). Kutokana na umuhimu wa utanzu huu kwa jamii, methali zinaendelea kufundishwa katika ngazi mbalimbali za elimu hapa nchini hasa katika taaluma ya fasihi. Kutokana na kufundishwa kwake katika ngazi mbalimbali za elimu, wanafunzi hupata maarifa kuhusu mambo mbalimbali yanayohusu historia jamii yao, asili yao, mila na desturi zao pamoja na taratibu za maisha katika jamii (Njogu na Chimera, 1999). Methali ni tamathali muhimu sana kutokana na kufuatilia kwa karibu maisha ya jamii ya kila siku.

Washairi wametumia methali kama mbinu ya kuwasilisha dhamira mbalimbali kwa jamii. Katika diwani ya *Chini ya Mwembe*, mshairi ametumia methali kuionya jamii kuachana na masuala ya tamaa mbaya. Tamaa mbayani matarajio ya kupata kitu ambacho hustahili au huna uwezo nacho. Baadhi ya wanajamii wamepatwa na matatizo mengi kutokana na kuwa na tamaa mbaya. Tamaa mbaya huleta madhara makubwa kwa mwanadamu (Mohamed, 1990). Tamaa ya kuwa na vitu vingi nje ya uwezo wa mtu aghalabu huleta madhara makubwa kwa mhusika. Katika shairi la *Acha Kujishebedua*, msanii anaeleza:

Acha kujishebedua,
Utakuja teketea, kwa kupenda kunyotoa,
Yakhe acha kunyapua, bure wajiharibia,
Mtaka nyingi nasaba, hupata mingi misiba (uk. 34).

Katika shairi hili, mshairi ametumia methali inayosema ‘Mtaka nyingi nasaba, hupata mingi misiba’. Methali hii imetumika kuionya jamii kujiepusha na tamaa mbaya. Tamaa mbaya inaweza kumtia mtu katika hatari kubwa katika maisha yake. Jamii iinuke na kupingana na aina zote za tamaa mbaya. Kila mtu anapaswa kulinda mawazo yake, mwili wake na utu wake dhidi ya mashambulizi ya tamaa (Mills, 2015). Tamaa mbaya miongoni mwa wanajamii imeondoa umoja na mshikamano miongoni mwao. Wanajamii wengi, hususani vijana wamekuwa na mwisho mbaya wa maisha yao kutokana na kuendekeza tamaa mbaya katika mapenzi, mali na mafanikio katika nyanja wasizokuwa na uwezo nazo (King’ei, 2002). Baadhi ya wanajamii wamejikuta wakipata maambukizi ya magonjwa hatari kama vile UKIMWI na kusababisha kupoteza nguvu kazi za taifa. Tamaa ya utajiri wa haraka imesababisha watu wengi

kutapeliwa. Tamaa mbaya imekuwa ni moja ya vikwazo vikubwa vya maendeleo katika jamii yetu ya leo.

Katika diwani ya *Chini ya Mwembe*, msanii ametumia methali kuhamasisha jamii kufanya kazi kwa bidii. Bidii katika kazi huleta matokeo chanya katika maisha ya jamii. Jamii inapokosa bidii katika kazi ni vigumu kukamilisha mipango yake iliyojiwekea (Kibao, 1972). Mipango yoyote ya jamii haiwezi kufanikiwa kama wanajamii wake hawafanyi kazi. Jamii ikifanya kazi kwa bidii ni lazima itapata mafanikio. Katika shairi la *Mwangwi wa Uhuru*, msanii anaeleza:

Hangelijua, mgaagaa na upwa singalikula wali mkavu,
Kwa kuwa ni juha, akaonekana mstahilimivu kwa kula mbivu,
Japo sura zinafuraha lakini moyoni wana maumivu,
Jahazi likajitia mwangwi kuizuia, likapasuka kwa nguvu (uk. 134).

Katika shairi hili, msanii ametumia methali inayosema, ‘mgaagaa na upwa singalikula wali mkavu’. Methali hii inaihimiza jamii kufanya kazi kwa bidii na kuepuka tabia ya uvivu. Mtu anayefanya kazi hujipatia riziki bali mvivu na asiyefanya kazi huandamwa na shida na umaskini. Mtu anayefanya kazi kwa bidii huheshimika katika jamii. Kufanya kazi ni mojawapo ya falsafa za jamii ya Kiafrika zilizojenga mizizi imara ya uwajibikaji (Hassan, 2013). Kutokufanya kazi na kuendekeza uvivu ni kwenda kinyume na maadili yanayokubalika katika jamii.

Katika diwani ya *Chini ya Mwembe*, msanii ametumia methali kusesitiza umuhimu wa kutimiza ahadi. Ahadi ni agano analotoa mtu kwa mwenzake na ni sharti kutimiza (Jackline, 2016). Wajibu wa mwanajamii ni kuhakikisha kuwa wanatimiza ahadi walizoweka. Kuna baadhi ya viongozi ambao si waadilifu kwani hutoa ahadi za uwongo na zisizotekelezeka. Wengi hutoa ahadi zenye kuwarubuni wananchi kwa malengo yao ya kisiasa. Katika shairi la *Zawadi YanguKwako*, msanii anaeleza:

Khanga pia kugaiwa, fulana hata kofia,
Na fedha tukaachiwa, sote tukafurahia,
Tukazidi kupagawa, nyimbo tukawatungia,
Akili za kuambiwa, tuchanganye na za kwetu.

Miongo ikasogea, ahadi zikayeyuka,
 Tukabaki kushangaa, vile tulohadaika,
 Wageni wakaingia, rasilimali kuteka,
 Akili za kuambiwa, tuchanganye na za kwetu (uk. 89).

Katika nukuu ya shairi hili, msanii ametumia methali isemayo, ‘*Akili za kuambiwa, tuchanganye na za kwetu*’. Hapa msanii anaitaka jamii kuchuja ahadi zinazotolewa na viongozi wao. Viongozi na wanajamii wote wanapaswa kuhakikisha kuwa, kabla ya kutoa ahadi ni wajibu wao waweze kupima kama wanaweza kutimiza ahadi, vinginevyo, ni vema kuifuta ahadi hiyo. Wanajamii wanapaswa kuchambua ahadi zenye tija kwao kwa manufaa ya muda mrefu na zenye maslahi mapana kwa jamii nzima kutoka kwa viongozi wao. Kwa kiongozi mwadilifu na hata mwanajamii, kukosa kutimiza ahadi humkosesha furaha (M’ngaruh, 2019). Viongozi wanapaswa kutimiza ahadi walizotoa ili kujijengea heshima na kukubalika katika jamii.

3.5 Misemo

Misemo ni maneno yenye upana na hutumiwa kuelezea matamko au kauli zinazoelezea ukweli fulani. Msemu ni usemi ambao hutumiwa kutambulisha mazingira maalum au kuijulisha hadhira wakati unaohusika katika kazi ya fasihi inayoshughulikiwa. Matumizi ya misemo katika kazi za fasihi hushabihiana sana na yale ya methali. Misemo huwa na ujumbe mbalimbali (Senkoro, 2011). Misemo ni dhana ambayo hutumiwa kuelezea tungo ambazo hutupatia picha, ishara na tamathali katika kuelezea kitu au wazo kwa ufupi ili kuiadilisha na kuionya jamii. Hutambulisha mazingira, hadhira na wakati unaohusika katika kazi ya fasihi inayoshughulikiwa.

Misemo husaidia sana katika kuibua hisia za msomaji na kuelezea dhamira (Okemwa, 2017). Misemo ni fungu la maneno lililofumbata maana kimafumbo ambayo imekusudiwa kutoa mafunzo kwa jamii. Misemo huwa na dhima ya kueleza ukweli fulani wa maisha ya jamii husika. Misemo huzuka na kutoweka kufuatana na hali mbalimbali za kimazingira za jamii husika na hali yake ya matumizi.

Misemo ni chombo chenye kuchochea maendeleo katika jamii. Katika diwani ya *Wasakatonge*, msanii ametumia misemo kuihimiza jamii kufanya kazi kwa

bidii na kujiepusha kufanya kazi kwa ulegevu. Kazi ni shughuli inayohusisha akili au nguvu za mwili kwa lengo la kufikia kusudi au kupata matokeo yaliyokusudiwa (Calium, 2018). Matokeo yanayotarajiwa hayawezi kufanikiwa endapo jamii itafanya kazi kwa uvivu. Katika shairi la *Mcheza hawi kiwete*, msanii anaeleza:

Ngoma yataka matao, huchezwa kwa kudemka,
Kwa maringo na pumbao, mwili wote kunyumbuka,
Haichezwi kama bao, kwa mwezako kupangika,
Mcheza hawi kiwete, ngoma yataka matao (uk. 32).

Katika shairi hili, msanii ametumia misemo ‘*Mcheza hawi kiwete* na *Ngoma yataka matao*’. Misemo hiyo imetumika kuihimiza jamii kufanya kazi kwa bidii. Bidii huchochea maendeleo katika jamii (Silau, 2013). Kufanya kazi kwa uvivu husababisha umaskini katika jamii. Kufanya kazi kwa bidii huisaidia jamii kupiga hatua kimaendeleo. Kuna manufaa makubwa ya kufanya kazi kwa bidii. Manufaa hayo ni pamoja na jamii kuheshimika, kufanikisha kukamilika kwa mipango iliyopangwa, kuepusha lawama na kuboresha maisha ya jamii na taifa zima. Mtu mwenye bidii hujitesa kwa muda mfupi lakini matokeo yake huwa ni mazuri na ya muda mrefu (Maanga, 2020). Jamii inapaswa kufanya kazi kwa bidii na maarifa na si kama kwa kulazimishwa katika kujiletea maendeleo.

Katika diwani ya *Chini ya Mwembe*, mwandishi ametumia misemo kuonesha suala la demokrasia katika jamii. Demokrasia ni mfumo wa serikali ambapo wananchi wote ni sawa mbele ya sheria na wanashiriki katika kufanya maamuzi ya kitaifa juu ya masuala ya umma (Wikipedia, 2020). Katika utawala wa kidemokrasia viongozi hutegemewa kuongoza kwa ridhaa ya wananchi wote bila ubaguzi. Demokrasia maana yake ni nguvu ya wengi katika kufanya maamuzi yanayohusu umma na kuweka usawa (Bjuremalm na wenzake, 2016). Pia, inategemewa kuleta na kudumisha haki za watu kujieleza bila kuingiliwa. Katika jamii za kiafrika, kuna ukiukwaji mkubwa wa demokrasia kabla na baada ya kupata uhuru wa bendera. Mara tu baada ya Waafrika kushika hatamu za uongozi, tabaka lililokuwa katika hatamu za uongozi lilianza kukiuka misingi ya kidemokrasia (Massoud, 2018). Viongozi wakaanza kuwatesa wananchi kwa kuwanyima haki zao za msingi. Katika shairi la *Chini ya Mwembe*, msanii anaeleza:

Nipo chini ya mwembe,
 Wamekata ulimi, wamekata mikono,
 Hawana tena usemi, imebaki minong'ono,
 Wameshapoteza ndimi, yamekwisha malumbano,
 Ningali chini ya mwembe, wamenipora maneno (uk. 39).

Katika shairi hili msanii ametumia misemo, 'Wamekata ulimi, wamekata mikono' na 'Wameshapoteza ndimi'. Misemo hii imetumika kuonesha kukosekana kwa uhuru wa kujieleza na kufanya kazi. Nchi nyingi za Kiafrika hazina utawala wa kidemokrasia. Katika Bara la Afrika, baadhi ya wenye mamlaka hutumia vibaya mamlaka yao kwa kukiuka kanuni za kidemokrasia (Adero, 2005). Licha ya katiba ya nchi nyingi za Kiafrika kuingiza baadhi ya vipengele vya kidemokrasia kama vile uhuru wa kujieleza na kufanya kazi katika katiba zao, bado utekelezaji wake umekuwa ni mdogo. Demokrasia ni lazima iwape wananchi uwezo wa kujieleza na kuwasilisha hoja zao kwa utaratibu mzuri unaowafikia wawakilishi wao. Viongozi wa serikali wamekuwa wakitumia vyombo vya dola kuhakikisha kwamba wananchi hawawezi kujieleza na kutoa maoni yao. Demokrasia inapokosekana, chuki huimarika dhidi ya viongozi na serikali yao na hata miongoni mwa wananchi wenyewe.

4.0 Hitimisho

Makala hii imechunguza jinsi matumizi ya lugha yanavyoibua dhamira katika ushairi wa Kiswahili kwa kurejelea diwani ya *Wasakatonge* (2003) na *Chini ya Mwembe* (2017). Mjadala wa data zilizowasilishwa katika makala hii umeonesha namna kipengele cha lugha kinavyoibua dhamira katika diwani za jamii teule. Vipengele vya lugha vilivyowasilishwa vilikitwa katika mazingira, historia na utamaduni wa jamii ya mwandishi iliyochunguzwa. Kwa ujumla, lugha na dhamira ni vipengele viwili vinavyotegemeana na kukamilishana katika kazi ya fasihi.

Marejeleo

Adero, M. C. (2005). Uwezo wa Lugha katika Matini ya Siasa Nchini Kenya Kuanzia Mwaka 2002 Hadi 2005. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Ali, D. M. (2017). Kuchunguza Maudhui ya Nyimbo za Kampeni za Uchaguzi

- Mkuu Zanzibar 2000-2010. Tasinifu ya Umahiri, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Ambose, K. N., Enock, M., na John, K. (2015). Mwingiliano Matini katika Tamthiliya za Kiswahili: *MashetaninaKijiba cha Moyo* katika *SWAHILI FORUM* 22 (2015): 42-71.
- Bishop, E. (2007). *Schooling and Pastoralists, Livelihoods: A Tanzanian Case Study*. Doctor of Philosophy Thesis, University of London.
- Bjuremalm, H., Gibaja, F. A., na Molleda, J. V. (2016). *Uwajibikaji wa Kidemokrasia Katika Utoaji wa Huduma: Mwongozo wa Kiutendaji Katika Kubainisha Maboresho Kupitia Tathimini*. Stockholm-Sweden: Internal IDEA.
- Calium, M. (2018). Maudhui na Fani katika Tamthiliya za Kiswahili: Utafiti Linganishi wa Tamthiliya za *Mashetani* na *Kivuli Kinaishi*. Tasinifu ya Umahiri, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Dongier, P. (2015). 'Tanzania Haina Ubunifu' katika Mwanahali Online.com. Imesomwa 3/4/ 2021.
- Fungavyema, L. (2019). 'Vikwazo vya Ubunifu' katika Mbunifu-home.blogspot.com. Imesomwa tarehe 19/07/2022, Saa 6:00 Mchana.
- Hassan, A. U. (2013). Dhima ya Methali katika Kudumisha Maadili ya Jamii ya Wapemba. Tasinifu ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Dodoma.
- Jackline, G. B. (2016). Uchanganuzi Linganishi wa Swala la Maadili kwa Vina wa Kiume katika Tenzi Mbili: *Siraji* na *Adili*. Tasinifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Jesse, M. J. (2017). 'Itikadi katika Riwaya za Said Ahmed Mohamed'. Tasinifu ya Shahada ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Jilala, H. (2008). *The Artistic Uses of Metaphors in Constructing Meanings and Messages in New Generation Songs in Tanzania*. M. A. Dissertation, University of Dar es Salaam.
- Khatib, M. S. (2003). *Wasakatonge*. Dar es Salaam: Oxford University Press.

- Kibao, S. A. (1972). *Utenzi wa Uhuru wa Kenya*. Nairobi: Oxford University Press.
- Kibiki, E. (2011). 'Umuhimu wa Elimu' katika Tuelimishane-Wazojipya.blogspot.com.
- King'ei, K. (2002). *Miadi ya Uzalendo*. Nairobi: Phonex Publishers.
- Kuhenga, C. (1977). *Tamathali za Semi*. Dar es Salaam: EALB.
- Kyabalishanga, F. H. (2018). "Kuchunguza Sanaa na Dhima za Methali za Wahaya". Tasinifuya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- M'Ngaruth, T. K. (2019). 'Umbuji wa Wahusika katika Ushairi wa Kiswahili: Mifano Kutoka kwa Diwani ya *Jicho la Ndani* (S. A. Mohamed, 2002)'. Chuo Kikuu cha Embu-Kenya: *East African Scholars Journal of Educational of Education, Humanities and Literature*.
- Madumulla, J. (2009). *Riwaya ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Mture Educational Publishers Ltd.
- Mahenge, E. (2009). 'Uchambuzi wa Fani na Maudhui katika Semi Zilizoandikwa katika Tiketi za Daladala' katika *Kioo cha Lugha* Juz. Na. 7, kur. 51-67.
- Maitaria, J. N. (2014). 'Dhima ya Ushairi katika Kuelimisha Jamii Kuhusu Demokrasia' katika *KISWAHILI*, Juz.77, Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Massoud, S. S. (2018). Kutathmini Matumizi ya Mtindo na Dhamira katika Tamthiliya za *Mashetani* na *Mashetani Yamerudi*. Tasinifu ya Umahiri, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Matei, A. K. (2011). *Fasihi Simulizi kwa Shule za Upili*. Nairobi: Oxford University Press.
- Mills, D. H. (2015). *Inamaanisha Nini Kuwa na Baraza Kama Nyoka?* Parchment House.
- Mohamed, S. A. (1990). *Sikate Tamaa*. Nairobi: Longhorn Publishers.

- Mulokozi, M. M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili: Kozi za Fasihi Vyuoni na Vyuo Vikuu*. Dar es Salaam: KAUTTU.
- Ngugi, E. (2018). Maudhui na Mtindo katika Ushairi wa Watoto: Uchanganuzi wa Utenzi wa *Haki za Watoto* na *Mashairi Bulbul*. Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Njogu, K. na Chimera, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Ntarangwi, M. (2004). *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*. Rock Island, IL61 201: Augustana College.
- Nyerere, J. K. (1967). *Ujamaa: The Basis of African Socialism*. Dar es Salaam: Tanganyika Standard.
- Okemwa, M. K. (2017). Mchango wa Fasihi Simulizi katika Fasihi Andishi: Mfano wa Visa katika *Mafuta* (1984) na *Walenisi* (1995). Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Sabasaba, N. (2016). “Tamaa” katika Jitambue TBC Taifa katika facebook.com/jitambuetbc.
- Silau, G. K. (2013). Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Tsuma, S. M. (2014). Uhakiki wa Mtindo katika *Vipanya vya Maabara*. Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publications Ltd.
- Wamitila, K. W. (2008). *Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide Muwa Publishers.

**Uchimuzi wa Fikra za Kijaala katika Ushairi wa
Kiswahili: Mifano Kutoka *Tungizi za Mnyogatwa*
na *Diwani ya Midulu***

Hassan R. Hassan
Chuo Kikuu cha Waislamu cha Morogoro

Athumani S. Ponera
Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere
atponeraman@gmail.com

Ikisiri

Makala hii imechunguza fikra za kijaala zinazosawiriwa katika ushairi wa Kiswahili. Makala imetokana na utafiti wa kimaktaba. Data zilipatikana kwa njia ya usomaji na uchambuzi wa matini mbalimbali na kuchambuliwa kwa kutumia mbinu ya usimbishaji wa maudhui. Matokeo yamewasilishwa na kujadiliwa kwa kutumia nadharia ya Ujaala. Matokeo yanaonesha kuwa diwani teule zilizochunguzwa zimesawiri fikra za kijaala kupitia mianzo na miisho ya mashairi, falsafa kuhusu uwezo wa kutunga mashairi na mielekeo ya vipengele vya kimaudhui vinavyohusu uhai, ndoa, uzazi, ibada na kifo. Makala hii inapendekeza kufanyika kwa uchunguzi zaidi kuhusu uwezo na kiasi cha tanzu nyingine za fasihi ya Kiswahili kusawiri ujaala. Pia, uchunguzi unaweza kufanyika ili kulinganisha uwezo na kiasi cha usawiri wa ujaala kati ya fasihi na tawi lingine lolote la sanaa au baina ya fasihi ya jamii ya Waswahili na ya nje ya jamii ya Waswahili.

Istilahi za Msingi: Uchimuzi, ujaala, ushairi, fikra, falsafa na itikadi.

1.0 Utangulizi

Makala hii inafafanua fikra anuwai za kijaala zinazosawiriwa katika diwani teule za ushairi wa Kiswahili. Ujaala unahusiana na nguvu au kani maalumu inayotawala kuwapa kwa ulimwengu, walimwengu na mambo mbalimbali yanayowahusu. Kani hii iko bayana kwa kila kiumbe razini aliyepo

**MAKALA HALISI
HISTORIA YA
MAKALA**

Kupokelewa: 05 Machi
2022

Kurekebishwa: 15 Juni
2022

Kukubaliwa: 29 Julai
2022

Kuchapishwa: 20
Septemba 2022

ISSN: 2799 – 2187

Juzuu 1,

Toleo 1,

uk. 17 – 33.

NUKUU

Hassan, H. R. & Ponera, A. S. (2022). Uchimuzi wa Fikra za Kijaala katika Ushairi wa Kiswahili: Mifano kutoka *Tungizi za Mnyogatwa na Diwani ya Midulu. Jarida la Fahari ya Kiswahili, 1(1), 17 – 33.*

ulimwenguni. Kietimolojia, neno jaala limetokana na maneno mawili, ambayo ni ‘mja’ na ‘Allah’ (Ponera, 2014). ‘Mja’ maana yake kiumbe, Allah ni neno la Kiarabu linalomaanisha Mungu. Maneno yote haya mawili yananasibishwa na dini ya Uislamu. Hata hivyo, pamoja na istilahi ya ujaala kuchipuka kutoka kwenye muktadha wa dini ya Uislamu, ukweli ni kwamba, kimatumizi, dhana ya ujaala haifungwi tu katika mawanda ya dini hiyo pekee.

Ujaala huweza kuelezwa kwa mielekeo mikubwa miwili, ki-dhana na ki-nadharia (Hassan, 2018). Mwelekeo wa ki-dhana huuelezea ujaala kwa kuegemea katika dhana za falsafa na itikadi. Ujaala kama dhana ya kifalsafa hurejelea undani wa mfumo wa fikra ambao mtu au jamii huuegemea katika kuendesha maisha yao. Ujaala kama dhana ya kiitikadi humaanisha nyenzo ambayo mtu au jamii huitumia kufikia kilele cha mfumo anauegemea (Ponera, 2019). Mwelekeo wa ki-nadharia huuelezea ujaala kama umbo kuu lenye kubeba dhana mbalimbali, pamoja na uelekeo wa kifikra unaotokana na mkusanyiko wa misingi husika.

Dhana ya ujaala ilikuwepo hata kabla ya kuzaliwa kwa Kristo. Matalani, fikra hizi zinaonekana kupitia wanafalsafa wa mwanzo wa Kiyunani kama vile Sokrates Sophroniscus, Aristocles Ariston Plato na Aristotle Nicomachus (Senkoro, 1987 & Ponera, 2010). Katika uga wa fasihi, mawazo ya kijaala yanaanza kujitokeza kwenye nadharia zinazoelezea chimbuko la fasihi. Mojawapo ya nadharia hizo inaeleza kuwa chimbuko la fasihi ni Mungu. Wafuasi wa nadharia hii wanaamini kuwa Mungu ndiye msanii mkuu aliyeuumba ulimwengu kwa usanii wa ajabu. Nadharia hiyo inamwona mwanadamu kama zao la Mungu. Pia, inaamini kuwa chimbuko la sanaa ni jazba inayompata msanii. Mawazo haya yanafungamana na dhana ya ujaala ambayo inaamini kuwa kila jambo linalomfika binadamu hukadiriwa na Muumba wake mwenye uwezo wa kuyaendesha maisha yake.

Mawazo haya ya kijaala yaliendelea kuwaathiri wasomi wa mwanzo wa Kiyunani, hasa Hesiod na Plato (Mulokozi, 2017). Katika fasihi na maisha ya Waswahili, mawazo haya yameendelea kujitokeza kupitia fikra za wataalamu kama vile Nkwera (1976). Mlaga (2017) anabainisha kuwa mawazo ya namna hii yanajitokeza hata sasa katika jamii ya Wasukuma nchini Tanzania ambapo manju huaminika kupata uwezo wa kuimba kutokana na kuchanjiwa dawa za

asili. Wamitila (2003) anadai kuwa ujaala ni mtazamo wenye misingi ya kidini. Izingatiwe kuwa, dhana ya dini hapa inatumika kurejelea imani yoyote ambayo kiumbe razini wa ulimwengu huu huifuata au huwa nayo kuhusu kani inayoongoza mustakabali wa kuwapo kwake. Akishadidia hoja hii, Hameed (2011) anasema:

Waislamu ulimwenguni kote huishi katika wingu la ujaala na kutokuwa na hakika kuhusu yatakayowatokea katika nyakati zijazo. Wakati Kurani pia imeweka msisitizo katika uhuru wa maamuzi pamoja na mienendo ya kimaadili ya mtu binafsi na kijamii, fikra na matendo yao kwa kawaida ni ya kijaala sana (uk. 21).

Ingawa imani kuhusiana na ujaala ina misingi ya kidini, lakini huwa na tofauti katika kuiendea kati ya jamii moja na nyingine. Tofauti hii hutokana na kila jamii kuwa na itikadi yake. Tofauti hiyo haiwi kwa ngazi ya jamii tu, bali hata baina ya mtu na mtu. Mathalani, kuna baadhi ya jamii huamini kuhusu uwepo wa Mungu na nyingine huamini kuhusu miungu, mizimu na vitu vingine kama vile miti, mapango, hirizi na majabali. Imani zote hizo huwaelekeza katika kuitakidi kuwa kuna kani inayowaongoza katika maisha yao. Kani hiyo huwa mtu hawezi kushindana wala kupingana nayo.

Jamii za Wayunani zilikuwa zikiamini katika Mungu na miungu mbalimbali iliyokuwa ikiwasaidia katika mambo yao. Cuddon (1998) anabainisha kuwa *Muse* ni jina lililorejelea Mungu yeyote kati ya miungu tisa ya Wayunani ambayo ni watoto wa *Zeus* na *Mnesmosyne*. Miungu hiyo ilikuwa na mgawanyo katika kutawala aina mbalimbali za sanaa. Katika mgawanyo huo, kuna *Calliope* (Mungu wa ushairi na tendi), *Clio* (Mungu wa historia), *Urania* (Mungu wa unajimu) na *Erato* (Mungu wa ushairi wa mapenzi). Pia, kuna *Euterpe* (Mungu wa ushairi wa tumbuizo), *Melpomene* (Mungu wa tanzia), *Polyhmnia* (Mungu wa ushairi wa kusifu Miungu), *Terspsichone* (Mungu wa dansi) na *Tnalia* (Mungu wa ufutuhi).

Ponera (2014) anaitaja miungu mingine iliyoaminiwa na jamii ya Wayunani na Warumi kuwa ni *Saturnalia* (Mungu wa mazao au mavuno), *Cupid* (Mungu wa mapenzi), *Aesculapius* (Mungu wa dawa), *Minerva* (Mungu wa uwindaji) na *Samnus* (Mungu wa usingizi). Kwa ujumla, miungu hawa walihusishwa na

matukio yaliyokuwa yanawatokea wanajamii. Pia, Wayunani walikuwa wakiamini katika utabiri kuhusiana na maisha yao (Brondsted, 2007). Utabiri huo ulikuwa sanjari na nguvu za miungu yenye dhima hiyo. Miungu hao walibashiri jinsi mtu atakavyozaliwa, mahali atakapozaliwa, namna atakavyoishi, jinsi atakavyokufa na sehemu atakapofia. Thomas (2011) anaongezea kuwa Wayunani wa kale walikuwa wanakwenda kwa waaguzi kwa lengo la kuuliza na kujulishwa kuhusu habari za jaala au kudra zao. Hata hivyo, kwa lolote waliloambiwa, ilikuwa vigumu kwa mtu kubadilisha yaliyopangwa na miungu anayohusiana nayo.

Kwa upande wa jamii za Waafrika, fikra za kijaala ziliegemezwa katika miungu ya mizimu. Murphy (2003) anadokeza kuwa Waafrika walikuwa na imani zao zilizoamini Mungu, miungu na mizimu. Miungu hiyo iliheshimiwa, kuthaminiwa na kuenziwa. Mungu aliutawala ulimwengu kupitia miungu na mizimu iliyokuwa ikiwajibika kwa mambo muhimu ya jamii kama vile uzazi, kilimo, mvua, kuponywa maradhi na kuondoa balaa. Mulokozi (1997) anatoa mfano kwa kutaja miungu mbalimbali walioaminiwa na kuabudiwa na watu wa jamii ya Wakiziba. Mungu wao mkuu ambaye ni muumbaji wa nchi na anga ni *Ruhanga*. Ruhanga alikuwa na miungu waliomsaidia ambao ni *Mugasha* (Mungu wa ziwa, upepo na mvua), *Lweru* (Mungu wa Ziwa Viktoria), *Nyakalembe* (Mungu wa kilimo), *Kasana* (Mungu wa uwindaji na ardhi), *Irungu* (Mungu wa mapori), *Lyang'ombe* (Mungu wa wafugaji), *Kaithura-Nkuba* (Mungu wa radi na dhoruba) na *Rugila* (Mungu wa uzazi).

Hivi sasa, imani ya ujaala imechukua mwelekeo mpya kwa baadhi ya watu Barani Afrika, hususani baada ya kuja kwa wageni kutoka Mashariki ya Kati (Waarabu) pamoja na Ulaya (Wazungu). Licha ya mambo yao mengine, wageni hao waliasisi na kueneza dini za kigeni (Uislamu na Ukristo) Barani Afrika. Kuja kwa dini hizi kumebadili mtazamo huu wa ujaala kwa kuwaelekeza watu wake kuamini juu ya 'Mungu Mpya'. Tofauti hii ya kiimani miongoni mwa wanajamii kuhusiana na dhana ya ujaala, bado haiwatoi katika duara la kuamini kuhusiana na kani inayoongoza maisha yao. Wote huelekeza imani zao kuwa ipo kani yenye nguvu inayowaongoza binadamu, vyote vilivyomo pamoja na matukio yanayowakumba hapa ulimwenguni.

Imani kuhusu ujaala imekuwa ikiwawezesha wanajamii kuishi katika hali ya utu, uadilifu, hofu na kuridhika juu ya mambo yote yanayowakumba. Hali hii hutokana na jamii kuamini kuwa yote yanayotokea yanasababishwa na kani hiyo inayomtazama muda wote (Chacha, 1992). Katika ushairi wa Kiswahili, fikra za kijaala zinaonekana kujitokeza katika kazi za watunzi mbalimbali. Mlaga (2017) anasisitiza kuwa jambo hili litaendelea kuwepo maadamu watu wataendelea kuwa na imani juu ya kuwapo kwa Mungu. Makala hii imechunguza fikra za kijaala zinazosawiriwa katika ushairi wa Kiswahili.

2.0 Mbinu za Utafiti na Nadharia

Makala hii imechunguza fikra za kijaala zinazosawiriwa katika ushairi wa Kiswahili. Makala imetokana na utafiti wa kimaktaba. Data za msingi zilipatikana kutoka katika diwani teule za *Tungizi za Mnyagatwa* na *Diwani ya Midulu*. Njia ya usomaji na uchambuzi wa matini ilitumika kupata data zilizolengwa na kuchambuliwa kwa kutumia mbinu ya usimbishaji wa maudhui. Matokeo yamewasilishwa na kujadiliwa kwa kutumia Nadharia ya Ujaala. Waasisi wa Ujaala kama mkabala wa kushughulikia sanaa ni wataalamu wa Kiyunani, Plato na Aristotle. Wananadharia hawa wanatazama jaala kama kani isiyoelezeka, nasibu na isiyo ya kibinafsi inayoamua matokeo ya matukio fulani (Wamitila, 2003). Pia, wanaamini kuwa kama jambo limepangwa kutendeka, haiwezekani kujaribu kuliepuka au kuliathiri kwa namna yoyote ile. Wanaongeza kuwa, matukio yote katika historia ya ulimwengu pamoja na visa vya maisha ya kila siku hukatiwa shauri na jaala au majaaliwa.

Nadharia hii inasisitiza kuwa maisha ya kila binadamu hayana budi kuufuata mkondo fulani ambao umepangwa na kani asiyoweza kuidhibiti. Mawazo ya wataalamu hawa yanatumulikia mihimili ya nadharia ya Ujaala. Mosi, vitu na mambo yote yaliyopo hapa duniani yamesanwa na Mungu. Pili, kila kiumbe ana fikra za kuwepo kwa kani asiyoweza kupambana nayo popote atakapokuwa. Tatu, juhudi za binadamu haziwezi kudhibiti wala kukwepa matukio yanayomtokea. Nne, maisha ya duniani ni nukta ndogo sana ya duara zima la maisha ya wanadamu. Mihimili hii tuliitumia katika ukusanyaji, uchambuzi na mjadala wa data zilizowasilishwa katika utafiti uliofanyika.

3.0 Fikra za Kijaala Zilizosawiriwa katika Diwani Teule

Mshairi wa diwani zilizotafitiwa amesawiri fikra za kijaala kwa kujiegemeza katika mambo matatu. Mambo hayo ni mianzo na miisho ya mashairi, falsafa

kuhusu uwezo wa kutunga mashairi na mielekeo ya vipengele mbalimbali vya maudhui.

3.1 Mianza na Miisho ya Mashairi

Namna ya kuanza na kumaliza kazi ya kifasihi ni miongoni mwa masuala ya kifani. Washairi wa Kiswahili wamekuwa wakiomba dua na baraka kutoka kwa Mungu ili awape uwezo wa kufanikisha walichokiazimia kukiwasilisha. Pia, mwishoni mwa utungo humshukuru kwa kuwezeshwa kufanikisha. Vionjo wanavyotumia katika kuomba na kushukuru huko ni kutaja majina mbalimbali ya Mungu na kumsalia Mtume. Hali hii huonekana katika tenzi na mashairi ya watunzi wanaofuatilia dini zote, ingawa walio wengi ni wale wanaofuatilia dini ya Uislamu (Shariff, 1988 & Chacha, 1992).

Mshairi ambaye diwani zake zilitafitiwa amesawiri fikra za ujaala mwanzoni na mwishoni mwa baadhi ya mashairi yake. Mifano ya mashairi yaliyoanza kwa kusawiri fikra za kijaala. Mwandishi anaeleza:

Bismillahi naanza, kwa jina lake Manani,
Allahu ndiye wa kwanza, akhera na duniyani,
Muumba mwenye kufunza, ya pepo na ya motoni,
Kwake zetu shukurani.

(Shairi la *Allah*, uk. 23).

Wa kuanza kutajika, ni Allahu msifika,
Katujaliya kufika, vitini twajikaliya,
Wajibu wetu wa pili, kumuomba Rasuli,
Yeye na zake ahali, rehema kuwafikiya.

(Shairi la *Karibu Mgeni Wetu*, uk. 62).

Mifano hii michache inayakinisha hoja kuwa mshairi anasawiri fikra za kijaala mwanzoni mwa mashairi yake. Katika mifano hii, Mungu anatangulizwa kwa kusifiwa, kuombwa na kutajwa kwa majina kama vile Allahu, Muumba, Mola na Manani. Pia, mshairi anamwomba amani Rasuli (Mtume Muhammad). Mshairi amefanya hivi ili kuendeleza kaida maarufu ya kumtegemea Mungu katika utungaji wa kazi mbalimbali za ushairi wa Kiswahili. Kwa upande wa miisho, fikra za kijaala zimebainika katika mashairi ya *Umri Wazidi Kwenda* (Diwani ya *Tungizi za Mnyagatwa*) na *Juzi si Jana ni Leo* (Diwani ya *Diwani ya*

Midulu). Katika ubeti wa mwisho wa shairi la *Umri Wazidi Kwenda*, mshairi anasema:

Nimefika kituoni, namshukru Swaburu,
Kwani Sengo ana nini, nina Mwenyezi na nuru,
Umri nauthamini, mmiliki ni Ghafuru,
Nyinyi mwajifanya huru, hesabu zi Qiyamani (uk. 210).

Katika mifano hii, mshairi anamshukuru Mungu ambaye anamtaja kwa majina ya Swaburu (Mwenye subira), Mwenyezi (Mmiliki wa zama zote), Ghafuru (Mwenye kusamehe), Mola na Mpaji (Mwenye kutoa). Majina na mawazo haya yanaonesha namna mshairi anavyosawiri thamani ya kani ya Mungu katika maisha yake. Hizi ni fikra za kijaala.

3.2 Falsafa Kuhusu Uwezo wa Kutunga

Kiini cha falsafa hii ni kumuona mshairi kama mtu maalumu aliyeruzukiwa na Mungu kipaji cha kutunga mashairi. Ushairi huonwa kama sanaa yenye upekee ambayo inahitaji mtu mwenye kipawa ili aweze kuisana. Kwa hiyo, si kila mtu anaweza kuwa mshairi mzuri (Abedi, 1965 & Nassir, 1979). Mshairi wa diwani mbili zilizotafitiwa anaamini kuhusu Mungu kuwa chanzo cha uwezo wake wa kusana tungo za kishairi. Mshairi anashadadia hoja hii katika *Tungizi za Mnyagatwa*:

Tungizi hizi kwa wema utakaonekana umo, si wa mtu, si wa jamii bali ni nyunyizi, mawaga, chechezi za Uungu wake *Allah* (s.w) ampaye mtu tusomjuwa, ampaye kitu tusichokijuwa. Lionekalo la hovyoy, mtunzi hakulikusudia kwani uwovu ni wa Iblis, na sina urafiki naye (uk. 241).

Maelezo hayo yanadhihirisha bayana fikra za kijaala. Mtunzi ana yakini moyoni mwake kuwa mashairi aliyoyatunga yana hadia kutoka kwa Mungu ambaye ameyanyunyuzia cheche za Uungu wake. Dondoo linatusisitizia kuwa kama kuna ovu litakaloonekana katika mashairi hayo, basi ni la ibilisi ambaye mtunzi hana urafiki naye.

3.3 Mielekeo ya Maudhui ya Mashairi Yake

Mshairi amewasilisha mawazo mbalimbali yenye mwelekeo wa kusawiri ujaala katika diwani zake mbili zilizotafitiwa. Makala hii imeyasinyaza mawazo hayo katika makundi mbalimbali. Baadhi yake ni uhai, ndoa, uzazi, maradhi na kifo.

3.3.1 Uhai

Uhai ni hali inayomwezesha kiumbe kuishi duniani. Uhai ni kinyume cha ufu. Wanaujaala wanaamini kuwa uhai huanzishwa, hudhibitiwa na kutamatishwa na Mungu. Kila kiumbe huwa na muda maalumu wa kuishi hapa duniani (Hassan, 2018). Katika jitihada za kuthamini uhai na kuona kuwa ni hidaya ambayo mja amekirimiwa na Mungu, watu wamekuwa wakimshukuru Mungu muda wote kwa kuwajaalia kuendelea kupumua mpaka muda huo. Mshairi wa diwani teule amezungumzia uhai kwa kutumia fikra za kijaala. Katika diwani ya *Tungizi za Mnyagatwa*, kuna shairi la *Allah* linalosawiri fikra za kijaala. Katika ubeti wa tatu, mshairi anasema:

Nasi tuzidi ibada, ndugu zangu sikizeni,
Uhai si wa kubweda, ni mwingi wa mitihani,
Kina kaka kina dada, tuwache ya ujanani,
Kwa *Allah* ndiko rejeyo (uk. 218).

Mshairi anaikumbusha jamii kutojisahau na uhai walionao kwa sababu ni mali ya Mungu. Anaikumbusha zaidi kwamba kila chenye mwanzo kina mwisho. Hivyo, watu wautumie uhai wao vizuri kwa kumcha Mungu ambaye kila kiumbe hapa duniani kitarejea kwake. Fikra hii inaumana vyema na mhimili wa Nadharia ya Ujaala kuwa maisha ya duniani ni nukta ndogo sana ya duara la maisha ya wanadamu.

Pia, katika shairi la *Al-Hamdu-Lillah!*, mshairi anamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kumjaalia uhai na afya njema. Pia, anaikumbusha jamii kuhusu kumcha Mungu pamoja na wazazi wawili, baba na mama. Ubeti wa sita wa shairi hili unaizindusha jamii kuhusiana na suala la kuumbwa kwao, uhai walionao, pamoja na yote wanayotendewa na Mungu hapa ulimwenguni. Mshairi anasema:

Uumbizi na uhai, uzima pamwe huduma,
Ni zaidi ya jinai, tukisahau ya nyuma,
Bora kujirairai, dini si ya nyumanyuma,
Wa pili baba na mama, *Ali-hamdulillah!* (Uk. 226).

Katika ubeti huu, mshairi anausawiri uhai kwa kuuegemeza katika fikra za kijaala kuwa Mungu ndiye mwenye mamlaka nao. Mshairi anaiambia jamii kuwa ni kosa la jinai kusahau namna ya kuumbwa kwao, aliyewaumba, uhai

wao pamoja na huduma zote wanazotendewa na aliyewaumba (Mungu). Hivyo, anaitaka jamii kujibiidisha katika kuishika dini.

3.3.2 Ndoa

Ndoa ni mkataba wa hiyari baina ya mwanamke na mwanamume kuishi pamoja kama mume na mke. Kuo au kuolewa ni jambo la lazima kwa mtu aliyefikia umri unaokubalika na jamii husika. Ulazima huo unatokana na haja za maumbile ya mtu binafsi pamoja na haja za mazingira ya ulimwengu unaomzunguka (Sengo, 2008). Kila jamii ina taratibu zake za kuiendea ndoa. Zipo jamii zinazojigeza katika misingi ya dini za kijadi kwa kufanya ibada maalumu ya kuwaombea maharusi kabla na baada ya ndoa.

Pia, zipo jamii zinazozingatia mafundisho yaliyomo kwenye vitabu vitakatifu vya dini za Ukristo na Uislamu, yaani Biblia na Kurani mtawalia (Hassan, 2018). Makala hii inalinasibisha suala la ndoa na fikra za kijaala kutokana na imani waliyonayo wanajamii kuwa ‘Ndoa hupangwa mbinguni’, yaani, hupangwa na Mungu. Kila mmoja anapoingia katika umri wa kuo au kuolewa huomba Mungu amjaalie mke au mume bora wa kudumu naye maishani. Katika diwani ya *Tungizi za Mnyagatwa*, kuna shairi la *Mirathi* linalohusianisha suala la ndoa na kani ya Mungu. Mshairi anasema:

Nikazipiga sigida, nyingi za kuomba mke,
Dua nyingi nizigida, kupata aso makeke,
Nikampata Seyyida, yatima mpwekepweke (uk. 49).

Katika ubeti huu, mshairi anadhihirisha imani yake kuwa alikithirisha sala na dua kwa Mungu ili ampatie mke mwema na, hatimaye, dua lake likakubaliwa na Mola kwa kumpata mke mwema. Pia, katika diwani hiyohiyo kuna shairi la *Wake Zangu* linalodhihirisha fikra za kijaala kuhusiana na ndoa. Mshairi akimshukuru Mungu kwa kumjaalia kuo, anatoongoa hivi:

Namshukuru Manani, kunijaliya kuowa,
Fatuma wa Udigoni, Songeya alikozawa,
Tukutana Mngotini, ambako alilelewa,
Si tajiri masikini, kwa hali alivyokuwa,
Ndiye wa kwanza nyumbani (uk.102).

Mifano hiyo inaonesha jinsi ndoa inavyohusishwa na mawazo ya kijaala. Watu wamekuwa wakimuomba Mungu awajaalie kupata wenza wema ambao wataungana nao katika kuyajenga maisha. Kitendo hiki cha mwanadamu kumuelekea Mungu katika mambo yake kinadhihirisha wazi kuwa matendo, nia na mustakabali wa maisha yake hapa ulimwenguni yanaamuliwa na jaala.

3.3.3 Uzazi

Uzazi ni jambo ambalo binadamu hatuna uwezo nalo. Katika jamii ya Waswahili, uzazi huchukuliwa kuwa jambo la majaaliwa ambalo linaidhinishwa na Mungu (Sengo, 2008). Jambo hili linadhihirika pia kupitia semi za Kiswahili kama vile kuolewa ni sheria, kuzaa majaaliwa. Msingi mmojawapo wa ujaala unatuelekeza kuwa vitu na mambo yote yaliyoko hapa duniani yameumbwa na Mungu. Miongoni mwa mambo hayo ni uzazi. Inapotokea kuwa wanandoa wamekaa muda mrefu bila kujaaliwa watoto, jitihada mbalimbali hufanywa ili kumuomba Mungu. Maombi hayo hufanywa kulingana na itikadi ya wanandoa husika pamoja na ndugu au/na jamaa. Hivyo, huweza kufanywa kwa kuzingatia miongozo ya kijadi, Kikristo au Kiislamu. Shairi la *Ithineni Majaliwa* lililomo katika *Diwani ya Midulu* linaonesha imani ya mshairi katika suala zima la uzazi. Mshairi anasema:

Namshukuru Wahabu, kunijaliya thineni,
Wote kwangu mahabubu, ni tunu mwangu moyoni,
Kwa ndowa za taratibu, kwa radhi yako Manani,
Sikujuwa sikudhani, baba mmoja kwa babu (uk. 20).

Katika ubeti huu, tunamuona mshairi akimshukuru Mungu kwa kumjaalia watoto wawili ambao wamepatikana baada ya kuishi kwa muda mrefu na mkewe wa awali bila kupata mtoto. Mtunzi anaonesha kuwa mwenye uwezo wa hilo ni Mungu. Anabainisha zaidi jambo hili katika ubeti wa tatu. Anasema:

Ishirini ilipita, miyaka mke Fatuma,
Bahati hatukupata, kushika hakukufuma,
Kumbe mambo yamkuta, mahaba ya wake mama,
Si kazi kurudi nyuma, kupata kuna utata.

Baada ya miaka 20 ya kuishi bila kupata mtoto kutoka kwa mkewe wa awali, Bi. Fatuma, mshairi aliwaoa wake wengine wawili, Bi. Zawadi na Bi. Jamillah. Hawa walimpatia watoto wawili, Yusufali na Khalifah. Mshairi anaonesha

imani yake kuwa uzazi hutoka kwa Mungu anapotuambia kuwa kupatiwa watoto wawili siyo makusudi yake, bali ni mapenzi ya Mwenyezi Mungu. Pia, anazidi kuomba dua ili apate watoto zaidi kwa mkewe wa nne, Bi. Sheikha. Ushikamani wa fikra hii unapata nguvu tunaposoma shairi la *Mirathi* (uk. 49) katika diwani ya *Tungizi za Mnyagatwa*. Shairi hilo linaeleza kuhusiana na Mwenyezi Mungu alivyotibu utasa kwa Bi. Jamilah na hatimaye, akamjaza heri kwa kushika ujauzito na kuzaliwa Khalifah. Mshairi anaandika:

Kasilimu kwa khiyari, kabla ndowa kujibu,
Allah kamjaza kheri, utasa akautibu,
Kazaliwa mshauri, Khalifah wetu muhibu.

Mifano hiyo inakazia ukweli wa jinsi dhana ya uzazi inavyofungamanishwa na ujaala. Hali hii ni kwa sababu mwanadamu huamini kuwa mambo yote yameshapangwa na Mungu, hivyo hana budi kuyapokea.

3.3.4 Maradhi

Maradhi ni kitu kinachompata mtu au mnyama na kuathiri afya yake. Fikra za kijaala huhusisha maradhi na Mungu; kwamba, ndiye humpa maradhi mja amtakaye na kumponya amtakaye. Wafuasi wa ujaala wa kijadi huhuhusisha maradhi na Miungu na mizimu; ndiyo maana, mtu anapougua hupelekwa kwa mizimu au waganga ili kuendesha mchakato wa uponyaji. Wafuasi wa ujaala wa kisasa huitakidi kuwa maradhi hushushwa na Mungu. Wafuasi hawa hufuata tiba za hospitalini pamoja na maombezi kutoka kwa wabobezi wa dini ambao hufanya kwa kutumia miongozo ya vitabu vitakatifu. Katika *Diwani ya Midulu*, mshairi anaonesha fikra zake kuhusu fikra za kijaala kuhusiana na maradhi kupitia shairi la *Bwana Mwarabu Saidi*. Anasema:

Tangu upate maradhi, bwana Mwarabu Saidi,
Sijapata kukukidhi, kwa kitu cha ushahidi,
Ila duwa za hifadhi, na pilika za ahadi,
Bwana Mwarabu Saidi,
Pole sana kwa maradhi.

Tiba nikakufanyiya, na safari kujituma,
Leo tutakusomeya, duwa yenye kuzizima,
Allah ataipokeya, maradhi atayazima,
Bwana Mwarabu Saidi,

Pole sana kwa maradhi (uk. 81).

Katika beti hizi mbili, tunamuona mshairi akiamini kuwa maradhi huondoshwa na Mungu kupitia dua. Fikra hizi zinadhihirika pia katika *Tungizi za Mnyagatwa*, kupitia shairi la *Uganga*. Ubeti wa pili una mishororo ifuatayo:

Aliyeumba maradhi, ndiye mwenye lahaula,
Kila tiba ina radhi, Allah hupokeya sala,
Halikidhi halikidhi, hata la kinyamkela,
Ila kwa yake hifadhi, na kubuli zake Mola,
Uganga! (uk. 7).

Mshairi anayakinisha kuwa maradhi yameumbwa na Mungu. Mungu ndiye mponyaji wa maradhi yote kwa kadri atakavyo. Pia, anawashajiisha watu kumwomba Mungu kwa sababu mgonjwa huona baada ya dua yake kukubaliwa.

3.3.5 Kifo

Kifo ni hali ya kiumbe kufikia mwisho wa uhai. Wafuasi wa ujaala wa kijadi huamini kuwa wafu huwa bado wana uhai. Aidha, huamini kuwa watu hawafi bali hujificha. Pia, wanaamini kwamba wafu na walio hai huendelea kuwa na uhusiano wa karibu (Sengo, 1995). Mtazamo wa wafuasi wa ujaala wa kisasa (Ukristo na Uislamu) unahusisha dhana ya kifo na nguvu au mipango ya Mungu. *Biblia Takatifu* inabainisha suala hili katika kitabu cha *Mwanzo*, 3:19 kuwa: ‘Kwa jasho la uso wako utakula chakula, hata utakapoirudia ardhi ambayo katika hiyo ulitwaliwa; kwa maana u mavumbi wewe, nawe mavumbini utarudi’ (Chama cha Biblia cha Tanzania, 1997).

Pia, Kurani inalizungumzia suala hili katika sura mbalimbali. Sura ya 3:186 inabainisha: “Kila nafsi itaonja umauti, na bila shaka mtapewa ujira wenu sawasawa siku ya kiyama. Aliyewekwa mbali na moto na kuingizwa peponi, basi amefaulu na maisha ya dunia hii si kitu ila ni starehe idanganyayo”. Sura ya 21:36 inaeleza: “Kila nafsi itaonja umauti na tutakujaribuni kwa shari na heri, na kwetu mtarejeshwa” (Al-Farsy, 1969).

Kutokea kwa kifo huchukuliwa kuwa ni kutimia kwa maandiko ya Mungu kwa mja wake. Hii ndiyo sababu ya kuwapo kwa kauli kama vile “Kazi ya Mungu,

haina makosa”. Sengo (2008) anaeleza kuwa watu wenye imani kuhusu uwezo wa Mwenyezi Mungu huyatazama maisha kama safari fupi, nzuri na ya haraka. Mtu hupewa nafasi hiyo ya kusafiri ili aweze kuona sehemu tu za mifano ya kila namna kuhusu maisha ya kweli na ya kudumu. Anaongeza kuwa, maisha yote yamejaa majaribu ya namna mbalimbali na, kwamba, maisha si yake.

Matapo yote haya mawili ya ujaala wa kisasa yanaamini kuhusu kuwapo kwa maisha baada ya kufa; ambapo roho ya mfu huhifadhiwa mahali fulani milele na milele. Pia, huamini kuhusu kufufuliwa na kupewa malipo yanayotokana na matendo ya mtu akiwa duniani. Mtu aliyeishi kwa kufuata maamrishi ya Mungu huingizwa peponi na yule muovu huingizwa motoni. Kwa hiyo, kifo kinapotokea, waumini wa kundi hili hufanya jitihada za kumwomba Mungu ili ampokee maiti wao pamoja na kumpa makazi mema huko aendako. Katika diwani ya *Tungizi za Mnyagatwa*, kuna shairi la *Twamtakiya Rehema Dida Wetu Kibokoni* linaeleza fikra hii ya kifo na kuihusisha na ujaala. Mshairi anasema:

Ni Mola ndiye mneni, mwenye kumiliki “Kuni,”
Kila roho qiyamani, tapitiya kaburini,
Kwetu sote mtihani, imesema Quruwani,
Dida sasa yu mavani, na sisi tuko nyumbani.
Nyumbani roho kutokwa, si khiyari ni lazima,
Nafsi ni kama kokwa, mmeya kihimahima,
Uhai wetu kupokwa, katupangiya Rahima,
Twamtakiya rehema, Dida wetu Kibokoni (uk. 94).

Mshairi anaamini kuwa kifo ni kazi ya Mungu na mauti ni mlango ambao kila kiumbe atapitia. Kwa kuwa fikra za ujaala huu huamini kuwa anayekufa hurudi kwa Muumba wake, wanaobaki huzidi kumuomba dua ili maiti apumzishwe mahali pema kama mshairi anaposema, ‘Twamtakiya rehema, Dida wetu Kibokoni’. Katika *Diwani ya Midulu* kuna shairi la *Ramadhani wa Hassan* linaloonesha kuwa fikra ya kifo inafungamana na ujaala. Pia, linabainisha kuwa kifo hupangwa na Mungu na wajibu wa wanaobaki ni kumuomba dua njema maiti wao. Mshairi anasema:

Umetuwaga mwenetu, Ramadhani wa Hassani,
Sungu da udele jetu, umefika kaburini,
Ahadi ya Mola wetu, asiye na mshindani,

Yapozwe yalo mavani, ukapumuwe mwakwetu.

Duwa tunakuombeya, upokelewe peponi,
Mungu atakupokeya, akuweke pa amani,
Adhabu kukufutiya, akutowe madhambini,
Nasi tumo msibani, hatwishi kukuliliya (uk. 49).

Dhana ya kifo, kama fikra mojawapo ya kijaala, inatilia nguvu imani ya wanaujaala kuwa mwanadamu hawezi kuyakwepa matukio aliyopangiwa na Mungu. Matukio mengine kama vile uzee, ajali na maradhi huchukuliwa kama viambata tu vinvavyowezesha tukio hilo kubwa la kijaala kutokea. Ndiyo maana, ijapokuwa mwanadamu hujitahidi katika kujinasua na kifo, mathalani kwa mgonjwa kwenda au kupelekwa hospitali kwa lengo la kupatiwa tiba, lakini Mungu hupitisha kani yake kwa kumtwaa kiumbe wake.

4.0 Hitimisho

Makala hii imebainisha namna fikra za ujaala zinavyosawiriwa katika ushairi wa Kiswahili. Mjadala ulijiegemeza kwenye diwani mbili za *Tungizi za Mnyagatwa* na *Diwani ya Midulu*. Msanii amesawiri ujaala kupitia mambo matatu. Jambo la kwanza ni mianzo na miisho ya mashairi. Mtunzi ameanza na kumaliza baadhi ya mashairi yake kwa kumtaja, kumsifu, kumshukuru na kumwomba Mungu. Jambo la pili ni falsafa kuhusu uwezo wa kutunga mashairi. Diwani zilizotafitiwa zimeonesha kuunga mkono fikra inayoaminiwa na watunzi wengi wa mashairi kuwa ushairi ni sanaa inayohitaji karama maalumu kutoka kwa Mungu.

Jambo la tatu ni mielekeo ya vipengele mbalimbali vya maudhui. Mtunzi amesawiri fikra za kijaala kupitia vipengele mbalimbali. Baadhi yake ni uhai, ndoa, uzazi, maradhi na kifo. Kwa kuwa diwani zilizotumika ni za mashairi anayetokea katika jamii ya Waislamu, ni wazi kuwa kijitapo cha ujaala kilichochukua nafasi kubwa katika makala hii ni ujaala wa Kiislamu. Makala hii inapendekeza tafiti zaidi zifanyike kuhusu mdhihiriko wa ujaala wa matapo mengine katika tanzu mbalimbali za fasihi, uwezo na kiasi cha tanzu nyingine za fasihi ya Kiswahili kusawiri ujaala, kulinganisha uwezo na kiasi cha usawiri wa ujaala kati ya fasihi na tawi lingine lolote la sanaa na kulinganisha mdhihiriko wa ujaala katika fasihi ya jamii ya Waswahili na ya jamii ya nje ya Waswahili.

Marejeleo

- Abedi, K. A. (1965). 'Utangulizi' katika Mnyampala, M. *Waadhi wa Ushairi*. Nairobi: East African Literature Bureau.
- Al-Farsy, A. S. (1969). *Tafsiri ya Qurani Tukufu*. Nairobi: The Islamic Foundation.
- BAKIZA, (2010). *Kamusi la Kiswahili Fasaha*. Nairobi: Oxford University Press.
- Brondsted, M. (2007). *The Transformations of the Concept of Fate in Literature*. Oxford: Oxford University Press.
- Chacha, C. N. (1992). *Ushairi wa Abdilatif Abdalla: Sauti ya Utetezi*. Dar es Salaam: Dar esSalaam University Press.
- Chama cha Biblia cha Tanzania, (1997). *Biblia: Maandiko Matakatiifu*. Dodoma: The Bible Society of Tanzania.
- Chuachua, R. (2016). *Falsafa ya Riwaya za Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi katika Mukadha wa Epistemolojia ya Kibantu*. Tasinifuya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Dodoma.
- Cicero, M. T. (1962). *On Old Age*. (Mh na mf. Andrew Preston). Cambridge: Cambridge University Press.
- Cuddon, J. A. (1998). *The Penguin Dictionary of Literary Terms and Literary Theory 4th Edition*. London: Penguin Books.
- Hameed, S. (2011). Is Islam a Religion of Fatalism? Ilisomwa Aprili 11, 2022 katika <http://www.irfi.org/articles/articles.htm>.
- Hassan, H. R. (2018). Ujaala katika Ushairi wa Kiswahili: Mifano Kutoka *Tungizi za Mnyagatwa na Diwani ya Midulu*. Tasinifu ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Dodoma.
- Mlaga, W. (2017). *Misingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Fasihi Karne ya 21*. Dar es Salaam: Heko Publishers Ltd.
- Mulokozi, M. M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: KAUTTU Limited.

- Mulokozi, M. M. (1997). *Utenzi wa Nyakiiru Kibi*. Morogoro: Ecol Publications.
- Murphy, G. L. (2003). *African - American Faith in America*. Oxford: Oxford University Press.
- Nassir, A. (1979). 'Dibaji' katika *Utenzi wa Mtu ni Utu*. London: Macmillan Education Ltd.
- Nkwera, F. M. V. (1976). "Fasihi" katika *Uandishi wa Tanzania* (Mh. J. M. Mbonde). Nairobi: East African Literature Bureau.
- Origen, A. (1960). *On First Principal*. (Mh., na mf., A. O. Robert). London: George Fox University Press.
- Ponera, A. S. (2019). *Misingi ya Utafiti wa Kitaamuli na Uandishi wa Tasinifu*. Dodoma: Central Tanganyika Press.
- Ponera, A. S. (2014). *Utangulizi wa Nadharia ya Fasihi Linganishi*. Dar es Salaam: Karljamer Print Technology.
- Ponera, A. S. (2010). Ufutuhi katika Nathari za Shaaban Robert: Maana Yake, Sababu za Kutumiwa na Athari Zake kwa Wasomaji. Tasinifu ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Dodoma.
- Sengo, T. S. Y. (2010). *Diwani ya Midulu*. Dar es Salaam: Al-Amin Education and Research Academy.
- Sengo, T. S. Y. (2009). *Tungizi za Mnyagatwa*. Dar es Salaam: Al-Amin Education and Research Academy.
- Sengo, T. S. Y. (2008). *Tafakuri ya Utu na Uhai*. Dar es Salaam: Huda Publishers.
- Sengo, T. S. Y. (1995). "Itikadi katika Jamii za Kiswahili" katika *Lugha, Utamaduni na Fasihi Simulizi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.
- Senkoro, F. E. M. K. (1987). *Fasihi na Jamii*. Dar es Salaam: Press and Publicity City.
- Shariff, I. N. (1988). *Tungo Zetu*. Trenton: The Red Sea Press Inc.

Thomas, R. (2011). “Taswira ya Nyoka katika Ngano za Kiswahili: Mifano Kutoka Milima ya Usambara”. Tasnifu ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Books.

Nyimbo za Asili Zinavyoimarisha Mafunzo ya Jadi nchini Tanzania

Deus Gracewell Seif
Chuo Kikuu Huria cha Tanzania
deusgs@yahoo.com

Ikisiri

Makala hii imechunguza dhamira za nyimbo za Wakaguru katika kujenga na kuimarisha mafunzo ya jadi nchini Tanzania. Data za msingi za makala hii zilikusanywa uwandani kwa kutumia mbinu za mahojiano na usaili. Utafiti ulifanyika uwandani katika mkoa wa Morogoro, wilaya ya Gairo. Utafiti uliozaa makala hii umebaini kuwa dhamira za nyimbo za Wakaguru hutumiwa kama ghala maalumu lililosheheni taarifa na maarifa yaliyopo katika jamii. Nyimbo hizo zinasaidia kuifunza jamii masuala ya utamaduni, siasa na uchumi wa jamii hiyo kutoka kizazi kimoja hadi kizazi kingine. Misingi ya mila, desturi, falsafa, historia na maendeleo yao yanarejelewa katika vipengele vingi vya maisha yao ya jadi. Pia, hutumika kama kiungo thabiti cha kiasili kinachojenga mfumo wa kuifunza, kuiimarisha na kuiweka jamii pamoja katika misingi ya utamaduni na falsafa nzima ya maisha tangu kale mpaka sasa. Makala hii inapendekeza kuwa ufundishwaji wa fasihi za jadi utolewe na taasisi husika na zifanyiwe tarajama kwa ajili ya vizazi vilivyopo na vijavyo. Pia, serikali itunge kanuni kali za kudhibiti matumizi ya fasihi za kigeni zisizoendana na uhalisi wa mazingira ya kiasili, zikiwemo kanda za picha za utupu.

Istilahi za Msingi: Nyimbo za kiasili, nyimbo za Wakaguru na mafunzo ya Jadi.

1.0 Utangulizi

Makala hii imechunguza dhamira za nyimbo za Wakaguru katika kujenga na kuimarisha mafunzo ya jadi nchini Tanzania. Dhamira ni ile jumla ya maana

MAKALA HALISI HISTORIA YA MAKALA

Kupokelewa: 04 Machi
2022

Kurekebishwa: 26 Juni
2022

Kukubaliwa: 29 Julai
2022

Kuchapishwa: 20
Septemba 2022

ISSN: 2799 – 2187

Juzuu 1,
Toleo 1,
uk. 34 – 53.

NUKUU

Seif, D. G. (2022). Nyimbo za Kiasili Zinavyoimarisha Mafunzo ya Jadi Nchini Tanzania. *Jarida la Fahari ya Kiswahili*, 1(1), 34 – 53.

anayoivumbua mwandishi anapoandika na anayoitambua msomaji au msikilizaji (Kinge'i, 2002). Tunaweza kuivumbua maana ya kazi fulani kwa kuisoma au kuisikiliza kazi hiyo. Dhamira ni sehemu ya maudhui yanayotuelekeza katika shabaha inayobainika tangu mwanzo hadi mwisho wa kazi ya fasihi. Pia, ni mojawapo ya vipengele vinavyojenga maudhui katika kazi ya kifasihi. Maudhui katika kazi ya kifasihi hujumuisha vipengele vingi. Baadhi yake ni dhamira, falsafa, mtazamo, msimamo, migogoro na ujumbe (Wamitila, 2008). Makala hii imechunguza kipengele cha dhamira kinachojitokeza katika nyimbo za jamii ya Wakaguru.

Kihistoria, Wakaguru walianza kujulikana kama kabila kabla ya ujio wa Wakoloni miaka ya 1800 (Silau, 2013). Jamii hiyo inapatikana Mashariki ya Himaya ya Wagogo kwenye milima ya Itumba. Kuna historia simulizi inayoeleza kuwa jamii ya Wakaguru imetokana na muunganiko wa makabila matatu makubwa ya Wanguu, Wasagara na Wagogo, hasa katika eneo la Gairo (Sengo, 2009). Jamii hiyo ilianza kujulikana zaidi kuanzia 1876 baada ya Wamisionari wa dhehebu la Kianglikana kutoka Uingereza kuweka makao yao eneo la Mamboya katika Wilaya ya Gairo (Belidemen, 1997). Gairo inasemekana kuwa ndio asili ya jamii ya Wakaguru. Jamii hii ni mojawapo ya makabila madogo nchini Tanzania.

Jamii ya Wakaguru ina utaratibu uliozoeleka unaoongoza taratibu zote zinazohusu maisha ya kila siku ya jamii. Utaratibu huo ni mapokeo ya vizazi vingi katika jamii hiyo. Kiongozi mkuu wa jamii hiyo aliitwa *Mndewa*. Maamuzi makubwa ya uongozi yalitemgemea Mndewa. Mndewa ndiye mwenye madaraka na ndiye kituo cha mwisho katika masuala ya kiutawala, kimila na kisheria. Pia, alisimamia shughuli zote za kijamii kama vile kumaliza msiba, tohara, unyago, tambiko, mizimu na sherehe za mavuno (Wizara ya Elimu, 2011). Pia, huongoza mikutano ya masuala ya kijamii, sala na matambiko ya jamii. Nguvu za utawala wa jadi katika jamii hiyo zinaendelea kudhoofika kutokana na kuimarika kwa mifumo ya kisasa ya uendeshaji wa serikali.

Tangu awali, jamii ya Wakaguru ilishughulika na shughuli za ufugaji na kilimo. Wakaguru wanathamini sana mila na desturi za jamii yao. Mila na desturi ndio msingi wa malezi na makuzi kwa vijana (Nzobe, 2012). Mila hizo ni pamoja na

matambiko, tohara kwa wanaume, unyago kwa wanawake, ujenzi wa nyumba, kilimo, ufugaji na kuabudu. Shughuli nyingi za jamii hiyo ziliegemezwa katika misingi imara ya mila na desturi katika uendeshaji wake. Mpaka sasa vipo viashiria vya jamii hiyo kufuata mila na desturi zake. Mathalani, kuwepo kwa *jenga* (kiongozi) wa kuongoza mapambano na vita. Jenga ni mtu maalumu wa kutoa dawa kwa ajili ya kuwakinga vijana wakati wa vita. Imani hiyo bado inaendelea katika vijiji vya Idibo, Iyogwe, Italagwe na Makuyu.

Kisanaa, namna ya kudokeza anayofikiria mtu katika jamii ya Wakaguru ni kuimba. Pia, tanzu za hadithi, vitendawili, methali na misemo hutumika. Matukio ya kila siku huelezwa kupitia nyimbo. Nyimbo hutumika kama chombo thabiti kinachojenga mafunzo kuhusu maisha, malezi, tabia, mila na desturi za jamii (Wizara ya Elimu, 2009). Jamii hupata mafunzo mbalimbali kupitia katika tanzu za misemo, vitendawili, hadithi na methali. Nyimbo za jadi ni mojawapo ya vyombo vinavyopewa uwanja mpana wa kutekeleza shabaha ya masuala mbalimbali katika jamii. Makala hii imechunguza dhamira za nyimbo za Wakaguru katika kujenga na kuimarisha mafunzo ya jadi.

2.0 Mbinu za Utafiti

Makala hii imechunguza dhamira za nyimbo za Wakaguru katika kujenga na kuimarisha mafunzo ya kijadi nchini Tanzania. Utafiti ulifanyika katika mkoa wa Morogoro, wilaya ya Gairo katika vijiji vya Majawanga na Mkalama (Kata ya Mkalama), Luhwaji na Msingisi (Kata ya Msingisi), Sanganjelu na Madege (Kata ya Madege) na Makuyu na Italagwe (Kata ya Italagwe). Maeneo hayo yaliteuliwa kwa kuwa yana mawanda ya kutosha yaliyosheheni data zilizolengwa ili kukidhi malengo ya makala hii. Mapitio ya nyaraka zilizotumika kufafanua data za msingi za makala hii zilipatikana kwa kudurusu nyaraka mbalimbali kutoka katika maktaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Maktaba hiyo iliteuliwa kwa kuwa ina data za kutosha zilizohusiana na mada ya makala iliyoshughulikiwa.

3.0 Mafunzo ya Jadi katika Nyimbo za Wakaguru

Fasihi ni usawiri mkamilifu ambao huyasawiri maisha kwa undani na huyachunguza kwa mtazamo mpana (McNiff, 1992). Nyimbo za jamii ya Wakaguru zilichunguzwa kama kiungo maalumu cha mahusiano ya kijamii kwa kuzingatia historia yake, falsafa yake, utamaduni wake, uchumi wake na siasa

zake. Mtafiti alitumia maarifa hayo kuchunguza namna nyimbo za jamii hiyo zinavyobeba misingi inayolenga kujenga na kuendeleza mafunzo ya kiasili. Mafunzo ya dhamira za nyimbo hizo yamejikita katika vipengele mbalimbali vya maisha ya kila siku ya jamii kama yalivyoelezwa katika sehemu inayofuata.

3.1 Matumizi ya Tiba za Asili

Katika kuenzi asili, utamaduni ni kama moyo wa taifa. Nyimbo za kijamii ni miongoni mwa vielezea halisi vya asili vya kijamii vinavyojishughulisha na masuala ya tiba za asili katika jamii. Nyimbo za Wakaguru zimesheheni maelezo ya matumizi ya tiba asili kama vile mizizi, majani, magome, matunda yake, pamoja na viungo vya wanyama vinavyotumika kutibu na kuimarisha afya za wagonjwa wanaohusika. Tiba asilia ina chimbuko lake linalotofautiana baina ya mtumiaji mmoja na mwingine (Mwangosi, 2019). Mwanajamii anaweza kurithi masuala ya uganga na tiba asilia kutoka kwa wazazi wake, walezi wake, ndugu zake na jamaa zake. Wapo pia wanaoeleza kuwa kuoteshwa na mizimu. Wapo wanaojifunza kwa kunuia ama kuinunua taaluma husika kulingana na mahitaji binafsi au jamii zao. Vyanzo vya maarifa ya taalimu hiyo ni vingi mno katika jamii za Kiafrika.

Fasihi simulizi ni miongoni mwa vyombo vinavyohakiki mienendo na harakati za jamii inayohusika. Pia, husawiri kwa undani masuala ya kuwepo kwa matumizi ya tiba asilia yanayoendelea katika jamii nyingi hapa nchini, ikiwamo jamii ya Wakaguru. Fasihi simulizi kupitia utanzu wa nyimbo imekuwa ikieleza na kuhimiza matumizi ya tiba za asili, wajibu wake na kutoa mafunzo kuhusu jinsi bora ya kuzitumia. Maelezo haya yanazingatia na kurejelea matumizi ya dawa za asilia na uzoefu wa mfumo wa maisha ya jamii ya kiasili kwa kurejelea kutamalaki kwa mazoea ya utamaduni wa jamii husika. Kuwepo kwa matumizi ya dawa asilia ni sehemu kamili ya mila na desturi za jamii nyingi zilizopo hapa nchini.

Katika jamii ya Wakaguru, wapo waganga wa tiba za asili wanaojishughulisha kwa namna mbalimbali. Miongoni mwao ni kuwepo kwa wataalamu wa tiba za binadamu, ukunga na uzazi, mifugo na mazindiko. Wapo pia wanaofanya kazi kama waamuzi wa masuala yanayohusu utamaduni wa jamii kwa kushirikiana na viongozi wa jadi wa eneo linalohusika. Dawa za asili zinazotumika kutibu magonjwa kwa kipindi kirefu kilichopita mpaka sasa na kuendelea. Dawa hizi

zinatokana na rasilimali asili zinazopatikana katika mazingira yetu hususani mimea kama vile mwarobaini, ambao ni moja ya mimea inayotumika kama tiba asilia ya kuponya magonjwa. Wasanii katika wimbo wa *Miti ya Katali* (Tiba Asilia) wanaeleza:

<i>Ikalamu nikulonda,</i>	Kalamu ninachukua,
<i>Asili niikuilonga,</i>	Asili kuelekea,
<i>Ni imwengele iswamu,</i>	Mwarobaini sawi,
<i>No miti yetu ya katali,</i>	Ndiyo dawa maridhawa.

<i>Milela mpaka mahamba,</i>	Mizizi hata majani,
<i>Ni miti yetu ya jadi,</i>	Ni dawa ilo thamani,
<i>Ikuhonya kabisa,</i>	Hutobaki taabani,
<i>Na sinhamu sidukile.</i>	Kwa magonjwa yalo sugu.

Maelezo katika wimbo huu yanaonesha kuwa tiba asilia zina mchango mkubwa sana katika jamii za hapa nchini na Afrika. Licha ya kukumbana na changamoto ya utamaduni kutoka nchi za Kimagharibi ambapo baadhi ya jamii huendeleza kutumia dawa za asili zinazotazamwa kama hazina kemikali (Ngadala, 2003). Aidha, kuna haja ya kutumia dawa za asili ili kudumisha afya na maendeleo ya afya za jamii kwa sababu dawa hizo hazina kemikali na hata kuzipata kwake hakuhitaji kiasi kikubwa cha fedha na upatikanaji wake ni rahisi. Dawa za asili ni bora na hazina madhara yanayoweza kusababishwa na kemikali.

Tiba asili ni sehemu kamili ya uponyaji wa mtu kwa kutumia mitishamba inayotuzuguka katika mazingira yetu. Kwa kiasi kikubwa, watu hutumia dawa za kisasa kwa kuamini kuwa ni bora kuliko dawa za asili. Matumizi ya dawa za asili yanasibishwa na kutoleta madhara yoyote kwa mtumiaji kwa sababu hazichanganywi na kemikali zinazoweza kuibua magongwa mengine kwa mtumiaji (Kisanji, 2012). Pia, wasanii wameeleza kuhusu madhara ya utumizi wa dawa za kisiasa yanayotoka katika jamii za Mashariki na Magharibi kwani hutengenezwa kwa kemikali zinazoathiri afya. Tiba za asili zilizotumiwa toka enzi za zamani huwa ndizo muhimu kama wasanii wanavyoeleza katika wimbo huohuo wa *Miti ya Katali* (Tiba Asilia):

<i>Afya swamu ni nghongelo,</i>	Afya bora ni mtaji,
<i>Mitishamba ni dhahabu,</i>	Miti shamba ni dhahabu,
<i>Ina singufu za katali,</i>	Yenye nguvu za asili,

Ikuleusa sumu mumwili. Hutoa sumu mwilini.

Maelezo katika wimbo yanaonesha namna tiba za asili zilivyo na thamani ukilinganisha na dawa za kisasa. Dawa za asili hazina sumu katika matumizi yake zikilinganishwa na utumiaji wa dawa za kisasa. Hata hivyo, ni vizuri ieleweke kwamba tiba za kisasa zichukuliwe kama tiba mbadala ili kuimarisha afya kwa wagonjwa kwa sababu baadhi ya maradhi yanaweza kutibika kwa urahisi kwa kutumia dawa za kisasa au za asili. Makala hii inatoa wito wa kutokupuuza matumizi ya dawa za kisasa na za asili. Kila dawa ina umuhimu wake kutegemeana na maradhi yaliyopo katika jamii.

Katika jamii ya Wakaguru, tiba asilia hutazamwa kama tiba mbadala dhidi ya zile za kisasa zinazotoka katika jamii za Magharibi na Mashariki ya dunia. Waimbaji wanahimiza kuidumisha na kuendeleza utaalumu wa taaluma hiyo kutokana na upana wa dhima zake. Uzito unachukuliwa kuwa baadhi ya magonjwa yanayoshindikana katika hospitali za kisasa hutibiwa kwa urahisi na kwa gharama nafuu kwa kutumia tiba asilia. Wataalamu wa tiba asilia wanatoa tiba mbadala kwa kutibu maradhi sugu yanayoshindikana katika hospitali za rufaa zilizosheheni hapa nchini. Wasanii katika wimbo wa *Chinghauleke* (Tiba Mbadala) wanaeleza:

<i>Miti za katali,</i>	Dawa za asili,
<i>Miti za kulewa wakulu,</i>	Dawa za tangu jadi,
<i>Miti ya jadi adhimu,</i>	Tiba mbadala adhimu,
<i>Waganga wa miti za jadi,</i>	Waganga wa tiba asilia,
<i>Watalamu mbadala,</i>	Wataalamu mbadala,
<i>Wakuhonja nhamu nyingi,</i>	Hutibu maradhi mengi,
<i>Wakuhonya nhamu nyingi,</i>	Huponya wengi,
<i>Chinghauleke.</i>	Tuezienzi!

Fungu hili linaonesha umuhimu wa kuwepo kwa dawa za asili na wataalamu wake wanachukuliwa kama waganga wa tiba mbadala katika jamii nyingi hapa nchini na kwingineko barani Afrika. Katika jamii nyingi zilizo nje ya mji, hasa za vijijini, wataalamu hao wanategemewa sana katika masuala yote yanayohusiana na ukunga na uzazi na kuzima magonjwa ya mlipuko (Mwangosi, 2016). Tiba asili hutazamwa kuwa zina gharama nafuu na ni rahisi kupatikana. Pia, hazina madhara ambayo ni matokeo ya kuwepo kwa kemikali

katika dawa za viwandani. Dawa asilia hutibu maradhi mengi, hata yale yaliyoshindikana katika hospitali za kisasa.

Waganga wanaorejelewa katika utafiti sio madaktari na wauguzi waliosomea hospitalini. Hawa ni wale wa mitishamba waliotamalaki hasa vijijini. Waganga hao hutibu kwa kutumia mimea inayoota milimani, jangwani, makondeni na misituni. Wataalamu hao kwa weledi wao, hupaendea hapo ilipo wapate kuichimba na kuichuma. Wataalamu hao, hawana budi kufanya kazi zao kwa ukamilifu, uaminifu, uadilifu, weledi na misingi bora taaluma zao adimu na adhimu. Hii ni kwa sababu tiba za asili husaidia kutibu maradhi mengi yaliyoshamiri katika jamii. Wanajamii wanakumbushwa kuenzi utamaduni wa asili na falsafa zao kwa manufaa ya jamii na taifa.

3.2 Malezi

Suala la malezi bora ya watoto linapewa mkazo na msukumo mkubwa kuanzia ngazi ya familia katika jamii ya Wakaguru. Wakaguru wanashirikiana kwa hali na mali ili kuwalea, kuwatunza na kuwajenga katika misingi sahihi, imara na bora ya kimaadili na kiutamaduni. Watoto wanaangaliwa kuwa ni mali ya wanajamii katika jamii hiyo. Licha ya ukweli kuwepo kwa mtazamo huo, wasanii wa nyimbo za Wakaguru wanampa nafasi ya pekee mwanamke kuwa ni nguzo kuu na imara kwa malezi ya familia katika jamii hiyo. Mwanamke anategemewa kuijenga familia yake katika misingi bora ya kiutamaduni na kimaadili. Kutokana na umuhimu huo, waanawake wanapaswa kuwekewa mikakati imara ya kuwajengea nguvu inayolenga kuzimudu harakati zao za kiutamaduni, kimaadili na kimalezi.

Katika jamii nyingi malezi ni jambo la msingi, hasa katika kuwalea vizuri watoto katika maezi yalio bora. Malezi bora ni yale ambayo baba na mama wanawalea kwa pamoja watoto wao ili wawe na tabia njema. Watoto wana haki ya kupata mahitaji yao muhimu kama vile chakula, mavazi, elimu, kuwakinga na kuwatibu kwa maradhi pamoja na kuwajenga katika maadili mema (Mwakanjuki, 2011). Jamii nyingi zinazotuzunguka ziko bega kwa bega katika kuhakikisha kuwa watoto wanakua katika maadili mema na kuwa mfano mzuri hata kwa watu wengine. Jamii zetu za sasa zimeshindwa kuwalea watoto katika maadili mema na kusababishia kuwa na tabia isiyo nzuri kwa jamii na taifa. Wasanii katika wimbo wa *Matunzo* (Malezi) wanaeleza:

<i>Wakulu na walelaji,</i>	Wazazi hata walezi,
<i>Kefa wachulusi,</i>	Mithiri ya waachuuzi,
<i>Wakuleka kuzuia,</i>	Wasokua Wazuizi,
<i>Kwale wanaotunza.</i>	Kwa wanao kuwatunzi.

Wimbo huo unaeleza kuwa kuna umuhimu mkubwa wa kuwalea vyema watoto katika maadili mazuri yanayoweza kusababisha kuwepo kwa maadili mema kwa vijana wa kike kwa wa kiume. Pia, wanaeleza kuwa kuna haja ya kuwalea watoto katika maadili mema ili kuweza kukua katika misingi imara itakayowajengea uwezo wa kuyamudu maisha yao ya baadaye. Malezi ni jambo ambalo wazazi wote wanahusika katika kulifanikisha vyema na inabidi wazazi wote washirikiane kwa pamoja katika kuwalea vyema watoto wao. Wazazi wakishindwa kuwaandaa vizuri, watakuwa mzigo kwa wazazi wenyewe, jamii na taifa.

Malezi bora ya watoto ni nyenzo kuu inayojenga msingi sahihi wa maisha kwa mtoto. Wazazi hatuna budi kutoa uangalizi wa kutosha kwa watoto ili kuweza kuwajenga katika misingi ambayo inakubalika kwa jamii na taifa kwa ujumla (Legulegule, 2016). Katika jamii zetu wazazi wamekuwa na mchango mkubwa katika kutoa malezi kwa watoto wao kwa lengo la kuwawezesha kuishi katika misingi bora ya kimaisha kwa kukemea tabia mbalimbali zisizo za kimaadili kwa jamii kama vile masuala ya wizi na ujambazi kwani tabia hizi zimekuwa ni janga kwa maendeleo ya jamii.

Katika jamii wazazi wamekuwa wakipambana kutaka kutoa elimu kwa jamii zao kwa lengo la kuwajenga watoto waenende katika misingi inayokubalika ili waweze kuishi sawa sawa na matakwa ya jamii inayowazunguka na kwa faida ya maisha yao kwa ujumla. Katika jamii nyingi, malezi ya watoto ni muhimu sana kwasababu huwasaidia watoto kuishi katika misingi mizuri ya maadili kwa kufuata mila na desturi za jamii husika. Basi, wazazi wanawajibu wa kuwapatia malezi bora watoto wao ili waweze kuishi vizuri katika jamii na kuwaasa watoto kujiepusha na mambo yasiyofaa katika jamii. Mfano, wasanii katika wimbo wa *Matunzo* (Malezi) wanaeleza:

<i>Wala sikuseka mahengele,</i>	Hata sichekei ufa,
<i>Kojenga ukuta,</i>	Utaujenga ukuta,
<i>Kwanza sikulangisa sifa,</i>	Wala sitafute sifa,

Kumwanda nghateseke. Mwisho wake utajuta.

Pia, wasanii katika wimbo huu wanaeleza kuwa dunia hii si kapa kwa sababu ina mambo mengi ambayo yanatesa mfano magonjwa mbalimbali. Wazazi hupaswa kuwaeleza watoto kwa kuwapatia malezi mazuri. Kila mzazi anapaswa kuisimamia familia yake vizuri kwa kadri anavyoweza. Usimamizi mzuri utawasaidia watoto kuwajengea uwezo mkubwa wa kumudu maisha yao na mazingira ya wakati wao. Watoto wakiandaliwa vema watakuwa msaada kwa familia, jamii na taifa lao. Dunia ina mengi yanayoweza kuwasonga kama hawatajengewamisingi imara ya kupambana nayo.

Watoto walelewe kwa mujibu wa utamaduni na maadili bora yaliyopo katika jamii. Jamii inaaswa pia kuacha tabia ya kuwanyanyasa, kuwasonga na kuwatumikisha watoto katika shughuli za uzalishaji mali na uchumi kabla ya umri sahihi. Jamii inapaswa kuacha tabia mbaya ya kuwatesa watoto. Watoto waandaliwe kikamilifu kwa kufuata misingi bora ya utamaduni na maadili bora yaliyopo na yanayofaa katika jamii na taifa lao. Watoto watunzwe na kukua kwa manufaa ya ustawi na uendeleu wa kizazi kilichopo sasa na kijacho (Mgogo, 2012). Watoto ni hazina kama wasanii katika wimbo wa *Kulela* (Kulea) wanavyoeleza:

<i>Amaisha unghapange,</i>	Malezi ukiyapanga,
<i>Ukuwenghha mwanga,</i>	Utawajengea mwanga,
<i>Wakuufuta ubwalazi,</i>	Wataufuta ujinga,
<i>Mipango mingi kupanga,</i>	Mipango bora kupanga,
<i>Kuakulu ukonele,</i>	Uzeeni utalinga,
<i>Wanago wakukinga,</i>	Watoto watakukinga,
<i>Ifiswamu saufundigwe,</i>	Vizuri uwaleavyo,
<i>No wana fowakukula!</i>	Ndiyo watoto wakuavyo!

Ubeti huu unaonesha jinsi suala la malezi linavyopaswa kupewa umuhimu mkubwa katika jamii mbalimbali hapa nchini. Malezi yanahitaji umoja na ushirikiano ambao ni wenzo thabiti katika harakati za kuwajenga watoto kimaadili na kimaisha. Dira ya ustawi na uendeleu sahihi wa jamii na taifa lolote katika mataifa ya ulimwengu hutegemea sana kuwepo kwa misingi imara ya uwekezaji kwenye malezi bora na endeleu ya watoto.

Malezi bora na yenye tija kwa watoto yana mchango mkubwa katika kuimarisha misingi ya kimaadili inayotakiwa katika ngazi ya familia, jamii na taifa. Kila mwanadamu hutengenezwa na maadili yaliyopo katika jamii na taifa lake lililomkuza na kumlea. Kila hatua ya maisha ya binadamu ina athari za pekee na za msingi katika jamii na taifa. Kushamiri kwa matendo yasiyo na tija katika jamii nyingi ni matokeo ya kuanguka kwa maadili ya kiasili katika jamii na taifa linalohusika (Paul, 2016). Wajibu wetu ni kujenga misingi imara itakayoziba mianya inayosababisha kudhoofika kwa maadili katika jamii zetu.

3.3. Matambiko

Matambiko, salana sadaka ni njia za kushirikiana na Mungu, mizimu na pepo. Sala zinazoelekezwa kwa Mwenyezi Mungu haziambatani na sadaka isipokuwa kwa mizimu. Sala na sadaka kwa pepo zimeendelea kusahauliwa kwa kuwa taratibu zake hazieleweki ama zimeendelea kufifia sasa (Sengo, 2009). Madhumuni ya sala na sadaka yanatokana na kuharibika kwa taratibu za kawaida za maisha kama vile kupata mavuno haba, kuleta tumaini la mavuno mazuri, kutostawi kwa mifugo, vifo, utasa na ugumba. Pia, hushughulikia magonjwa na matatizo ya kujifungua. Mtu akifuata ushauri kuhusu sala, sadaka, tambiko na dawa anaweza kuona matokeo mazuri kwa wakati muafaka.

Tambiko linahusishwa na kifo cha mnyama, lakini sadaka inahusisha vyakula pamoja na vitu vingine vinavyotolewa ambavyo si lazima uhai utolewe. Pia, linategemea uzito wa tukio ama mwiko uliovunjwa kuhusu uhusiano baina ya Mungu, mizimu na roho kama umeharibiwa (Pembe, 2012). Wakaguru huamini kuwa chukizo lolote haliachwi bila kurekebishwa. Inajulikana wazi kuwa wizi, uchawi na kutokufuata miiko ya jamii ni kosa kwa Mungu na mizimu. Chukizo hilo lazima liondolewe kwa kutambika kwa Mungu au mizimu. Matukio kama ya kukosekana kwa mvua kwa muda mrefu na kuwepo kwa magonjwa ya kuambukiza hujulikana kuwa ni pigo kutoka kwa Mungu. Tambiko hupaswa kufanywa kwa kuelekezwa kwa Mungu. Tambiko huongozwa na chifu baada ya kufanyika kwa mkutano kabla jua halijachomoza. Mkutano wa namna hiyo unalenga kubaini sababu za kutokea kwa hali au matukio yaliyopo kabla ya kufanya tambiko.

Aghalabu ni vigumu kujua kitu kinachotakiwa kutolewa wakati wa tambiko kulingana na kosa lililofanyika. Wapiga bao na watambuzi ndio wanaotakiwa

kusema kitu cha kutoa kwa tambiko au sadaka. Misingi ya kufanya tambiko kwa Wakaguru hulenga kuziba mpasuko uliopo baina ya Mungu na watu, watu na mizimu ambao husababishwa na makosa yaliyokwishafanyika. Makosa hayo husababisha kuvunjika kwa uhusiano na ushirikiano kati ya Mungu, binadamu na mizimu (Mgogo, 2017). Pia, hutambika ili kutaka ushirikiano kati ya Mungu na watu au kati ya watu na mizimu. Kutambika ni njia mojawapo ya kumshukuru Mungu au mizimu kwa ajili ya mema fulani ambayo mtambikaji ameona kuwa ametendewa. Mara nyingi sadaka na matambiko yanatolewa kwa Mungu kwa ajili ya upatanisho, shukrani na kushirikiana na Mungu. Sadaka zinahesabiwa kuwa ni zawadi kwa Mungu kwa sababu kila jambo na mafaniko yote hutokana naye.

Kutambika ni utekelezaji wa ada maalamu ili kutuliza mizimu au pepo mara nyingi matambiko hufanyika kwa kuambatana na kafara. Baadhi ya jamii huweza kutambika kwa kuchinja wanyama na wengine pombe. Wakati mwingine, kafara iliweza kutolewa katika tambiko hutemeana na aina tambiko katika jamii. Tambiko ni sadaka inayotolewa kwa Mwenyezi Mungu, miungu, mizimu na pepo kwao binafsi au kupitia kwa Mwenyezi Mungu wakati wa kusali. Matambiko huweza kurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kizazi kingine. Wasanii katika wimbo wa *Makumbiko* (Matambiko) wanaeleza:

<i>Baho katali za chakuku,</i>	Hapo zamani za mababu,
<i>Chakuku na cha mama,</i>	Mababu na mabibi zetu,
<i>Wejawowa na milungu wao,</i>	Waliabudu sana miungu,
<i>Mabiki gowa uno Ngo.</i>	Miti mawe yalikuwa sehemu.

Matambiko ni sadaka inayotolewa kwa Mwenyezi Mungu au miungu na mara nyingi huambatana na kafara. Katika jamii nyingi za Kiafrika, wazee hasa mababu na mabibi, ndio wenye dhamana ya kutambika kutegemeana na lengo mahususi (Mhegera, 2016). Matambiko ni njia mojawapo ya kutatua matatizo ya kimaisha mila na desturi zao.

Matambiko hujenga na kuimarisha imani kwa watu katika jamii. Kuimarika kwa imani kulikifanya kizazi cha hapo kale kifanikiwe katika masuala ya kijamii. Kwa mfano, jamii ikikosa mvua kwa muda mrefu walikuwa wakitambika na kuomba. Kwa kufanya hivyo, mvua zilikuwa zinanyesha. Mambo haya kwa sasa yamepungua kutokana na kuingia kwa dini mbalimbali. Mfano, Wakristo

huyachukulia matambiko ya jadi kuwa ni shughuli za kishetani na kipepo. Matambiko husaidia kutuliza na kutatua matatizo ya jamii kwa njia ya imani. Pia, hujegwa na imani kama chombo cha kutatulia matatizo yanayoisibu jamii. Matambiko yalionekana kuchukua nafasi kubwa katika jamii katika suala la kuendeleza mila na desturi. Matambiko pia hutumika kuendeleza na kudumisha suala la mila na desturi za jamii husika. Wasanii katika wimbo huo huo wa *Makumbiko* (Matambiko) wanaeleza:

<i>Ikuku yejayanela,</i>	Babu alifurahi,
<i>Mali zake zikiishi,</i>	Mali zake ziliishi,
<i>Mifugo zejajakilela,</i>	Mifugo kujizalisha,
<i>Kukumbika kwejakongesa.</i>	Na kutambika kulichangia.

Wasanii wanaonesha suala la kutambika lilivyokuwa ni sehemu kubwa katika jamii nyingi za Kiafrika hivyo jambo hili lilirithishwa kizazi hadi kizazi kingine. Hapana shaka kuwa matambiko ni sehemu mojawapo ya kuwafundisha vijana kuhusu namna ya kuishi kwa imani na kutegemea nguvu za kimuujiza au miungu. Matambiko huiongoza jamii katika mapambano dhidi ya matatizo yanayoikabili jamii (Rajabu, 2012). Katika jamii nyingi za Kiafrika pia matambiko yana umuhimu kwa sababu yanasimama kama dira ya kupambana na changamoto mbalimbalizinazoikabili jamii. Kwa mfano, ukosefu wa mvua na matatizo ya wanawake kama kutokupata mtoto. Nafasi ya kutambika huwa kama mwongozo ili kuweza kutatua changamoto hizo.

Wasanii wnjariibu kuonesha namna matambiko yanvyosimama kama dira ya kutatua changamoto katika jamii, ukiwemo ukosefu wa mvua na kutokuwepo kwa amani. Jamii inaamua kutambika ili kutatua matatizo hayo. Suala hili lilikuwa na nguvu kubwa upande wa jamii nyingi za Kiafrika kabla ya ujio wa wazungu waliokuja na dini zingine hata kuweza kuingilia imani na utamaduni wa kiafrika. Maendeleo ya sayansi na teknolojia pamoja na utandawazi ambao ndio chanzo kufifia kwa suala la matambiko katika jamii nyingi hapa nchini, ikiwemo ya Wakaguru. Kila kukicha vijana wanazidi kuacha mila na tamaduni zao kwa kuiga mila na tamaduni za kigeni. Kutokana na mabadiliko haya wazazi na walezi wanapaswa kuongeza juhudi ya kuwapatia vijana mafunzo bora yaliyojengwa katika misingi thabiti ya utamaduni wa asili wa jamii zetu za Kiafrika.

3.4 Uke Wenza na Ndoa za Mitala

Uke wenza ni ile hali ya wanawake wawili au zaidi kuolewa na mwanaume mmoja. Katika jamii yetu ya leo suala la uke wenza limekuwa ni jambo la kawaida sana hasa ukizingatia katika upande wa dini ya Kiislamu wameruhusu suala la uke wenza. Hii inasababisha suala hili kuwa ni jambo la kawaida sana katika jamii. Wasanii wa kizazi kipya wamejaribu kufikisha ujumbe kuhusiana na suala hili kupitia kazi zao. Jamii nyingi za watu wa Tanzania, hasa Wasukuma na jamii nyingine wamejikita katika kuoja ndoa za mitala ambapo mwanamume ana mke zaidi ya mmoja. Jambo hili la uke wenza lipo katika jamii yetu na kuweza kusababisha kutokea kwa migogoro katika jamii. Katika wimbo wa *Mfele* (Mwanamke) wasanii wanasema:

<i>Dyangu penzi dinihabwasa,</i>	Langu penzi linapoza,
<i>Gomgonikukusa,</i>	Mume ninakuuliza,
<i>Ikundetela mihali,</i>	Waniletea mke mwenzwa.
<i>Inhole iyo sikuleka,</i>	Hilo penzi sitaweza,
<i>Kwaimo sikuidaha.</i>	Kwa hili sitaweza.

Wanawake wengi hawawezi kuishi katika ndoa za mitala ambapo wanawake wengi hawezi kuishi pamoja na mke mwenzake hasa nyumba moja. Jambo hili lipo katika jamii zetu ambapo tunashuhudia watu wengi wakifikia hadi hatua ya kutoa uhai wa mwezake kisa ndoa hizi za uke wenza. Msanii anaeleza kuwa mwanamke ameshindwa kuvumilia na kutamani aweze kurudishwa nyumbani kwao mwanzo kwa sababu uvumilivu umemshinda wa kuishi pamoja na mke mwenzake. Jambo hili lipo katika maisha yetu ya kila siku na kufikia muda kunakuwa hakuna maelewano mazuri katika familia zao. Jamii inabidi ipige vita ndoa za mitala pamoja na uke wenza katika familia zetu.

Kwa kawaida, uke wenza ni hali ya wanawake zaidi ya mmoja wanaoshiriki na walioolewa na mwanaume mmoja. Uke wenza umekuwa ukisababisha madhara makubwa sana kwa baadhi ya wanawake ambao wamejiingiza katika suala hili (Kiyimba, 2001). Wanawake hawa wanasababisha kuwe na ugomvi kati yao na wengine hufikia hata kuuana. Katika wimbo wa *Mfele* (Mwanamke) wasanii wanasema:

<i>Asai nihungila,</i>	Sasa nimenyongonyea,
<i>Amani ileuka,</i>	Amani imetoweka,

<i>Nisigale kudeseka,</i>	Nabaki kuumia,
<i>Mfele mkulu kunitisha,</i>	Mke mkubwa kunitishia.
<i>Sikubesa mihali.</i>	Sikashifu uke wenza.

Nukuu hii inaonesha kuwa suala la uke wenza linasababisha watu kutoaminiana na kutoweka kwa amani ambapo inakuwa ni kikwazo kikubwa cha uzalishaji, hasa kiuchumi; wanawake hawa huishia kugombania mume. Asilimia kubwa ya wanawake kwenye jamii yetu wanaishi kwenye familia za uke wenza na imeshazoeleka kununiana, kulaumiana na kulumbana mara kwa mara. Matatizo ya uke wenza wakati mwingine yanasababishwa na mwanamume kushindwa kumudu mahitaji ya msingi ya kindoa na kifamilia (Kwayu, 2016). Baadhi ya wanaume wanashindwa kuweka uwiano wa kuwahudumia wake zao. Suala la upendeleo pia linajitokeza kwa baadhi ya wanaume kuangukia na kufungamana na mke mmojawapo na kuitelekeza familia ya mke mwingine.

Katika wimbo huu wanawake wameshachukulia suala la uke wenza kama ni sehemu ya maisha na ni jambo linalokubalika kwenye jamii. Pia, suala la uke wenza linaweza kusababisha mivutano katika jamii (Seif, 2011). Uke wenza unaweza kusababisha wanawake wasielewane katika familia kwa sababu ya wivu na kupelekea kutokea kwa migogoro katika familia zao. Mara nyingi amani kuvunjika kutokana na uke wenza kusababisha kuwepo kwa ongezeko la watoto wa mitaani, hasa familia inapobaki na mzazi mmoja baada ya ndoa kuvunjika. Wasanii katika wimbo *Mhali* (Mwenza) wanaeleza:

<i>Mihali ikuchishinda,</i>	Uke wenza utatushinda,
<i>Wagosi wechika uaminifu,</i>	Wanaume uaminifu hawana,
<i>Chisha saidi cha atali hechaka,</i>	Kipya zaidi cha awali hapana,
<i>Ukwangu mwasamu siukelefa,</i>	Kwangu mazuri huleti,
<i>Kumi yangu gameme,</i>	Kwa mwezangu yamejaa,
<i>Hata ninghagolose suwamu,</i>	Hata nikifanya zuri,
<i>Ukunyona chefu,</i>	Unaniona kinyaa,
<i>Ukughatisha tamaa,</i>	Mwatukatisha tamaa,
<i>Binadamu siyo Mkungu,</i>	Binadamu si Mungu,
<i>Mihali mbuli ya shida.</i>	Uke wenza shida.

Katika wimbo huu inaonesha jinsi suala la uke wenza linavyosababisha migogoro mwanamume atakapoanza kuonesha upendeleo kwa mwanamke mmoja. Mke mwingine hujisikia wivu na kuzua migogoro katika familia kwa

sababu wivu unaweza kuleta uhasama, malumbano, wivu na chuki. Pia, wanawake walioko katika uke wenza baadhi yao wanaathirika kisaikolojia kutokana na kuwepo kwa mabadiliko makubwa ya mitindo na mienendo ya maisha baada ya mume kuoja mke mwingine. Kutokana na wivu wanawake wanaweza wakakubali kuwa katika uke wenza, lakini lazima mwanamke aathirike kisaikolojia pale atakapokuwa anafikiria mume wake anapokuwa kwa mke mwenzie. Wasanii katika wimbo huo huo wa *Mhali (Mwenza)* wanaeleza:

*Unghowa kwemiyangu,
Mgosi yoyanyemchilo,
Uuya wangu kubeswa,
Nisigale mkopi,
Kukopa sherehe,
Kulipa maafu,
Mtima ukose amani,
Mtima siukulia,
Nyono zikwila,
Mihali mi tabu ya wose.*

Akiwa kwa mwezangu,
Mume niliyempenda,
Fadhira zangu kapuuza,
Nipo kama mkopaji,
Kukopa sherehe,
Kulipa maafa,
Moyo wakosa amani,
Nafsi haitulii,
Hasira zanipanda,
Uke wenza shida.

Uwepo wa ndoa za mitala au uke wenza ni chanzo cha migogoro mbalimbali katika familia na jamii, hasa inapotokea mwanaume amaeshindwa kumudu na kusimamia misingi imara ya kuwepo ndoa za mitala na umuhimu wake. Migogoro pia inajitokeza kutokana na urithi wa mali ambapo kila mmoja huona kama anastahili zaidi kuliko mwenzake. Kwa upande mwingine, baadhi ya wanajamii wanaona kuwa ndoa za namna hiyo ni chanzo cha magojwa ya zinaa, hasa wanandoa wanapokosa uaminifu wa kutunza na kusimamia ndoa zao.

Kuporomoka na kuanguka kwa uaminifu katika ndoa za mitala ni baadhi ya sababu za kuongezeka kwa kasi ya maradhi ya kuambukizwa. Suala la mitala katika jamii ya Wakaguru linaangaliwa kama ishara ya umaarufu ama alama ya kutoridhika kimapenzi. Utafiti huu unatambua kuwepo kwa baadhi ya dini zinazoruhusu kuoja mke zaidi ya mmoja kwa kurejelea misingi ya imani zao. Mitala si tatizo kama suala la uaminifu na uadilifu wa kindoa litazingatiwa na wanandoa (Senzighe, 2004). Kasi ya maradhi ya kuambukiza imekuwa kubwa zaidi kutokana na kukosekana kwa uaminifu katika ndoa za mitala.

Suala la kuwepo kwa maradhi ya kuambuza linapaswa kuchunguzwa kwa umakini zaidi kwa kuzingatia hali halisi ya vyanzo vya maambukizi na jitihada zinazopaswa kuchukuliwa. Jitihada za kuyakabili maradhi hayo zinapaswa kuanzia katika ngazi ya kaya badala ya kuwapa nafasi kubwa watumishi wa umma walio katika ngazi za juu serikalini, hasa waliopo katika miji mikubwa hapa nchini (Mnyagatwa, 2009). Uwiano uwepo katika harakati za kuyakabili maambukizi zaidi. Vita dhidi ya maradhi hayo havina budi kubainisha na kuelekezwa kwenye vyanzo halisi vya maambukizi.

3.5 Uwajibikaji

Suala la uwajibikaji katika utekelezaji wa mambo katika harakati za kila siku za jamii na taifa lolote ni msingi sana. Viongozi wa jamii wanapaswa kushirikiana katika shughuli zote za kijamii na kimaendeleo (Katimba, 2015). Umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu. Mojawapo ya majukumu ya wasanii ni kuhimiza na kusimamia mipango ya jamii ya utekelezaji wa mipango ya maendeleo kwa manufaa ya jamii na taifa lao. Katika jamii ya Wakaguru, vijana walihimizwa kujenga misingi imara ya uwajibikaji katika harakati za utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku. Vijana wanaangaliwa kama ishara ya nguvu ya jamii yao. Uwajibikaji katika jamii ni njia mojawapo ya kuliwezesha taifa lolote liweze kuendelea katika nyaja za kijamii, kisiasa na kiuchumi. Msanii katika wimbo wa *Kumgunda* (Shambani) anasisitiza suala la uwajibikaji:

<i>Ni wajibu wako,</i>	<i>Ni wajibu wako,</i>
<i>Kumgunda chilute,</i>	<i>Na shambani tuende,</i>
<i>Wanike chiwajibike,</i>	<i>Vijana tuwajibike,</i>
<i>Sinda sisigonaga njala.</i>	<i>Tumbo halilali njaa.</i>

Msanii anaonesha jinsi vijana wanavyopaswa kuwajibika katika shughuli mbalimbali kwa maendeleo ya taifa lao. Jamii haiwezi kujenga kufanikiwa katika maendeleo yake bila kuwepo kwa uwajibikaji katika shughuli mbalimbali za uzalishaji mali na uchumi, hasa katika kilimo, biashara na ufugaji. Pia, wanaendelea kueleza kwamba vijana hawana budi kufanya kazi kwa juhudi na maarifa ili tuweze kupiga vita umaskini na jamii ya sasa wengi wamejikita katika kufanya kazi kwa bidii ili waweze kujikwamua na hali duni ya kimaisha.

Uzembe na kutowajibika hufifisha jitihada za maendeleo ya jamii. Pia, huonesha namna uzembe unavyoweza kuathiri utekelezaji wa maendeleo katika

familia, jamii na taifa kwa ujumla. Uwajibikaji unapaswa kufuatwa na kupewa uzito katika kufanikisha suala la ujenzi wa jamii endelevu. Wananchi wanapaswa kuwajibika kwa kufanya kazi kwa jitihada na maarifa katika kuyakabili matatizo mbalimbali ili kujenga uchumi imara kwa manufaa ya jamii na taifa. Uwajibikaji katika kazi ni chachu ya maendeleo ya jamii. Uzembe na kutowajibika ni kikwazo kikubwa kinachokwamisha maendeleo ya jamii yoyote ile. Hivyo, mwandishi anaitaka jamii yetu ijue umuhimu wa kazi nani anawajibika katika jamii (Isakwisa, 2003). Wasanii katika wimbo wa *Kungunda* (Shambani) anasema:

<i>Magendelelo gakufika?</i>	Maendeleo yatafikaje?
<i>Wannu chikuamini,</i>	Watu tulio waamini,
<i>Chwengha samana,</i>	Tukawapa dhamana,
<i>Wadia rushwa?</i>	Ni wala rushwa?

Wasanii wanaonesha jinsi ya uwajibikaji kwa waganga ili kuwahudumia wagonjwa. Pia, makundi mbalimbali katika jamii yatupaswa kuwajibika. Uwajibikaji wa dharti ni kitendo cha kufanya kazi kwa pamoja na kujitoa pasipo kusukumwa na mtu yeyote. Hali hii inamaana kuwa kufanya kazi na wengine ili kuleta maendeleo katika jamii. Pia, ni muhimu katika kufikia malengo ya maendeleo endelevu. Watu wakiwajibika katika kufanya kazi jamii hiyo lazima iendelee kwa sababu uwajibikaji ni chachu ya maendeleo (Nathanael, 2006). Ikiwa viongozi na wananchi hawatawajibika kutakuwa na kila uwezekano wa kutokea kwa maafa mengi katika jamii.

Kila mtu katika jamii anapaswa kutimiza wajibu wake ili kuendana na kasi ya maendeleo katika ngazi ya familia, jamii na taifa. Pia, viongozi wanapaswa kutumia madaraka yao kwa kufuata kanuni na taratibu za nchi badala ya kuendeleza rushwa na ubinafsi kitu ambacho kinaweza kuathiri maendeleo ya jamii. Jamii haina budi kuwajibika vyema ili kujenga jamii yenye maendeleo mazuri. Jamii haina budi kupingana na viongozi ambao hawawajibiki badala yake wamekuwa wanyonyaji kwa kupokea rushwa kwani wanaoteseka ni watu wa tabaka la chini kwa kuishi maisha ya unyonge na shida.

4.0 Hitimisho

Makala hii imechunguza dhamira za nyimbo za Wakaguru katika kujenga na kuimarisha mafunzo ya kijadi nchini Tanzania. Baadhi ya dhamira

zilizowasilishwa zinahusu malezi, matambiko, uwajibikaji, uke wenza na umuhimu wa tiba asilia. Matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba nyimbo za Wakaguru ni kiungo muhimu cha kijadi kujenga misingi ya kuielimisha na kuielewa jamii hiyo kwa kurejelea misingi imara ya kihistoria, mazingira, falsafa na utamaduni wake. Jambo hilo huipa jamii fursa pana ya uelewa wa mazingira yao, falsafa yao na utamaduni wao kwa undani.

Marejeleo

Isakwisa, C. (2003). *Nyimbo za Harusi za Wanyakyusa na Mabadiliko ya Jamii. Tasinifu ya Shahada ya Kwanza, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.*

Katimba, Y. (2015, Desemba 14 – 20). ‘Wafrika Wakemee Ma-Vasco da Dama. *MwanaHalisi*. Namba 317, uk. 19.

King’ei, K. (2002). ‘Suala la Uana katika Fasihi ya Kiswahili: Uhakiki wa Utafiti Kutoka Kenya katika Utafiti wa Kiswahili’. Moi University Press. Uk.87 - 95.

Kisanji, J. (2012). *Kuuwawa kwa Miiko na Kupotoka kwa Maadili: Uchunguzi Kifani wa Jamii ya Wabungu. Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.*

Kiyimba, A. (2001). *Gender Stereotypes ni the Folkloretales and Proverbs of the Baganda. A Thesis of a Doctor of Philosophy, University of Dar es Salaam.*

Kwayu, E. (2016, Julai 18 – 24). ‘Viongozi Vijana Wasibweteke’. *MwanaHalisi*. Namba 348, uk. 17.

Legulegu, S. (2016). *Siasa na Uchumi Katika Fasihi ya Kiswahili. Tasinifu ya Shahada ya Kwanza, Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira.*

McNiff, J. (1992). *Art as a Medicine*. London: Jessca Kingsley Publisher.

Mgogo, Y. P. (2012). *Matumizi ya Nyimbo za Wanyiha Misibani. Tasinifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.*

Mgogo, Y. P. (2017). *Kuchunguza Hadithi za Wanyiha katika Kurithisha Elimu ya Jadi. Tasinifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.*

Mhegera, E. (2016, Februari 15 – 21). ‘Vijana: Serikali Ziache Ubabe’.

MwanaHalisi. Namba 326, uk. 15.

Mwakanjuki, N. (2011). Athari za Mabadiliko ya Kijamii na Kiuchumi katika Nyimbo za Kapote za Mwimbaji Mwandwanga katika Jamii ya Wanyakyusa. Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dodoma.

Mwangosi, G. (2016). Kufungamana kwa Vitendawili vya Wanyakyusa na Matukio ya Kijamii. Chuo Kikuu cha Katoliki Ruaha, *RUJASS*, Vol 2: 50 - 67.

Mwangosi, G. (2019). Kuchunguza Dhamira na Fani katika Nyimbo za Magosi za Jamii ya Wanyakyusa. Tasinifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Nathanael, C. (2016, Februari 15 – 21). ‘Unyanyasaji Uliofanyika India Haukubaliki’. *MwanaHalisi*. Namba 326, uk. 18.

Ngadala, D. K. (2003). *Ujenzi na Mmomonyoko wa Maadili ya Taifa: Mkutano wa Sekta ya Utamaduni*. Morogoro.

Nzobe, R. L. (2012). Fasihi Simulizi na UKIMWI: Mifano Kutoka katika Nyimbo za Ngoma ya Wigashe ya Wasukuma. Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Paul, S. B. (2016). Dhima za Fasihi Simulizi: Mifano Kutoka katika Nyimbo za Ngoma ya Bunungule ya Jamii ya Wasukuma. Tasinifu ya Shahada ya Kwanza, Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira.

Rajabu, A. (2012). Misemo ya Kiswahili katika Vazi la Fulana: Uchambuzi wa Dhamira na Matumizi ya Lugha. Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Sengo, T. S. Y. M. (2009). *Sengo na Fasihi za Kinchi*. Dar es Salaam: The Registered Trustee of Al-Amin Education and Research Academy.

Senzighe, R. (2004). *Usawiri wa Mwanamke katika Methali za Wapare*: Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Silau, G. K. (2013). Kutathmini Dhima ya Nyimbo katika Kukuza na Kuimarisha Malezi: Mfano wa Kabila la Wakaguru. Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Wamitila, K.W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi, Misingi ya Vipengele Vyake*. Nairobi, Phoenix Publishers Ltd.

Wizara ya Elimu, (2009). *Kitabu cha Watu Wazima, Historia, Hatua ya Sita*. Dar es Salaam: Wizara ya Elimu.

Wizara ya Elimu, (2011). *Kitabu cha Watu Wazima, Historia, Hatua ya Sita*. Dar es Salaam: Wizara ya Elimu.

Ufutuhi kama Mbinu ya Kuwasilisha Dhamira za Kisiasa katika Katuni za Mtandaoni za Masoud Kipanya

Majuto Kapaya Manyuka
Chuo Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam
manyukakapaya@gmail.com

Ikisiri

Makala hii inashughulikia ufutuhi katika katuni za kisiasa za Masoud Kipanya. Kilichochunguzwa hapa ni mbinu za ufutuhi katika katuni za kisiasa na namna zinavyowasilisha mawazo ya kisiasa katika jamii ya Tanzania. Data za msingi zilikusanywa maktabani kwa mbinu ya uchanganyuzi matini wa katuni zilizochapishwa katika akaunti ya Masoud Kipanya katika mtandao wa kijamii wa *Instagram*. Data za upili kwa ajili ya ufafanuzi wa data za msingi zilipatikana kwa mbinu ya usomaji wa nyaraka. Nadharia ya Semiotiki imetumika ili kufasili ishara za katuni na mawazo ya kisiasa yanavyowasilishwa na mbinu za ufutuhi. Makala hii imebainisha kuwa katuni za kisiasa za Kipanya hutumia mbinu za ufutuhi katika kujadili na kuwasilisha mawazo mbalimbali ya kisiasa. Mbinu za ufutuhi ni muhimu katika kuwasilisha ujumbe uliokusudiwa. Makala hii inapendekeza kufanyika kwa tafiti zaidi kuhusu ufutuhi katika tanzu mbalimbali za fasihi.

Istilahi za Msingi: Ufutuhi, mbinu za ufutuhi, katuni, katuni za kisiasa na mtandaoni.

1.0 Utangulizi

Neno ‘katuni’ limetokana na neno la Kiingereza ‘*Cartoon*’ ambalo linatokana na neno la Kifaransa ‘*Cartouch*’ lenye maana ya kuchora. Katuni ni mchoro, kiwakilishi au ishara inayosababisha ucheshi, utani au kejeli (Gunda, 2014). Katuni ni mchoro uliochorwa kwa ufundi na kwa namna ya kushawishi na kuchekesha ili kuwasilisha ujumbe fulani. Katuni huambatana na maelezo mafupi ambayo hudokeza jambo mahsusi lililokusudiwa na msanii. Wasanii wanaochora katuni huwasilisha mawazo yao kwa njia ya mchoro yenye kuibua

MAKALA HALISI HISTORIA YA MAKALA

Kupokelewa: 06 Machi
2022

Kurekebishwa: 18 Juni
2022

Kukubaliwa: 29 Julai
2022

Kuchapishwa: 20
Septemba 2022

ISSN: 2799 – 2187

*Juzuu 1,
Toleo 1,
uk.54 – 65.*

NUKUU

Manyuka, M. K. (2022). Ufutuhi kama Mbinu ya Kuwasilisha Dhamira za Kisiasa katika Katuni za Mtandaoni za Masoud Kipanya. *Jarida la Fahari ya Kiswahili*, 1(1), 54 – 65.

taswira fulani, utani, mzaha, kejeli, dhihaka, balagha na ucheshi. Katuni huchukua nafasi ndogo kuwasilisha habari zenye uzito zinazowekwa kimuhtasari (Meijs, 2011). Uchoraji wa katuni unaweza kufuata mikondo mbalimbali iliyosheni mbinu za ufutuhi.

Dhana ya ufutuhi inatumiwa kama kisawe cha neno la Kiingereza ‘comic’ linalodokeza hali ya ucheshi (Ponera, 2017). Ponera anaendelea kueleza kuwa ufutuhi unajadiliwa kama hali inayojengwa na maneno, matendo, matukio au mazingira yoyote yenye mnato na mvuto hali inayowafanya watu wachangamke, wacheke na kufurahi. Dhana ya ufutuhi inadokeza hali ya kuchekesha au kuchangamsha. Nchini Tanzania, uchoraji wa katuni umekuwa maarufu miaka ya hivi karibuni kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia. Wachoraji hawalazimiki tena kuchapisha michoro yao magazetini tu kwa sababu kuna majukwaa mbalimbali mtandaoni kama vile *facebook*, *twitter* na *instagram*.

Mbali na ukweli kuwa ufutuhi huibua ucheshi, vicheko na furaha, pia unakusudia kuwasilisha ujumbe fulani. Wasanii hubuni kazi zao kifutuhi ili kufikisha ujumbe kwa njia burudishi. Wabunifu wa katuni hutumia mbinu za ufutuhi katika kubuni na kuchora katuni ili ziweze kuelimisha kwa njia ya ucheshi, vicheko na furaha kwa hadhira (Mwatulindila na Kangira, 2012). Kuna mbinu mbalimbali zinazojenga ufutuhi katika kazi za kisanaa. Baadhi yake ni ubeuzi, kejeli, vijembe, utani, dhihaka, ufyosi na sitihizai (Ponera, 2014 & Gwanko, 2017). Makala hii inabainisha mbinu za ufutuhi pamoja na ujumbe unaobebwa katika katuni za kisiasa. Katuni za kisiasa ni zile zinazobeba maudhui yaliyofinyangwa katika michoro kwa kutumia sanaa ya hali ya juu.

Katuni ya kwanza ya kisiasa inaripotiwa kuonekana Misri mwaka 1300 KK. Sanaa hiyo ilizagaa pande mbalimbali za dunia mnamo karne ya 16, hasa Uingereza na Marekani. Inaaminika kuwa katuni ya kwanza kuchapishwa kwenye jarida ilikuwa ni katuni ya ‘JOIN OR DIE’ iliyochorwa na Benjamin Franklin (1754). Katuni hiyo ilionesha nyoka aliyekatwa vipandevipande, huku vipande hivyo vikipewa majina ya majimbo ya Marekani yaliyokuwa chini ya Ukoloni. Mchoro huo uliakisi imani kuwa nyoka anaweza kujiunga hata baada ya kukatwakatwa. Benjamin alikuwa akihimiza Wamarekani kuungana na kujenga umoja thabiti (Goguen, 2003). Katuni zinaweza kutumika kukejeli

mfumo wa kisiasa sanjari na kuonya na kuikosa jamii. Makala hii inabainisha mbinu za ufutuhi pamoja na ujumbe unaobebwa katika katuni za kisiasa za Masoud Kipanya zilizochapishwa katika mtandao wa kijamii wa instagram.

2.0 Nadharia na Mbinu za Utafiti

Makala hii imechunguza ufutuhi katika katuni za kisiasa za Masoud Kipanya. Data za msingi zilikusanywa maktabani kwa mbinu ya uchanganuzi matini wa katuni zilizochapishwa katika akaunti ya Masoud Kipanya katika mtandao wa kijamii wa Instagram. Mbinu ya uteuzi lengwa ilitumika kupata katuni 6 zilizokidhi mahitaji ya makala. Data za upili kwa ajili ya kuthibitisha data za msingi zilipatikana kwa mbinu ya usomaji wa nyaraka. Nadharia ya Semiotiki imetumika katika mjadala wa data zilizowasilishwa ili kufasili ishara za katuni na mawazo ya kisiasa yanayowasilishwa na mbinu za ufutuhi.

Nadharia ya Semiotiki iliasisiwa na mwanaisimu wa Kiswizi, Ferdinand de Saussure na Mwanafalsafa wa Kimarekani Charles S. Peirce mnamo Karne ya 19. Waasisi wake wanasisitiza uchunguzi na uchanganuzi wa mifumo ya ishara kwa kuzingatia uhusiano uliopo baina ya kiwakilishi na kiwakilishwa (Saussure, 1966). Katika makala hii, uchambuzi wa katuni za kisiasa umezingatia matukio yanayowasilishwa kwa njia ya katuni kwa kurejelea muktadha halisi wa siasa za Tanzania ili kupata maana yake. Katika ubainishaji wa mbinu za ufutuhi zilizotumika katika katuni za kisiasa za Masoud Kipanya, nadharia ya Semiotiki imetumika kuongoza uelezaji wa maana za katuni hizo.

3.0 Ufutuhi katika Katuni za Kisiasa za Masoud Kipanya

Data za makala hii zinaonesha kuwa ufutuhi katika katuni za kisiasa za Masoud Kipanya unajitokeza katika vijenzi mbalimbali. Baadhi ya vijenzi hivyo ni chuku, ubeuzi, kejeli, vijembe, utani na dhihaka. Mbinu katika vijenzi hivyo hubeba mawazo fulani ya kisiasa kama yalivyojadiliwa katika vipengele vinavyofuata. Sehemu inayofuata imewasilisha mbinu mbalimbali za ufutuhi pamoja na maana zake katika katuni za kisiasa za Masoud Kipanya zilizochapishwa katika mtandao wa *instagram*.

3.1 Chuku

Chuku ni maneno yaliyotiwa chumvi ili kuisisitiza ujumbe fulani au kusifia kitu fulani. Msemo ‘kupiga chuku’ ni hali ya kuongezea, kuzidisha au kutia chumvi

kitu, habari au jambo fulani (Wamitila, 2000). Chuku huwa na ukweli fulani unaotakiwa kuwasilishwa ila unakuwa umefichwa ndani ya kauli isiyo na uhalisi. Upigaji wa chuku hufanyika ili kuvuta hisia, kushawishi na kuchekesha hadhira. Mbinu hii inachukuliwa kuwa ni mbinu mojawapo inayojenga ufutuhi kwani huchochea hali ya ucheshi kwa hadhira. Imebainika kuwa upigaji wa chuku katika katuni zilizochunguzwa unajitokeza kwa kutumia mchoro uliovuka uhalisi ambapo ukubwa wa kiungo huzidishwa au kupunguzwa kuliko kawaida kama inavyoonekana katika mchoro ufuatao. Mfano 1:



Chanzo: Masoudkipanya (Akaunti ya *Instagram*)

Mfano 1 unadhihirisha kuwa kuna matumizi ya chuku. Mdomo wa katuni ya kwanza iliyo kushoto umefanywa uonekane mkubwa kuliko kawaida. Hivyo, umepigwa chuku kwani mtu hawezi kuwa na mdomo mpana kiasi hicho. Utiaji wa chuku, mbali na kusababisha hali ya ucheshi, husaidia kuelezea, kuelewa na kutathmini jambo au kitu kilichotiwa chuku (Leech, 1983). Mdomo umepigwa chuku ili kudokeza kuwa mbunge ni muongejaji sana anapokuwa bungeni. Pia, ni mbunge machachari katika kujenga hoja zenye kukosoa serikali na kutetea masilahi ya wananchi.

Katuni ya pili iliyo upande wa kulia inamuonesha mtu yule yule akinyonya maziwa kwenye chupa. Hali hii inaweza kuwa na maana kuwa hayo ndiyo malipo ya usemaji wake. Inawezekana ni kupewa uongozi wa juu zaidi kama vile uwaziri. Hali ya kupewa uongozi wa juu inaweza kuwa mbinu ya kumnyamazisha ili asiendele kuisakama serikali. Pia, inaweza ikawa ni kutoa fursa kwa mhusika ili aweze kutekeleza yale anayoyapigia kelele. Katuni hii imefanikiwa kuvuta hisia za ucheshi na kuchokoza fikra za hadhira kuhusu siasa.

3.2 Ubeuzi

Ubeuzi ni hali ya kushushia hadhi mtu kwa maneno au vitendo (TUKI, 2013). Ubeuzi husababisha hali ya furaha, kicheko au ucheshi kwa watazamanji au wasikilizaji. Tunakubaliana na fasili hii, kwa sababu, ubeuzi huwa ni aina fulani ya ucheshi ambao kwa namna moja ama nyingine humtweza au kumdunisha mhusika fulani. Baadhi ya katuni za kisiasa za Masoud Kipanya hutweza au kudunisha ili kuibua ucheshi miongoni mwa hadhira na hufikisha ujumbe fulani uliokusudiwa kama ilivyobainishwa katika katuni inayofuata. Mfano 2:



Chanzo: Masoudkipanya (Akaunti ya *Instagram*)

Katika mfano huo hapo juu, mwekezaji wa ndani ameshushwa hadhi kwani ameachwa nyuma na mavazi yake ni duni ukilinganisha na mwekezaji wa nje. Katuni hii inazungumzia masuala ya kisera na namna wanasiasa au viongozi wanavyowatweza wawekezaji wa ndani huku wakiwapendelea wa nje. Kiongozi anaonekana amemkumbatia mwekezaji wa nje jambo ambalo ni ishara ya upendo na kujali. Hali hii inadokeza kuwa viongozi wa kisiasa wanawapa fursa za kuwekeza nchini watu kutoka nje ya nchi huku wakiwanyima wazawa fursa hizo. Msanii anaikumbusha hadhira kutafakari na kuboresha sera ili kuleta usawa baina ya wawekezaji wa ndani na wale wawekezaji wa nje.

3.3 Kejeli

Kejeli ni mbinu ya kisanaa inayotumia maneno ya kudharau ya moja kwa moja au yaliyofichika ili kukemea kitendo, jambo, kitu au mtu fulani. Kejeli hukusudia kuleta maana iliyo kinyume na ile iliyokusudiwa au kinyume na ukweli ulivyo (Msokile, 1993). Kejeli kama mbinu ya ufutuhi huchekesha kutokana na aina ya maneno yanayotumika na uhusiano wa kile kinachorejelewa. Wasanii hutumia mbinu ya kejeli katika kujenga ufutuhi na kufikisha ujumbe kwa hadhira bila kuathiri hadhira inayohusika. Pamoja na kuwa na vituko na mbwembwe zinazofurahisha, kejeli huteta, hufunza na

kuonya jamii juu ya masuala mbalimbali yaliyo kinyume cha maadili. Katika baadhi ya katuni za kisiasa za Masoud Kipanya inabainika kuwa mbinu hii imetumika ili kufurahisha na kuwasilisha mawazo ya kisiasa kama ilivyodokezwa katika mfano ufuatao.

Mfano: 3



Chanzo: Masoudkipanya (Akaunti ya *Instagram*)

Katuni katika mfano 3, mtu mmoja anaonekana akilalamika kuwa wageni wamemaliza chakula baada ya kuingiza mkono wake kwenye sahani tupu iliyoandikwa neno ‘Ajira’. Halafu, mwakilishi wa serikali anajibu ‘Umeona eeh’. Kipanya amesimama pembeni anawaza ‘Si umwambie ukweli kwamba umeshindwa kupika’. Kwa kuzingatia muktadha wa kisiasa nchini Tanzania na kwingineko barani Afrika, tunaweza kusema kuwa msanii anakejeli serikali kushindwa kutengeneza sera nzuri za ajira na kuweka mazingira bora kwa sekta binafsi ili kukuza soko la ajira. Katuni hii inakejeli uongozi kwa kushindwa kuondoa tatizo la ajira nchini. Tafiti nyingi zinaonesha kuwa zaidi ya asilimia hamsini ya vijana katika nchi zinazoendelea, hawana ajira rasmi (OYE, 2016). Serikali inakumbushwa wajibu wake wa kutunga sera nzuri za uwekezaji na ajira nchini.

3.4 Vijembe

Vijembe ni maneno ya mafumbo ya kumsema mtu. Vijembe ni mbinu mojawapo ya ufutuhi (TUKI, 2013). Ufutuhi hapa hutokea pale mtu anayetaniwa au kuambiwa mara anapokosa jambo la kujibu na kuonekana kama kaaibishwa na kusababisha hali ya furaha au kicheko kwa anayesoma au anayesikiliza (Sheikh, 1993). Wasanii hutumia vijembe ili kukosoa, kuadilisha na kupuuza mambo yasiyomema katika jamii. Mchora katuni hutumia vijembe

katika katuni zake. Imebainika kuwa baadhi ya katuni za kisiasa za Masoud Kipanya zina vijembe ambavyo vimebeba mawazo fulani ya kisiasa. Mathalani, katuni ifuatayo inadhihirika kuwa na kijembe.



Chanzo: Masoudkipanya (Akaunti ya *Instagram*)

Mwanamke anaongea na mtu kwa njia ya rununu, anampiga kijembe anayeongea naye. Anasema: “Mume wangu alipotolewa uwaziri na nyie mkapotea! Leo karudishwa, ushoga kwangu umerudi!” Mwanamke anaonekana ni mke wa kiongozi ambaye amerudishwa kwenye cheo chake cha uwaziri, cheo ambacho aliwahi kukipata huko nyuma. Jambo hili limekuwa likitokea mara kwa mara katika nchi yetu. Mawaziri wamekuwa wakitenguliwa na baadaye kurudishwa tena madarakani. Kama ilivyo kawaida ya marafiki wanafiki hupenda kuwa na mtu mwenye uwezo wa kipesa. Pale anapokosa uwezo huo nao hung’atuka. Kasheshe huja pale mtu huyo anapopata uwezo tena, marafiki wote wa zamani hurejea. Mbunifu wa katuni hii huenda anataka kuwaasa wanajamii kudumisha urafiki wa dhati na kujenga urafiki wa kuvumiliana katika shida na raha.

3.5 Utani

Utani ni hali ya kufanyiana mizaha miongoni mwa wanajamii au jamii mbalimbali bila ya kuogopa wala kushtakiana (Wamitila, 2003). Utani katika jamii za Kiafrika hutumika kama wenzu wa kuliwaza, kuburudisha na kufunza mambo mbalimbali. Watu huweza kutaniana sehemu tofati tofauti kama vile msibani, arusini, vilabuni na ngomani. Wasanii wa katuni nao hutumia utani katika katuni zao ili kutimiza malengo yao ya kuburudisha na kuelimisha jamii. Mbinu ya utani katika katuni hutumika ili kuzua hali ya ufutuhi na wakati huo huo kuwasilisha ujumbe fulani kwa jamii. Kwa mfano, katuni ya kisiasa ifuatayo inathibitisha hili. Mfano 5:



Chanzo: Masoudkipanya (Akaunti ya *Instagram*)

Mazungumzo ya katuni, kama inavyoonekana katika mfano namba 5, yametumia mbinu ya utani. Maneno yametumika katika muktadha wa kimasihara. Kipanya anamuuliza mkurugenzi wa halmashauri kama pesa za kujengea barabara ndizo alizotumia kujengea jumba lake la kifahari. Mkurugenzi anakubali. Haiwezekani kiongozi atumie vibaya mali ya umma, kisha anapoulizwa akubali kirahisi bila ya wasiwasi. Kipanya anamhoji tena Mkurugenzi; “Na wewe unatumia barabara hizo hizo mbovu! Hiyo ni akili au matope?” Mkurugenzi anajibu “Nilitumia akili kubwa sana bro!”

Jibu la Mkurugenzi nalo linadokeza masihara. Haiwezekani kutumia mali ya umma kununua gari binafsi ikawa akili kubwa. Mazungumzo haya yanachekesha na yanatafakarisha. Viongozi wabadhilifu wanatumia vibaya mali za umma. Badala ya kutumia fedha za umma kwa masilahi ya wananchi wote, huzitumia kujinufaisha. Moja ya changamoto ya utekelezaji wa bajeti ya serikali ni matumizi mabaya ya rasilimali kwa baadhi ya viongozi (Kichere, 2021). Tabia hii inarudisha nyuma juhudi za serikali katika kuwaletea wananchi maendeleo.

3.6 Dhihaka

Dhihaka ni mbinu ya kisanaa ambayo huhusisha kufanya mzaha, dharau tabia au mienendo fulani isiyofaa kwa namna inayoibua dhana ya ufutuhi. Dhihaka ni aina ya kinaya au kejeli ambayo uwezo wake mkubwa hujitokeza katika nguvu za kibalagha (Wamitila, 2008). Hali hii ni aina ya usanii ambayo maneno yanayotamkwa wakati mwingine huandikwa yakizigusa hisia za mlengwa au walengwa kwa namna ambayo inaweza kukasirisha au kuwafanya watizame

hali fulani kwa undani na tafakuri zaidi. Dhihaka huweza kugusa hisia kwa namna fulani inayokasirisha kwa kuwa aghalabu hutumia maneno ya mzaha yanayouidhi, hasa katika kukemea mienendo mibovu katika jamii. Utafiti ulibaini kuwa Kipanya hutumia dhihaka katika katuni zake za kisiasa kuzichapisha katika mitandao ya kijamii. Mathalani: Mfano 6:



Chanzo: Masoudkipanya (Akaunti ya *Instagram*)

Katika mfano namba 6 tunabaini kuwa Kipanya anamdhihaki mtu anayeonekana kukerwa na matumizi ya fedha katika safari za viongozi. Mtu huyo anamwambia Kipanya kuwa “Tumeanza kuharibu pesa kwa safari”. Kipanya anadharau fikra za kupinga matumizi ya pesa katika safari za viongozi kwa kuwa anaamini kuwa upinzani unatokana na kwamba mtu huyo siyo sehemu ya wanufaika wa fedha hizo za safari. Mbinu hii ya dhihaka katika katuni inaonekana kubeba mawazo kuwa watu wanaopinga safari za viongozi baadhi yao wanafanya hivyo kutokana na wivu kwani enzi wakiwa sehemu ya utawala wa awamu ya 5 hawakunufaika na fedha za safari. Serikali ya awamu ya 5 haikupendelea kusafirisha viongozi na kuwalipa posho jambo ambalo linaonekana kuwa tofauti na serikali ya awamu ya 6 ambapo viongozi wanasafiri na kulipwa posho zao za safari. Mchoraji wa katuni huenda anataka kuitafakarisha jamii juu ya upinzani uliopo zidi ya serikari ya awamu ya 6.

4.0 Hitimisho

Katuni za kisiasa za Masoud Kipanya huvutia, huchekesha na kuchochea haja ya kutafakari upya mienendo ya siasa na wanasiasa nchini kutokana na matumizi ya mbinu mbalimbali za ufutuhi kama ilivyobainika katika makala hii. Kwa hiyo, tunashawishika kuamini kwamba mbinu za ufutuhi ni muhimu sana katika kuwasilisha ujumbe kwa hadhira. Hivyo ni vizuri tafiti zaidi zikaendelea

kufanyika kuhusu ufutuhi katika tanzu mbalimbali za fasihi ili kuzielewa zaidi tanzu hizo.

Marejeleo

BAKITA, (2015). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Longhorn Publishers.

Barthes, R. (1973). *Mythologies*. London: Made Simple Book.

Goguen, J. (2003). A Semiotic Analysis of Political Cartoons. Katika <https://cseweb.ucsd.edu/~goguen/courses/271sp03/spaper> on 06/08/209. Imesomwa Juni 2022.

Gunda, L. (2014). Katuni ni Nini? Ufasihi wa Katuni. Katika <http://jiandae.wordpress.com> Imesomwa Julai, 2022.

Gwanko, C. L. (2017). Kutathmini Mbinu za Ufutuhi katika Kuelimisha Jamii kuhusu Janga la UKIMWI katika Tamthiliya ya *Embe Dodo na Ushuhuda wa Mifupa*. Tasinifu ya Umahiri, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Kichere, C. (2021). Ripoti ya Mdhimiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/20. Dodoma: Government Printer.

Kilapilo, V. (2018). Changamoto za Kimaana katika Kusimbua Ujumbe kwenye Katuni-Mnato-Bubu za Magazeti ya Kiswahili nchini Tanzania. Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Meijs, E. (2011). *A Picture is Worth a Thousand Words; Framing the Eurozone Debt Crisis: Metaphors in Political cartoons*. Tiburg: Tiburg University.

Mrikaria, S. E. (2010). Kejeli na Fasihi ya Kiswahili – Tanzania. Katika *Swahili Forum*, Juz. 17: 104-125.

Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Dar es Salaam: East African Educational Publishers.

Mwetulundila, R., na Kangira, J. (2015). An Analysis of Rhetoric and Humour in Dudley's Political Cartoons Published in the Namibian Newspaper in 2012. Katika *International Journal of Research in Humanities and Social Studies*, Juz.2 (I6): 63 -75.

- Otuoma, D. A. (2015). Mitindo na Maudhui katika Uchanganuzi wa Vibonzo kwenye Gazeti la Taifa leo. Tasinifu ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Nairobi.
- OYE. (2016). Annual Report: Opportunities for Youth Employment in Tanzania. Katika www.snvworld.org Imesomwa Januari, 2022.
- Pierce, C. (1977). *Semiotics and Signifies*. Bloomington: Indiana University Press.
- Ponera, A. S. (2014). Ufutuhi katika Nathari ya Kiswahili: Ulinganisho wa Nathari za Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi. Tasinifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Dodoma.
- Ponera, A. S. (2016). Ufutuhi katika Jamii za Watanzania: Mjadala kuhusu Sura za Utokeaji na Dhima zake. Katika *MULIKA*, Juz. 37: 23 - 44.
- Ponera, A. S. (2018). Kutoka Futuhi hadi Ufutuhi: Chimbuko, Maendeleo na Nadharia zake. Katika *MULIKA*, Juz. 33: 1 - 20.
- Saussure, F. D. (1966). *Course in General Linguistics*. Wade Baskin (mfs). New York: MacGraw.
- Sani, I. Abdullah, M. H., Ali, A. M., na Abdullah, F. S. (2012). The Role of Humour in the Construction of Satire in Nigerian Political Cartoons. *Online Journal of Communication and Media Technologies*, 2(3):148-153. Katika <http://docs.google.com>. Imesomwa Agosti 2021.
- Sheikh, S. (1994). Yanayoudhi kuyaona Mafumbo na Vijembe vya Kiswahili. katika *Swahili Kolloquium*.
- TUKI (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.
- TUKI (2004). *Kamusi ya Kiswahili sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.
- Wamitila, K. W. (2008). *Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Nairobi: Vide Muwa.
- Wamitila, K. W. (2010). *Kazi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide Muwa.
- Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Wanjiku, K. H. (2006). Uwiano wa Picha na Mantiki katika Mabango ya Matangazo ya UKIMWI: Mtazamo wa Kisemiotiki. Tasinifu ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Wanyonyi, M. C. (2015). Ishara na Uashiriaji kama Nyenzo ya Mtindo, Maana na Kiwakilishi cha Itikadi katika Riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* katika *Swahili Forum*, Juz. 22:104-118.

Usawiri wa Lugha ya Ishara Iliyotafsiriwa katika *Shetani Msalabani*

Birigitha Ngwano John
Chuo Kikuu cha Dodoma
birigithangwano@gmail.com

Ikisiri

Makala hii inasawiri lugha ya ishara iliyotafsiriwa katika riwaya ya *Shetani Msalabani*. Mbinu ya usaili na usomaji matini zilitumika kupata data za msingi zilizotumika katika makala hii. Data za msingi zilipatikana kwa kurejelea riwaya ya *Shetani Msalabani* na matini chanzi yake ambayo ni *Devil on the Cross*. Nadharia ya Ulinganifu wa Kimawasiliano imetumika kama kiunzi cha uchambuzi wa data zilizowasilishwa katika makala hii. Makala hii imebaini kuwa lugha ya ishara iliyotafsiriwa katika *Shetani Msalabani* imejibainisha kupitia vipengele vya wahusika wa kiishara, matukio ya kiishara na katika kichwa cha riwaya. Makala hii inapendekeza kuwa wafasiri wa kazi za kifasihi wanapaswa kuzingatia misingi ya kiulinganifu katika kutafsiri lugha ya ishara ambayo ni kipengele muhimu cha matumizi ya lugha.

Ilstilahi za Msingi: Tafsiri, ishara, lugha ya ishara, usawiri wa lugha na ulinganifu wa kimawasiliano.

1.0 Utangulizi

Tafsiri ni taaluma kongwe iliyoanza tangu mwanadamu alipoanza kuwasiliana kwa njia ya lugha. Taaluma hii inahusu uhawilishaji wa mawazo, taarifa na ujumbe wa maandishi kutoka lugha chanzi (LC) kwenda lugha lengwa (LL) (Mwansoko na wenzake, 2006). Kwa upande wa fasihi, tafsiri hufanyika katika tanzu za nathari, tamthiliya na ushairi. Tanzu za nathari na tamthiliya kwa idadi kubwa zimefanyiwa tafsiri zaidi kuliko utanzu wa ushairi (Mekacha, 2013). Mojawapo ya sababu za kutafsiri kazi za fasihi ni pamoja na kueneza fasihi ya Kiswahili na utamaduni wake. Malangwa (2005) anadokeza kuwa mchakato wa

MAKALA HALISI HISTORIA YA MAKALA

Kupokelewa: 08 Machi
2022

Kurekebishwa: 12 Juni
2022

Kukubaliwa: 29 Julai
2022

Kuchapishwa: 20
Septemba 2022

ISSN: 2799 – 2187

Juzuu 1,
Toleo 1,
uk.66 – 76.

NUKUU

John, B. N. (2022). Usawiri wa Lugha ya Ishara Iliyotafsiriwa katika *Shetani Msalabani*. *Jarida la Fahari ya Kiswahili*, 1(1), 66 – 76.

kutafsiri matini za kifasihi hukumbana na changamoto mbalimbali zinazotokana na utofauti wa tamaduni baina ya lugha moja na lugha nyingine.

Makala hii imechunguza lugha ya ishara iliyotafsiriwa katika kazi za kifasihi. Mpemba (2016), Yegon (2016) na Mosha (2017) wanadokeza kuwa, lugha ya ishara hujengwa kitamathali kwa kutumia mbinu mbalimbali za kisanaa kama vile sitiari na tashibiha. Hali hii inatokana na ukweli kwamba lugha ya ishara hukuza na hujenga maudhui ya kazi inayohusika. Lengo la kujengwa hivyo ni kuifanya kazi iwe na mvuto wa kiusomaji. Wafasiri wanapaswa kumakinikia tafsiri ya lugha ya ishara ili matini lengwa (ML) iwe na mvuto unakaribiana na ule wa matini chanzi (MC). Wataalamu wengi wamechunguza changamoto za kutafsiri matini za kifasihi kwa ujumla wake, lakini suala la tafsiri ya lugha ya ishara halijashughulikiwa vilivyo. Makala hii yameshughulikia pengo hilo kwa kuchunguza lugha ya ishara iliyotafsiriwa katika *Shetani Msalabani*.

2.0 Nadharia na Mbinu za Utafiti

Makala hii yanasawiri lugha ya ishara iliyotafsiriwa katika riwaya ya *Shetani Msalabani*. Mbinu ya usaili na usomaji matini zilitumika kupata data za msingi zilizotumika katika makala hii. Data za msingi zilipatikana kwa kurejelea riwaya ya *Shetani Msalabani* na matini chanzi yake ambayo ni *Devil on the Cross*. Nadharia ya Ulinganifu wa Kimawasiliano imetumika kama kiunzi cha uchambuzi wa data zilizowasilishwa katika makala hii. Nadharia hii iliasisiwa na Nida (1964) na kuendelezwa na Catford (1965) na Nida & Taber (1969). Mkabala wake unasisitiza ulinganifu katika ujumbe na mtindo baina ya LC na LL. Pia, inalenga kuondoa tofauti zilizokuwepo baina ya utamaduni na isimu katika tafsiri. Nadharia hii imeleta mapinduzi katika tafsiri na kuifanya tafsiri kuwa zoezi la kisayansi. Jambo muhimu linalosisitizwa ni kuleta athari sawa kwa hadhira ya ML kama ilivyo kwa hadhira ya MC. Katika makala hii, nadharia hii imetumika kubainisha lugha ya ishara iliyotafsiriwa katika kitabu teule.

3.0 Lugha ya Ishara Iliyotafsiriwa katika *Shetani Msalabani*

Wafasiri wa matini za kifasihi, kwa kiasi kikubwa, huzingatia misingi ya nadharia ya Ulinganifu wa Kimawasiliano katika zoezi la kutafsiri. Makala hii yamebaini kuwa lugha ya ishara ambayo ni sehemu ya matumizi ya fani imesawiriwa kikamilifu katika riwaya ya *Shetani Msalabani*. Mjadala wa data

zilizowasilishwa umejikita katika vipengele vya wahusika wa kiishara, matukio ya kiishara na kichwa cha riwaya kama vilivyobainishwa katika sehemu inayofuata.

3.1 Wahusika wa Kiishara

Wamitila (2008) anaeleza kuwa wahusika ni watendaji katika kazi za fasihi. Wahusika wanaweza kuwa binadamu, wanyama, mimea, mizimu na viumbe vingine vinavyoweza kupewa kazi ya kiutendaji. Wahusika hutumiwa na watunzi wa kazi za kifasihi kufikisha ujumbe kwa hadhira waliyoikusudia. Wakati mwingine, watunzi hutumia wahusika wa kiishara kuwapa maana fulani ambayo wasomaji wanapaswa waing'amue. Wafasiri wa matini za kifasihi nao hutafsiri matini hizo kwa namna inayodumisha usanaa wa kifasihi ikiwa ni pamoja na kuwatafsiri wahusika na uhusika wao kwa namna inayoleta maana ya kiishara kwa wasomaji wa ML (Thomas, 2018). Wahusika wa kiishara wanaojitokeza katika kitabu teule ni Kaledi na Robin Mwaura. Wariinga anasema:

LC: *Take a girl like me, 'Wariinga said gazing down at one spot as if she were talking to herself. 'Or take any other girl in Nairobi. Let's call her Mahua Kareendi (uk. 17).*

LL: “Chukua mfano wa msichana kama mimi” Wariinga akasema huku anatazama chini kama kwamba anasema peke yake’ “Au chukua mfano wa msichana mwingine wa hapa Nairobi. Hebu tumwite **Maua Kaledi** (uk. 14).

Katika data hii, Wariinga amechukua nafasi ya kuwa msimulizi wa hadithi inayomhusu Maua Kaledi. Maua anapitia changamoto nyingi katika safari yake ya maisha, kiasi kwamba, anakata tamaa ya kuishi. Kaledi alipewa ujauzito akiwa kidato cha pili na kukataliwa na mtu aliyempa ujauzito. Wazazi wake wanamsomesha kozi ya ukarani kwa ngazi ya cheti na alipomaliza anaenda jijini Nairobi kutafuta kazi. Kaledi anafika Nairobi na kuanza kutafuta kazi. Anakumbana na changamoto ya kupata kazi kwa kuwa kila sehemu aliyoenda anaambiwa hakuna kazi. Baadhi ya sehemu wanataka atoe rushwa ya ngono. Inasimuliwa:

LC: *Our new Kenya, however, sings only one song to Kareendi: Sister Kareendi, the case of a fool takes a long time to settle. Sister Kareendi, every court session opens with feasting. Sister Kareendi, no man licks an empty hand. Take care of me, and I will take care of you. Modern problems are resolved with the aid of thighs. He who wishes to sleep is the one who is anxious to make the bed* (uk. 19).

LL: Kazi ataipata wapi? Hii Kenya inamwimbia Kaledi wimbo mmoja tu. Dada Kaledi, nipe nikupe. Dada Kaledi, tumbo kwanza. Dada Kaledi mkono mtupu haurambwi. Nifae nami nikufae. Mambo ya leo huhitimishwa mapajani! Mwamba ngozi huvuta upande wake! (uk. 18).

Katika nukuu hii, Kaledi anasisitiza kuwa nchini Kenya si rahisi kupata kazi hivihivi tu; ni lazima msichana atoe rushwa ya ngono. Baadaye, Kaledi anafanikiwa kupata kazi bila kutoa rushwa ya ngono, lakini kitu anachokumbana nacho akiwa kazini ni Mkurugenzi wake kumtaka kimapenzi. Mkurugenzi alitumia mbinu ya kumchelewesha kazini ili amchapie kazi yake. Baada ya Kaledi kubaki, Mkurugenzi alianza kumhadaa kwa maneno mazuri, akisema:

LC: *“Beautiful Kareendi, flower of my heart. No one but you can type them. ”No one but you can type them. For I want to send them care of the address of your heart, by the post of your heart, to be read by the eyes of your heart, thereafter to be kept within your heart, sealed there forever and ever. And you when you receive the letters, I beg you, don’t write Return to sender. Darling, flower of my heart, see how my love for you has weakened me?”* (uk. 21).

LL: Kaledi mrembo, kifu la moyo wangu. Hakuna mwingine anayeweza kuzipiga tapureta barua hizi isipokuwa wewe kwa sababu nataka kuzipeleka kwa anwani ya moyo wako zipitie katika sanduku la moyo wako, zisomwe na macho ya moyo wako, zidumu humo moyoni milele na milele. Nawe, ukisha kuzipokea usije ukasema, *Return to sender*. Mpenzi, kifu la moyo wangu, hebu nitazame uone ninavyosusurika kwa mapenzi yako! (uk. 20, 21).

Katika data hii, Mkurugenzi anamsifia Kaledi kuwa ni mrembo na hakuna mwingine anayeweza kuzipiga tapureta barua hizo, isipokuwa Kaledi. Mkurugenzi anamsifia ili ampate katika mahusiano ya kingono. Kaledi, baada ya kubaini nia hiyo, anamwambia kuwa atapiga kelele. Mkurugenzi baada ya kufikiria juu ya mke wake, watoto wake na uongozi wake kanisani anaamua amwache ili asije kuharibu heshima yake. Baada ya hapo, Kaledi anaamua kwenda nyumbani kwake. Kesho yake, Kaledi alichelewa kufika kazini kwa dakika chache. Mkurugenzi alitumia uchelewaji huo kama sababu ya kumfukuza kazi. Kaledi katika LL amekuwa ni mhusika wa kiishara kulingana na namna hadithi iliyosimuliwa na kuunda mkufu wa ishara.

Kaledi anawakilisha wanawake wengi wanaopata changamoto za kutafuta kazi na kukutana na madhila ya rushwa ya ngono. Wanawake hukumbana na wakati mgumu, hasa wanapolazimika kutoa rushwa ya ngono ili wapate ajira (Mattee, 2012). Rushwa ya ngono inadidimiza utu wa mtu na kuleta ukiukwaji wa haki. Mhusika wa pili ni Robin Mwaura. Robin amebeba lugha ya kiishara ndani yake. Robin Mwaura ni dereva wa gari inayojulikana kama Matatu Matata Matamu. Mwaura amesawiriwa kama dereva anayeitetea kazi yake na kulisifia gari lake kama wanavyoeleza:

LC: *But the matatu had a public relations officer in Mwaura. People would ask him: Mwaura, does this vehicle belong to the days of Noah? (uk.32).*

LL: Mwenyewe, Robin Mwaura, aliitetea sana watu walipoilaumu hiyo matatu yake. Walikuwa wakimwuliza: Hii matatu yako iliungwa wakati wa kizazi cha Nuhu? (uk. 35).

Nukuu hii inaonesha namna Mwaura alivyokuwa akiitetea matatu yake kutokana na chakavu wake. Mwaura anaonekana kuwa mbabe na mwenye kutumia maneno ya gubu kwa wasafiri wake wa matatu. Hali hii inaonekana pale anapomwambia Wangari:

LC: *I do not want any wrangling between us. This vehicle does not run on urine.’ (uk. 37).*

LL: Sitaki kelele hapa mama. Gari hili haliendeshwi kwa nguvu za mkojo! (uk. 42).

Mwaura aliyasema maneno haya kwa kuwa Wangari hakuwa na nauli ya kulipa. Uhusika wa Mwaura unabeba lugha ya ishara ambayo inawakilisha viongozi ambao kazi yao daima huwa kusifia kuwa taifa limepiga maendeleo, lakini katika hali ya kawaida si hivyo. Pia, anawakilisha viongozi wasio waadilifu katika nafasi zao kwa kuwa wanatumia madaraka yao kuwanyanyasa wanyonge. Jina Mwaura kwa lugha ya Gikuyu lina maana ya mwizi (Waigoko, 2002). Mwaura anashabihiana vilivyo na maana ya jina hilo kutokana na matendo anayotenda. Mwaura anawakilisha watu wasio na utu ndani yao kwani alishiriki kuwaua wale waliokuwa kinyume na karamu ya shetani. Ismail (2019) anasisitiza kuwa suala hili ni kinyume kabisa na utu na halifai kuendelea kufanyika katika jamii.

3.2 Matukio ya Kiishara

Kazi za kifasihi hubeba visa na matukio mbalimbali. Kuna wakati, matukio hayo husanwa kwa namna ya kutumia lugha ya ishara ambayo, kutokana na uelewekaji wake, wasomaji huweza kung'amua maana za kiishara zilizokitwa katika matukio hayo. Utafiti uliofanyika, umebaini kuwa lugha ya ishara iliyotafsiriwa katika *Shetani Msalabani* kupitia tukio la Wariinga kujichubua, Kaledi kutafuta ajira, Mwireri kuliacha jina la Kizungu, Kihaaku kubadilisha jina la shule, watoto wa Kihaahu kuzungumza Kiingereza na Gitutu kushikilia jina la Kizungu. Kwa mfano, Jacinta Wariinga (msichana mwenye ngozi nyeusi) anaonekana hapendezwi na rangi ya ngozi yake. Hivyo, anajaribu kuibadili. Hali hii inajitokeza pale inapoandikwa:

LC: *Wariinga was convinced that her appearance was the root cause of all her problems. Whenever she looked at herself in the mirror she thought herself very ugly. What she hated most was her blackness, so she would disfigure her body with skin-lightening creams like Ambi and Snowfire, forgetting the saying: That which is born black will never be white (uk. 11).*

LL: Wariinga daima alifikiri kuwa sura yake mbaya ndiyo iliyokuwa chanzo cha taabu zake. Kila alipojitazama kiooni alijiona kuwa ana sura mbaya sana. Aliudharau sana weusi wake. Alikuwa akiharibu ngozi yake kwa madawa ya Ambi

na Snowfire ati akitaka kuiondolea mbali hiyo rangi nyeusi (uk. 5, 6).

Data hii inaonesha kuwa Wariinga hakuikubali rangi yake nyeusi na kuchukua maamuzi ya kuharibu rangi yake kwa kutumia madawa ya Ambi na Snowfire. Waafrika wameamini kwamba weusi ni ishara ya udhaifu na weupe ni ishara ya uthabiti (Muhia na Kisurulia, 2019). Tukio la Wariinga kujichumbua ngozi yake linaashiria ukosefu wa uzalendo kwa kutopenda Uafrika. Hali hii inaenda mbali zaidi na kuonesha namna ukoloni mamboleo na ufungwa wa kifikra ulivyotamalaki katika nchi nyingi za Kiafrika. Wanawake wengi wa Kiafrika wamekuwa hawathamini ngozi zao nyeusi ndiyo maana wamekuwa wakitumia madawa mbalimbali ya kubadilisha ngozi ili wafanane wa Wazungu. Suala hili linajitokeza kwa sababu wametawaliwa kifikra kwa kuona rangi ya Wazungu ina thamani kuliko yao. Hivyo, nao wanafanya kila namna waweze kufanana na Wazungu hao.

Tukio la pili ni kitendo cha watoto wa Kihaahu kuzungumza Kiingereza. Kihaahu wa Gatheca katika ushahidi wake akiwa kwenye karamu ya shetani anaonekana akiwasifia watoto wake kuwa wanazungumza Kiingereza vizuri. Anasema:

LC: *‘As for my children, I have quite few. All of them speak Eanglish through the nose, exactly like people born and brought up in England. If you were to hear them speak Gikuyu or Kiswahili, you would laugh until you pissed yourself (uk. 109).*

LL: “Kwa upande wa watoto, ninao wengi. Wote huzungumza Kiingereza kama kwamba walizaliwa Uingereza na Wakalelewa huko huko. Ukiwasikia wakizungumza Kikuyu au Kiswahili unaweza kucheka mpaka uvunjike mbavu au pengine ujikojolee (uk. 145).

Maelezo katika nukuu yanaonesha namna Kihaahu anavyowasifia watoto wake wakizungumza Kiingereza. Pia, anaeleza kwamba watoto hao hawajui lugha ya Kikuyu ambayo ndiyo lugha yao mama na lugha ya Kiswahili. Hali hii inaashiria Kihaahu anasujudu utamaduni wa Kizungu. Kihaahu anaona ni umaarufu kwa watoto wake kujua Kiingereza, lakini hashangazwi na wao kutojua lugha yao mama. Waafrika wengi, bado wapo kwenye ukoloni mamboleo ambao umeimarika kwenye fikra zao. Wanashindwa kuthamini

utamaduni wao. Wanaendeleza utamaduni wa kigeni. Kujisifu kwa kuongea Kiingereza ni tabia iliyozeleka miongoni mwa Watanzania, hasa wasomi (Wafula, 1999). Hali ya kutukuza lugha ya Kiingereza husababisha wazazi wengi kuwakazania watoto kufahamu lugha ya Kiingereza kuliko kufahamu lugha zao za asili au za kijamii.

3.3 Kichwa cha Riwaya

Miongoni mwa lugha ya ishara iliyotafsiriwa katika riwaya teule ni kichwa cha riwaya kinachosomeka *Shetani Msalabani*. Kichwa hiki kimetafsiriwa kutoka katika kichwa cha MC ambacho ni *Devil on the Cross*. Kichwa hiki, *Shetani Msalabani* kimebeba maana mbalimbali ambazo zinapatikana katika dhana kuu tatu za ushetani, msalaba na shetani msalabani. Mosi, kuhusu dhana ya shetani, shetani ni malaika aliyekuwa na cheo cha juu aliyefukuzwa baada ya kuasi amri za Mungu (BAKITA, 2016). Shetani anasadikika kuwa ndiye chanzo cha maovu. Katika riwaya hii, Shetani anajidhihirisha kupitia matukio mbalimbali. Baadhi yake ni Wariinga akiota akiongeleshwa na sauti:

LC: *Wariinga: Those voices that I hear raised in self-praise in the cave - are they singing hymns to you?*

Voice: *Ah, those. Those are all my followers. Their cunning is a gift from me, and in exchange they have given me their souls to keep (uk. 192).*

LL: *Wariinga: Hao wote niliwasikia wakiutapia wizi na unyang'anyi humo pangoni wanakutukuza wewe tu?*

Sauti: *Hao? Hao wote ni wafuasi wangu. Hila zao na ujuzi wote walio nao nimewapa mimi; na kwanza walinipatia mioyo yao niwawekee (uk. 264).*

Majibizano hayo katika ya Wariinga na Sauti yanadhihirisha kuwa hiyo sauti ni shetani anayemjaribu Wariinga kwa kumuahidi kuwa atafanikiwa kimaisha kama atakubali kuwa mfuasi wake. Wariinga anaonekana kukataa kuwa mtumwa wa shetani. Shetani ni malaika aliyeanguka baada ya kukataa kwa hiari kumtumikia Mungu na mipango yake (Al-Farsy, 1991). Hivyo, tunaweza kusema kuwa shetani ni muasisi wa dhambi ulimwenguni. Kupitia maelezo haya, shetani anawakilisha ubaya na mambo yanayohusiana na hayo. Katika

riwaya teule, shetani anawakilisha viongozi na watu wenye kutenda maovu yanayohusiana na uasi. Pili, kuna dhana ya msalaba ambayo inaonekana katika kichwa cha riwaya. Chipalo (2021) anashadidia:

Msalaba ni neno ambalo kwa maana ya kawaida linatoa picha ya mistari miwili inayopishana na kukutana katikati. Neno hili linahusianishwa zaidi na dini ya Kikristo. Hali hii inatokana na tamaduni za Wayunani ambao walikuwa wakitumia misalaba kutoa adhabu ya kifo kwa wakosaji. Katika dini ya Kikristo, Yesu alisulubiwa msalabani kwa ajili ya watu wenye dhambi. Kutoka hapo, msalaba ukatumika kama ishara ya Ukristo ambayo ndani yake imebeba dhana ya ukombozi.

Maneno haya yanadokeza dhana ya msalaba imejitokeza katika kichwa cha riwaya teule. Msalaba ni muunganiko wa kulingana wa vipande viwili vya mbao, mmoja mrefu na mwingine mfupi, ambao waumini wa dini ya Kikristo huamini kuwa Yesu Kristo alibebeshwa, kisha kutundikwa juu yake ili asulubishwe (BAKITA, 2016). Katika riwaya teule, tunaona namna ukinzani wa kidhana unavyojitokeza kupitia kichwa hiki kinachoibua lugha ya ishara iliyojaa taharuki ya kufuatilia kisa cha shetani kusulubiwa msalabani badala ya Yesu kama ilivyoeleweka katika jamii za ulimwengu.

Pia, dhana ya shetani na ushetani inahusianishwa na msalaba. Wariinga alienda kanisani na kuangalia picha za Yesu akisulubiwa msalabani, lakini akirudi nyumbani anaota shetani ndiye anayeteswa msalabani. Anasema:

LC: *At night Wariinga would have a recurrent nightmare. Instead of Jesus on the Cross, she would see the Devil, with skin as white as that of a very fat European (uk. 139).*

LL: Usiku alikuwa akishikwa na jinamizi kwa sababu ya mapicha hayo. Lakini, badala ya kuota Yesu msalabani, alikuwa akimwota shetani mwenye ngozi nyeupe kabisa kama ya Mzungu mmoja (uk. 188).

Katika data hii, ndoto ya Wariinga inakinzana na kile alichokiona kanisani. Kuna ishara zinazingatia misingi ya kidini na kifasihi. Utafiti umebaini kuwa anayesulubiwa kwa muktadha wa riwaya hii ni shetani siyo Yesu Kristo. Dhana ya shetani kusulubiwa msalabani imebeba lugha ya ishara inayomaanisha kuwa

shetani anasulubishwa msalabani ili awaokoe wezi na wanyang'anyi wanaojipatia mali zao kwa njia isiyo halali. Dhana hii imetumika kama ukinzani wa hali inayofahamika kuwa Yesu Kristo alisulubiwa msalabani kwa ajili ya kuwakomboa wenye dhambi. Ktika riwaya hii, shetani ndiye anayesulubishwa kwa ajili ya kuwakomboa wezi na wanyang'anyi. Hali hii inadhihirisha kuwa wezi na unyang'anyi haujaondolewa kwa kuwa shetani alisulubiwa msalabani ili wezi na wanyang'anyi wapate kupona.

4.0 Hitimisho

Makala hii imemakinikia usawiri wa lugha ya ishara iliyotafsiriwa katika *Shetani Msalabani*. Makala imebaini kuwa wafasiri wa kazi za kifasihi hutafsiri kwa namna ya kudumisha umbo la kisanaa ili kuifanya ML ipate vionjo kama ilivyo katika MC. Hali hii ni kwa sababu zoezi la kutafsiri kazi za kifasihi ni tofauti na kutafsiri matini zisizo za kifasihi. Waandishi wa kazi za kifasihi husana kazi zao kwa kuzingatia misingi ya fani na maudhui. Makala inapendekeza wafasiri wa kazi za kifasihi kutopuuza lugha ya ishara katika tafsiri. Riwaya ya *Shetani Msalabani* ni zao la tafsiri ikiwa na lugha ya ishara inayofikisha ujumbe kwa wasomaji.

Marejeleo

Al-Farsy, S. S. (1991). *Kurani Tukufu* (Tafsiri). Nairobi: East African Literature Bureau.

BAKITA (2016). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Longhorn Publishers.

Cartford, J. (1965). *A Linguistic Theory of Translation*. London: Oxford University Press.

Jilala, H. (2016). Uchambuzi wa Nadharia ya Ulinganifu katika Fasihi katika Jilala, H. (Mh.) *Nadharia za Tafsiri, Ukalimani na Uundaji wa Istilahi*. Dar es Salaam: Daud Publishing Limited.

Malangwa, P. (2005). *Problems of Translating Literary Works: The Case of Julius Kambarage Nyerere's Translation of the Play Mabepari wa Venisi*. MA Dissertation, University of Dar es Salaam.

- Mattee, S. (2012). *Usawiri wa Rushwa ya Ngoni katika Riwaya za Kiswahili: Mifano Kutoka Kiu (1972) na Usiku Utakapokwisha (1990)*. Tasinifu ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Mekacha, R. D. K. (2013). Tafsiri ya Ushairi katika Mwansoko na Wenzake. *Kitangulizi cha Fasihi. Nadharia na Mbinu*. Dar es Salaam: TUKI.
- Mosha, D. (2017). Lugha ya Ishara katika Dhifa za Jikoni Nchini Tanzania katika *Kioo cha Lugha* Vol 15, No 1. Dar es Salaam: TUKI.
- Muhia, A., & Kisurulia, S. (2019). Utandawazi na Elimu Tumizi Barani Afrika: Haja ya Mustakabali Mpya kwa Mujibu wa *Dunia Yao, Msimu wa Vipepeo* na *Nakuruto*. *East African journal of Swahili Studies* 4:68-79.
- Mpemba, T. (2016). Nadharia za Tafsiri katika Jilala, H. (Mh.). *Nadharia za Tafsiri, Ukalimani na Uundaji wa Istilahi*. Dar es Salaam: Daud Publishing Limited.
- Mwansoko, H. J. M., na wenzake. (2006). *Kitangulizi cha Tafsiri. Nadhania na Mbinu*. Dar es Salaam: TUKI.
- Nida, E., & Taber, C. R. (1969). *The Theory and Practice of Translation*. Shanghai: Foreign Language Education Press.
- Wa Thiong'o. N. (1982). *Devil on the Cross*. Johannesburg: Heineman.
- Wa Thiong'o. N. (1982). *Shetani Msalabani* (Mfasiri). Nairobi: East African Educational Publishers.
- Wafula, R. M. (1999). *Uhakiki wa Tamthilia: Historia na Maendeleo yake*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.
- Wamitila, K. W. (2010). *Kanzi ya Fasihi 1: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide Muwa Publishers.
- Yegon, M. C. (2016). Uwasilishaji wa Ufeministi Kinzani katika Kiswahili Kupitia Tafsiri: Tathmini ya Riwaya ya *Barua Ndefu Kama Hii*. Tasinifu ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Utata katika Ufasiri wa Maana za Sitiari za Kiswahili

Mofart Onyoni Ayiega
Chuo Kikuu cha Kenyatta
mofartayiega94@gmail.com

Ikisiri

Makala hii imechunguza utata katika ufasiri wa maana za sitiari za Kiswahili. Data ya makala hii ilisakurwa mtandaoni kutoka kwa tafiti za awali, majarida na makala kwa kuongozwa na sampuli lengwa. Data ilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji makini. Ili kubaini utambuzi wa msikilizaji na msomaji ujumbe, mtafiti aliwaomba wazungumzaji 12 wa Kiswahili kufasiri maana ya sitiari husika kwa kuongozwa na maswali ya mahojiano huru. Nadharia ya Semantiki Tambuzi ilitumiwa katika uchambuzi wa data ya utafiti huu. Matokeo ya utafiti huu yalibaini kuwa utata katika ufasiri wa maana za sitiari za Kiswahili husababishwa na tajriba na maarifa ya mpokeaji ujumbe, muktadha wa matumizi ya sitiari, elimu, taswira na mazingira ya mpokeaji ujumbe. Pia, makala hii yameeleza namna uhamishaji wa maana hutokea katika uundaji wa maana katika sitiari inayohusika. Uchunguzi huu ulitambua kuwa hakuna maana mahsusi ya sitiari kwa kuwa maana zake huwa ni dhana zilizo akilini mwa binadamu. Makala hii inapendekeza kwamba ni vyema sitiari kufasiriwa bila kujikita katika maana moja.

Istilahi za Msingi: Sitiari, utata, semantiki, isimu tambuzi na uhamishaji maana.

1.0 Utangulizi

Kusudi la makala hii ni kubaini sababu za sitiari za Kiswahili kuzua utata katika ufasiri wa maana katika mawasiliano ya kila siku. Sitiari ni tamathali inayotumia ulinganishi wa vitu viwili ambavyo ni tofauti kitabia na kimaumbile vinafananishwa kwa njia isiyo ya moja kwa moja (Mbatiah, 2001). Sitiari ni

MAKALA HALISI HISTORIA YA MAKALA

Kupokelewa: 04 Machi
2022

Kurekebishwa: 24 Julai
2022

Kukubaliwa: 29 Julai
2022

Kuchapishwa: 20
Septemba 2022

ISSN: 2799 – 2187

Juzuu 1,

Toleo 1,

uk. 77 – 91.

NUKUU

Ayiega, M. O. (2022). Utata katika Ufasiri wa Maana za Sitiari za Kiswahili. *Jarida la Fahari ya Kiswahili*, 1(1), 77 – 91.

tamathali ya semi inayolinganisha vitu viwili vyenye uhusiano fulani kisemantiki. Pia, hutumika katika fikra na matendo ya maisha ya kila siku (Lakoff & Johnson, 1980). Mada ya makala hii inapatikana katika eneo la semantiki linaloshughulikia maana za maneno au tungo katika lugha.

Löbner (2013) anaeleza kuwa semantiki ni sehemu ya isimu inayohusika na maana. Maana ni dhana yenye matumizi mengi. Maneno huwa na maana kama ilivyo katika virai na sentensi. Katika lugha ya Kiswahili maana huwasilishwa kwa mbinu mbalimbali. Mbinu hizi huwa na utaratibu maalumu wa kuzalisha maumbo yenye sifa tofauti tofauti. Mbinu hizo ni kama vile tashibihi, tashihisi, methali na sitiari (Mwakio, 2016). Mbinu ya sitiari inahusika na kuhamisha maana ya sifa, tabia, sura na muundo fulani kutoka kwa kitu kimoja kwenda kwa kitu kingine.

Ullmann (1967) anasema kuwa ulinganisho wa vitu viwili katika sitiari huzua aina nne za uhamishaji. Mathalani, uhamishaji wa maana unaomhusu binadamu na viungo vyake vya mwili pamoja na vitu visivyo na uhai. Pili, uhamishaji wa maana wa kuweka tabia za wanyama kwa binadamu. Tatu, uhamishaji unaohusisha vitu halisi kwenda kidhahania na kinyume chake. Mwisho, uhamishaji wa maana unaohusika na milango ya fahamu. Uhamishaji huu, huunda sitiari ambazo katika semantiki hukiuka kanuni za kisemantiki katika mchakato mzima wa kuunda tungo hizi. Ukiukaji unaorejelewa hapa ni kama vile maana kama ukweli, ugeuzaji na urejeleaji. Hali hii ya ukiukaji wa kanuni za kisemantiki huzua utata wakati sitiari hizi zinapotamkwa na msikilizaji au msomaji wa taarifa hizo. Matokeo yake, hukosa kusimbua kile kinachokusudiwa na mnenaji. Utata tunaorejelea hapa, ni ugumu wa kufahamika vyema kwa kitu kinachorejelewa.

Katika matumizi ya sitiari za Kiswahili, hasa pale ambapo sitiari zinatamkwa, maana ya kileksika hufasiriwa kwanza kabla ya maana yoyote ya kitamathali. Maana ya kitamathali hutumiwa pale ambapo hutokea utata wa kisemantiki kwenye ufasiri na hili hudhihirisha sitiari kuwa na ukiukaji wa kanuni za kisemantiki wa aina fulani na ukiukaji huu ndio unaojitokeza kama utata. Hivyo, humfanya mpokeaji ujumbe kutafuta ufasiri wa ziada. Maana ya kitamathali huhitaji kufasiriwa kwa makini (Gaichu, 2016). Kutokana na maoni ya Gaichu ni wazi kuwa maana ya kitamathali hutegemea tajriba ya mpokeaji

ujumbe na huhitaji data za kiensaiklopedia ili kutatua utata huu. Jedwali 1 lifuatalo linadhihirisha jinsi utata katika ufasiri wa maana za sitiari hutokea.

Jedwali 1: Sitiari Zinazodhihirisha Utata katika Ufasiri wa Maana

Sitiari	Maana Kileksika	Maana Kitamathali
Mwanamke ni nguo	Vazi	Urembo, pambo, kinga mwili kutokana na baridi na kitambaa kilichoshonwa.
Aga dunia	Tamko la kwa heri	Kufa, maradhi yanapozidi, tamko la buriani na ajali.

Jedwali 1 linadhihirisha wazi kuwa sitiari hizi zina utata wa kufasiri maana kutokana na muundo wa sentensi ambazo kwa kiasi unaonesha kukosa mantiki na ukweli. Kwa mfano, ‘mwanamke ni nguo’ na ‘aga dunia’. Nomino *nguo* na kitenzi *aga* zinapotajwa fasiri ambazo hutolewa na mpokeaji ujumbe ni zile za kileksika, yaani *vazi* na *tamko la kwa heri*. Hata hivyo, ili maana za maneno haya kufasiriwa, maana za kitamathali hutolewa zinazotegemea maarifa ya msimbuaji anayepokea ujumbe huo. Kwa kuwa kila mtu ana maarifa na tajriba tofauti, kwa kawaida, kunazuka fasiri mbalimbali za maana na huzua utata katika matumizi kwani hatuwezi kujifunga katika fasiri ya maana moja. Kutokuwa na fasiri moja ya sitiari ndilo suala ambalo makala hii yalichunguza kwa kudhihirisha kuwa ufasiri wa maana za sitiari ni tata.

Mada ya makala hii yalichaguliwa ili kueleza namna maana za sitiari hufasiriwa na utata unaotokea katika matumizi yake. Sitiari ziliteuliwa na mtafiti kutokana na pengo lililobainika la kutoangalia sitiari katika mtazamo wa kiutambuizi. Maana za sitiari hutazamwa kama dhana zilizo akilini mwa binadamu na fasiri za maana za sitiari hutegemea miktadha ya matumizi ya sitiari, mazingira, elimu na taswira anayopata mpokeaji ujumbe anaposikia au kusoma sitiari. Sitiari hazina maana moja mahsusi.

2.0 Mapitio ya Tafiti Tangulizi

Akichunguza kuhusu miundo ya kisarufi ya lugha ya kitamathali, Muna (2017) alieleza jinsi sitiari za Kiswahili huundwa kwa kuelekezwa na nadharia tatu za

dhana ya nadharia ya Sitiari, Sarufi Tambuzi na Sarufi ya Ujenzi. Katika uchunguzi wake, alieleza namna sitiari huundwa kisarufi na kufasiriwa. Aidha, alibainisha ni kwa kiwango gani sitiari hueleza muktadha wa kitamaduni wa kijamii na tajiriba zinazojumuisha watumiaji wa lugha. Utafiti wake ulijikita katika kubaini maumbo ya sitiari, tofauti na mada yetu inayolenga kueleza utata katika ufasiri wa maana za sitiari.

Kitundu & Malangwa (2020) wakichunguza maumbo ya maana katika sitiari na tashibiha za Kiswahili, walibaini uwepo wa namna maalumu inayotawala ujenzi wa maana katika vipengele hivyo. Kila kipengele kikiwa na namna yake inayohusisha mwingiliano wa elementi mbalimbali. Pia, walieleza muundo wa maana za sitiari kwa kuongozwa na elementi tatu za mada, kibebeo na sifa bia. Tofauti na utafiti wa Kitundu na Malangwa uliotumia mkabala wa Mwingiliano katika mjadala na uchambuzi wa data. Makala hii ilitumia nadharia ya Semantiki Tambuzi kueleza utata katika ufasiri wa maana za sitiari za Kiswahili.

Akichunguza kuhusu mabadiliko ya maana katika leksia, Gichuru (2020) alibaini namna maana za leksia za Kiswahili hufasiriwa kwa kuongozwa na nadharia za Semantiki Tambuzi na Vikoa Maana. Kutokana na utafiti wake, mojawapo ya athari alizotambua za kubadilika kwa maana za leksia ilikuwa ni kuongezeka kwa lugha ya sitiari. Pia, alieleza kuwa maana ya leksia fulani haiwezi kueleweka kikamilifu bila kuhusisha maarifa ya kiensaiklopedia ya leksia hiyo. Uchunguzi huu ulifaa mtafiti kuelewa jinsi maana za sitiari hufasiriwa na kuelewa zaidi nadharia ya Semantiki Tambuzi iliyotumiwa katika makala hii.

Wakieleza ukiukaji wa kanuni za kisemantiki katika matumizi ya lugha, Mwita na Malangwa (2019) walibaini mojawapo ya ukiukaji huu kuwa ukinzani. Pia, walitambua sentensi kuzungumzia kitu kisicho cha kawaida kwa kujiondoa kwa mambo yanayotarajiwa au yanayokinzana na ukweli jinsi unavyofahamika. Walieleza kuwa sentensi zenye ukinzano huwa hazina maana katika maisha ya kila siku. Ili kufahamu ukinzano huo, inabidi mtu awe na habari muafaka kuhusu neno linalohusika. Ukinzano hutokea katika matumizi ya sitiari ambapo maana ya sitiari hufasiriwa kwa kuzingatia uelewa wa msemaji na msikilizaji wa kufasiri yanayosemwa katika muktadha fulani. Pia, walitambua aina tatu za

ukiukaji wa kanuni za kisemantiki katika sitiari. Aina hizo ni maana ni ukweli, ugeuzaji na urejeleaji. Maarifa kutoka kwa wataalamu hawa yalikuwa ni msingi wa kutambua maarifa yaliyoshughulikiwa.

Mwakio (2016) akitafiti kuhusu matumizi ya tashibiha, sitiari na taashira, alibaini jinsi vipengele vya tamathali vinavyojenga maudhui katika antholojia ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* kwa kuelekezwa na nadharia ya Uhakiki wa Kimtindo. Katika uwasilishaji wa matokeo ya uchunguzi wake, aliorodhesha tashibiha, sitiari na taashira ili kuyafikia malengo aliyokusudia kutimiza. Utafiti wa Mwakio ulijikita katika fasihi ya Kiswahili. Utafiti wake, kwa kiasi kikubwa, umefanikisha utafiti huu kupata data ya kuthibitisha uwepo wa suala lililoshughulikiwa.

Akitafiti kuhusu namna lugha inavyotumika katika methali za sitiari za Kiswahili kwa kuongozwa na nadharia ya Uhusiano, Gaichu (2016) alitambua jinsi maana halisi ya neno inavyoweza kubadilika na kuchukua maana nyingine tofauti na maana ya kiisimu ya neno linalohusika. Alitambua kuwa maana ya leksimu hubadilika na maana mpya huzuka kutokana na sheria za mawasiliano, kaida tambuzi na muktadha ambapo neno hilo hutokea. Gaichu aliainisha sitiari katika utafiti huu kwa kujikita katika maoni ya Sperber na Wilson (1995), Lakoff na Johnson (1980) na Shelestiuk (2006). Mapitio haya yamechunguza muundo wa sitiari na maana za leksimu katika lugha ya Kiswahili. Makala hii imechunguza utata katika ufasiri wa maana za sitiari za Kiswahili.

3.0 Nadharia na Mbinu za Utafiti

Data za msingi za makala hii zilisakurwa mtandaoni kutoka kwa tafiti za awali, majarida na makala kwa kuongozwa na sampuli lengwa. Data ilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji makini. Makala hii ilitumia sampuli ya kimakusudi kuteua sitiari zilizotumika katika mjadala wa data zilizowasilishwa. Katika makala hii sitiari 30 pekee ziliteuliwa ili kuthibitisha uwepo wa utata katika ufasiri wa maana za sitiari za Kiswahili. Ili kubaini utambuzi wa msikilizaji na msomaji ujumbe, mtafiti aliwaomba wazungumzaji 12 wa Kiswahili kufasiri maana ya sitiari husika kwa kuongozwa na maswali ya mahojiano huru. Wahojiwa hawa walikuwa wanafunzi wa Kiswahili wa Shahada ya Kwanza (4), Shahada ya Uzamili (4) na Shahada ya Uzamifu (4). Uteuzi ulizingatia maoni ya

Milroy (1987) anayependekeza matumizi ya sampuli ndogo katika uchunguzi wa lugha ili kuepuka kuzua matokeo yenye urudufu mwingi.

Nadharia ya Semantiki Tambuzi iliongoza katika uchambuzi wa data ya utafiti huu. Nadharia hiyo iliasisiwa na Lakoff (1987) na kuendelezwa na Lemmens (2017) miaka ya 1980 kama sehemu iliyopinga maelezo kuwa semantiki ilibuniwa baada ya sintaksia kama ilivyodaiwa katika nadharia zalishi za lugha. Semantiki Tambuzi ni sehemu pana ya Isimu Tambuzi yenye asili katika saikolojia tambuzi (Vyvyan, 2006). Isimu Tambuzi ni mtazamo unaochunguza uhusiano kati ya maumbo ya lugha, akili na maumbo yanayopatikana katika mazingira na jamii. Semantiki Tambuzi husisitiza kuwa utambuzi wa lugha ni utambuzi tu. Katika makala hii, nadharia hii imetumika kueleza maana za leksimu kuwa akilini.

4.0 Matokeo ya Utafiti

Makala hii ilibaini utata katika ufasiri wa maana ya sitiari za Kiswahili zinapotumiwa katika mawasiliano. Mtafiti alitambua kuwa maana za sitiari huwa si mahsusi kwa kuwa ni dhana zinazotegemea utambuzi wa msikilizaji na msomaji ujumbe unaokusudiwa kuwasilishwa. Uchunguzi huu ulibaini utata wa ufasiri wa maana katika sitiari za Kiswahili hutokana na kuwepo kwa sababu mbalimbali. Baadhi yake ni tajriba na maarifa ya mpokeaji ujumbe, miktadha ya matumizi ya sitiari, elimu, taswira na mazingira ya mpokeaji ujumbe kama zilivyofafanuliwa katika sehemu inayofuata.

4.1 Mazingira ya Mpokeaji Ujumbe

Kutokana na uchanganuzi wa data ya utafiti huu, mtafiti alitambua sitiari zifuatazo katika Jedwali 2 kuwa na maana zinazotegemea mazingira ya mpokeaji ujumbe.

Jedwali 2: Sitiari Zinazotegemea Mazingira ya Mpokeaji Ujumbe

Sitiari	Maana ya Kileksika	Maana ya Kitamathali Kulingana na Mazingira ya Mpokeaji Ujumbe
Mkono wa saa	Sehemu ya mwili ya binadamu ya kushikia kitu.	Sehemu ya saa ya kuonesha wakati.
Mguu wa	Sehemu ya mwili wa	Sehemu za kusimamishia

kitanda	binadamu ambayo hutumia kutembelea.	kitanda.
---------	-------------------------------------	----------

Aina ya sitiari katika jedwali 2 hudhihirisha uhamishaji wa maana ambao unaohusika na viungo vya mwili vya binadamu kufananishwa na vitu vingine. Sitiari zilizoordheshwa zinadhihirisha ugumu wa kufahamika vyema kwa kitu kinachorejelewa. Mpokeaji ujumbe anastahili kuwa na ensaiklopedia ya nomino *mkono* na *mguu* ili kufasiri dhana inayokusudiwa katika sitiari hizi. Kwa kawaida, leksimu hizi zinapotumika katika mazingira ya kawaida huashiria sehemu za mwili. Sitiari hizi hukiuka kanuni ya kisemantiki ya maana kama ukweli ambapo kwa ufahamu wa kawaida leksimu *saa* na *kitanda* haziwezi kuwa na *mkono* na *mguu*. Ili kuelewa leksimu hizi husababisha kuzuka kwa maana za kitamathali zinazotegemea mazingira ya mpokeaji ujumbe.

Sitiari *mkono wa saa* na *mguu wa kitanda*, ufasiri wa maana za kitamathali wake hujengeka akilini mwa msomaji au msikilizaji. Sitiari hizi hufasiriwa kuwa sehemu ya saa ya kuonesha wakati na sehemu za kusimamishia kitanda. Kutokana na data ya mahojiano huru, mtafiti alibaini kuwa baadhi ya watafitiwa walikuwa na saa za kisasa ambazo hazina mkono na hivyo, kubaini kuwa sitiari *mkono wa saa* ina utata iwapo dhana *mkono* inayorejelewa hapa haizuki katika akili ya mpokeaji ujumbe. Data ya mahojiano huru ilibaini uwepo wa utata wa sitiari *mguu wa kitanda* ambapo baadhi ya wahojiwa walieleza kuwa vitanda vya mguu havipo tena na kama vipo karibuni vitapotea kutokana na ujio wa teknolojia. Msamiati wa lugha huakisi kwa uwazi zaidi mazingira ya kimaumbile na ya kijamii ya wazungumzaji wake (Sapir, 1912). Maana ya kitamathali huhitaji kufasiriwa kwa makini ili kupata maana iliyokusudiwa katika sitiari yenyewe (Geeraerts, 2006; Gaichu, 2016 & Lemmens (2017). Maana hujumuisha maana msingi na pamoja na fahiwa zake zote. Hivyo, ufasiri wa maana ya sitiari hutegemea mazingira ya mpokeaji au msomaji ujumbe husika.

4.2 Maarifa na Tajriba ya Mpokeaji Ujumbe

Sitiari ambazo zilizodhihirisha maana zake kufasiriwa kwa kutegemea maarifa na tajriba ya mpokeaji ujumbe kutokana na data ya mahojiano huru kama zifuatazo katika Jedwali 3.

Jedwali 3: Sitiari Zinazotegemea Maarifa na Tajriba ya Mpokeaji Ujumbe

Sitiari	Maana Kileksika	Maana ya Kitamathali Kulingana na Maarifa na Tajriba ya Mpokeaji Ujumbe
Juma ni nyoka	Mnyama wa porini asiye na miguu anayetambaa.	Sumu, mtu asiyeaminika, hatari na mlaghai kutokana na dhana ya kurejelewa katika Biblia.
Fatuma ni simba	Mnyama wa porini ambaye ni jamii ya paka mwenye manyoya ya rangi ya majani makavu.	Mtu mkali, kiongozi na mbabe na shujaa.

Sitiari katika jedwali 3 zinaonesha hali ya tabia ya wanyama kunashibishwa sifa za binadamu. Kitundu & Malangwa (2020) wanaeleza kuwa sitiari za aina hizi huwa na tabia za wanyama kujitokeza katika sifa za binadamu. Ufasiri wa maana wa sitiari hizi haujikiti katika maana za msingi za leksimu ‘nyoka’ na ‘simba’ yaani wanyama wa porini, bali hutegemea fasiri zilizo akilini mwa binadamu. Pia, hutegemea maarifa na tajriba ya mpokeaji ujumbe ili kupata maana iliyokusudiwa. Muna (2017) anaeleza kuwa maneno hayawasilishi maana zinavyoonekana katika kamusi, isipokuwa huwa kama mlango wa kufikia hifadhi kubwa ya maarifa kuhusiana na dhana fulani.

Kutokana na leksimu hizo, tunaweza kusema kuwa, sitiari *Juma ni nyoka*, inaashiria sumu, mtu asiyeaminika, hatari na mlaghai kutokana na dhana ya kurejelewa katika *Biblia*. Pia, sitiari *Fatuma ni simba* inaweza kufasiriwa kuwa mtu mkali, kiongozi, shujaa na mbabe. Hapa ni vyema kuweka wazi kuwa maana za kitamathali za sitiari hizi hazina maana mahsusi kwa kuwa ufasiri wa sitiari hizi hutegemea utambuzi wa maana za mpokeaji ujumbe. Maoni yanayoingiliana na data ya mahojiano huru, ambapo mtafiti alibaini wahojiwa wa Kiswahili wa Shahada ya Kwanza, Shahada ya Uzamili na Shahada ya Uzamifu kutofautiana katika kufasiri maana ya sitiari inayohusika. Kutokana na hali hiyo, Onish & Murmpy (1993) wanaeleza kuwa sitiari zinaweza kuwa na fasiri mbalimbali na zinahitaji data za kiensaiklopedia ili kutatua utata katika matumizi yake.

4.3 Taswira Anayopata Mpokeaji Ujumbe

Kutokana na uchanganuzi wa data ya mahojiano huru iliyokusanywa katika makala hii, mtafiti alibaini sitiari zenye kutegemea taswira anayopata mpokeaji ujumbe anaposimbua maana zake. Jedwali 4 lifuatalo limeorodhesha sitiari zinazotegemea taswira anayopata mpokeaji ujumbe katika ufasiri wa maana za sitiari.

Jedwali 4: Sitiari Zinazotegemea Taswira Anayopata Mpokeaji Ujumbe

Sitiari	Maana ya Kileksika	Maana ya Kitamathali Kulingana na Taswira Anayopata Mpokeaji Ujumbe
Ujana ni moshi	Wingu linalotoka baada ya moto kuwaka.	Ujana unafananishwa na moshi, kuashiria kuwa ukienda haurudi. Ujana huwa na mambo chungu nzima ambayo yanahitaji busara.
Kamusi ni pori	Mahali ambapo wanyama wa mwituni huishi.	Kuwa na mambo mengi, binadamu hawezi kuitalii kamusi sawa na pori akalimaliza.
Elimu ni ngao	Kifaa cha kukinga mtu kutokana na adui wakati wa vita.	Elimu inafananishwa na ngao, uashiria mtu akiwa na elimu anaweza kuwa na mali. Aidha, anaweza kutumia elimu kujikinga na kujieleza.
Maisha ni safari	Kutoka eneo moja kwenda lingine	Kuna mambo mengi ambayo mja hupitia wakati anapoishi, maisha huwa na panda shuka tele.
Dunia ni watu	Viumbe hai walio na uwezo wa kuongea	Kuishi kwa kufaana, uhusiano mwema, n.k.

Aina hizi za sitiari zinahusika na uhamishaji wa maana kutoka vitu halisi kwenda dhahania na kinyume chake. Sitiari katika jedwali 4 zikifasiriwa moja kwa moja huzua utata katika ufasiri wa maana zake. Msomaji ili azielewe, inabidi atafute maana zake nje ya mipaka ya kawaida ya kisemantiki. Hali hii

inaingiliana na mhimili wa nadharia ya Semantiki Tambuzi unasisitiza kuwa lugha inahusisha ujenzi wa picha za mawazo na mipaka ya kidhana katika mawanda ya kiutambuzi. Msomaji wa sitiari ili aelewe maana zake huwa anavuta fikra na hili humfanya msomaji au msilizaji kuona ulinganisho uliopo baina ya mada na kifasiriwa (Fishelov, 2007). Mathalani, ‘ujana ni moshi,’ mpokeaji ujumbe hufananisha *ujana* (mada) na *moshi* (kibebeo) ili kupata maana inayokusudiwa. Leksimu *moshi, pori, ngao, safari, watu, mlima* na *ujanja* katika sitiari hizi, huwa hazina maana mahsusi zinapofasiriwa na msomaji au msikilizaji kama inavyojitokeza katika Jedwali 4.

Hali hii ya leksimu hizi kuwa na maana za ziada hutokana na taswira ya msomaji au mpokeaji ujumbe katika mchakato wa ufasiri wa maana za sitiari hizi. Wazungumzaji wanapokumbana na dhana mpya huchota maarifa kutoka kwa ‘ghala la maarifa’ ambayo yamefichamwa kwenye utambuzi wao na kuwasaidia kukabili ulimwengu mpya. Uwezo wa kutumia taswira hautokani na kaida za sarufi, bali hujikita katika utambuzi wa mpokeaji na msomaji ujumbe (Lakoff na Johnson, 1980 & Gichuru, 2020).

Sitiari ‘kamusi ni pori’ huwa haina maana mahsusi kwa kuwa fasiri za maana zake hutofautiana kutoka mtu mmoja hadi mwingine. Hapa tunaweza kupata maana kama vile kamusi kuwa na mambo mengi, binadamu hawezi kuitalii kamusi sawia na pori akaimaliza. Pia, sitiari ‘ujanja ni mali’ nomino *ujanja* limetumiwa kuashiria njia za mkato. Maana hii hutegemea taswira ya mpokeaji ujumbe. Sitiari kuwa na fasiri zaidi ya moja ni kile Leech (1981) anachoeleza kuwa pragmatiki ya sitiari ni aina moja ya upanuaji wa maana. Maana iliyowasilishwa huwa tofauti na maana leksika ya neno.

4.4 Mukadha wa Matumizi ya Sitiari

Kutokana na uchanganuzi wa data katika uchunguzi huu, sitiari ambazo zilidhihirisha maana zake kutegemea mukadha wa matumizi yake ni kama zifuatazo katika Jedwali 5.

Jedwali 5: Sitiari Zinazotegemea Miktadha ya Matumizi ya Sitiari

Sitiari	Muktadha wa Kifasihi	Muktadha wa Kiisimu
---------	----------------------	---------------------

Pendo tamu	Penzi la dhati	Uwepo wa pesa, zawadi za kupokezwa na kutalii mbugani.
Sauti nyororo	Sauti ya kupendeza	Ukwasi wa lugha, lugha yenye mnato na kulegeza ulimi.
Piga miguu	Kutembea	Ufukara, kukosa chombo cha kusafiri na kufanya mazoezi.
Tonesha kidonda	Kuharibu jambo	Kuzua rabsha, kuongeza uchungu kwa kitu kilicho chungu na kadhalika.
Moyo mweusi	Mtu hatari	Kutokuwa na utu, fisadi, katili na mbinafsi.

Sitiari katika Jedwali 5 zinadhihirisha sifa ya uhamishaji wa maana wa milango ya fahamu. Sitiari hizi huzua utata katika ufasiri wa maana, hasa vibeeo kama vile *tamu*, *nyororo* na *miguu* vinapotumiwa kufasiri maana za mada; *pendo*, *sauti* na *piga*. Mara nyingi leksimu za kibebeo katika sitiari za aina hizi huwa zinafasiriwa na msomaji na msikilizaji wa ujumbe kwa kuzingatia miktadha ya matumizi yake. Maoni ambayo yanashadidiwa na Jeffers na Lehiste (1979) wanaoeleza kuwa maana ya neno hutambuliwa kutokana na seti ya miktadha ambayo neno hilo hutokea.

Kulingana na data ya mahojiano huru, mtafiti alibaini sitiari katika jedwali 5 zilipofasiriwa katika muktadha wa kifasihi zilizua maana mahususi, yaani sitiari ‘pendo tamu’ huashiria penzi la dhati, ‘sauti nyororo’ humaanisha sauti ya kupendeza, ‘piga miguu’ huashiria kutembea, ‘tonesha kidonda’ humaanisha kuharibu jambo na ‘moyo mweusi’ huashiria kuwa mtu hatari. Sitiari hizi zilipofasiriwa na wahojiwa kwa kugegemea muktadha wa kiisimu maana za ziada zilizuka. Kwa mfano, sitiari ‘pendo tamu’ ilifasiriwa kuwa; uwepo wa pesa, zawadi za kupokezwa, kutalii mbugani na kadhalika. ‘Sauti nyororo’ ilifasiriwa kuwa ukwasi wa lugha, lugha yenye mnato na kulegeza ulimi. Kwa upande wa sitiari ‘kupiga miguu’ wahojiwa waliifasiri kuwa, ufukara, kukosa chombo cha kusafiri na kufanya mazoezi.

Pia, hali hii hutokea katika sitiari ‘moyo mweusi’ na ‘tonesha kidonda’ ambapo maana za vibeeo *mweusi* na *kidonda* hutegemea dhana ambayo huja akili ya msikilizaji na msomaji anaposikia au kusoma maneno haya. Kinachotokea

katika sitiari za aina hizi ni kuwa maana za sitiari hufasiriwa kwa kuzingatia uelewa wa msemaji na msikilizaji wa kufasiri yanayosemwa katika muktadha fulani. Maana ya sitiari hufasiriwa kutokana na muktadha wa matumizi yake (Akinyi na wenzake, 2017). Ufasiri wa maana ya sitiari ni tata kwa kuwa maana huwa na muundo wa kiensaiklopedia, yaani anayejua maana kuu ya leksia hujua maana nyingine zinazoambatishwa na leksia hiyo.

4.5 Elimu ya Msikilizaji na Msomaji Ujumbe

Kutokana na uchanganuzi wa data ya mahojiano huru, mtafiti alibaini sitiari 14 ambazo zilidokeza ufasiri wa maana zake kutegemea elimu ya mpokeaji ujumbe. Ili kuepuka urudiaji, mtafiti aliteua sitiari tano kuelezea jinsi elimu ya msikilizaji na msomaji ujumbe inavyozua utata wa matumizi ya sitiari za Kiswahili katika jedwali 6.

Jedwali 6: Sitiari Zinazotegemea Elimu ya Msikilizaji na Msomaji Ujumbe

Sitiari	Maana ya ziada Kulingana na Elimu ya Msikilizaji na Msomaji Ujumbe
Nywele za Ayubu ni kichaka	Kuwa na nywele nyingi kichwaji, kutochana nywele na kufuga nywele.
Rehema ni mtoto wa watu	Rehema kuwa mtoto aliyezaliwa na wazazi wakwasi, Rehema ana utu na Rehema anajua kutangamana na watu.
Kuuza upepo kwa dunia	Kutia kiwi, kupaka mafuta kwa tako au kwa mgongo wa chupa, kumpatia mtu ulimi wa kulazia na kupiga mafamba.
Kelele nyingi ni makeke	Machachari, usumbufu na kupayuka.
Piga moyo konde	Kutoacha, kujipa moyo, kujiliwaza na kujituliza.

Sitiari zilizoordheshwa katika jedwali 6 ni sitiari funge. Sitiari funge fasiri zake hupatikana katika kiwango cha kirai, kishazi na sentensi (Gaichu, 2016). Uchanganuzi wa data ya mahojiano huru wa sentensi za sitiari katika jedwali 6 ulidhihirisha utata katika ufasiri wa maana zake, kwa kuwa, virai vinavyounga sentensi za sitiari hizi huwa na maana za ziada. Mtafiti alibaini kuwa msikilizaji na mpokeaji wa sitiari hizi anastahili kuelewa maana ya msingi ya leksimu kabla ya kung'amua maana ya kitamathali inayokusudiwa katika sitiari

inayohusika. Makala hii ilitumia sitiari *Rehema ni mtoto wa watu* kutoka jedwali 6 kama kiwakilishi kueleza namna utata huzuka katika ufasiri wa maana za sitiari hizi.

Mtafiti alitambua kuwa, sitiari *Rehema ni mtoto wa watu* ilifasiriwa kuwa mtoto aliyezaliwa na binadamu, maana ambayo ni ya kimsingi. Hata hivyo, ni kiwango cha elimu ambacho husababisha utata kutokea wakati ambapo maana za ziada hutolewa kwani wahojiwa walioshiriki katika uchunguzi huu walidhihirisha uwepo wa ufasiri wa ziada wa maana za sitiari husika. Wahojiwa wa Shahada ya Kwanza, Shahada ya Uzamili na Shahada ya Uzamifu, mtafiti alitambua kuwa, sitiari *Rehema ni mtoto wa watu* ilipofasiriwa na wahojiwa wote walizua maana ya ziada iliyoingiliana, yaani Rehema kuwa mtoto aliyezaliwa wazazi wakwasi. Maana zaidi zilitolewa na wahojiwa wa Shahada ya Uzamili na Uzamifu, waliifasiri kuwa *Rehema ni mtoto wa watu* kuwa ana utu na anajua kutangamana na watu.

Sitiari zote katika kundi hili zinadhihirisha utata katika ufasiri wa maana, kwa kuwa ufasiri wa maana upo akilini mwa msikilizaji na msomaji wa sitiari inayohusika. Fasiri za maana hutegemea kiwango cha elimu ya mpokeaji ujumbe huwa nacho na kiwango hiki hubaini misamiati ambayo mpokeaji ujumbe ametangamana nayo katika usomi wake. Maoni haya yanaingiliana na mhimili wa nadharia ya Semantiki Tambuzi unaodai kuwa maana imejikita katika maumbile ya binadamu yakiwa msingi wa kufasiri dhana ya ulimwengu. Maana huumbika kutokana na tajriba za watu zinazohusiana na umbile la binadamu.

5.0 Hitimisho

Makala hii imeeleza kwa uwazi kuwa utata katika ufasiri wa maana za sitiari husababishwa na mazingira ya mpokeaji ujumbe, maarifa na tajriba ya mpokeaji ujumbe na taswira anayopata mpokeaji ujumbe. Pia, husababishwa na miktadha ya matumizi ya sitiari na elimu ya msikilizaji na msomaji ujumbe. Kutokana na sababu hizi, makala hii yalibaini kuwa maana za sitiari ni dhana za kiutambuzi. Ufasiri wake haujifungi katika maana moja, bali hutofautiana kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine. Pia, yametambua kuwa tamathali za semi zinaweza kutafitiwa katika isimu, tofauti na ilivyo zoeleka kuwa aina hii ya mbinu ya lugha hutafitiwa katika fasihi pekee. Kuna haja ya tafiti zaidi kufanywa

kuangalia namna maana zinavyofasiriwa katika vipashio vingine vya lugha kama vile polisemi na metonimu kwa kuongozwa na nadharia nyngine za isimu ili kuzua maarifa zaidi.

Marejeleo

Akinyi, M. F., Amukowa, D. N., Owala, S., & Jagero, J. (2017). Application of the Conceptual Metaphor Theory in the Analysis of Word Metaphors: A Case of Wamitilas Plays. *Saudi J. Humanities Soc. Sci.*; Vol-2, Iss - 10A (Oct, 2017):871 - 877.

Fishelov, D. (2007). Simile Understanding and Semantic Categories, *JLS*, 36:71-78. Gaichu, M. N. (2016). *Uchunguzi wa Sitiari Dhanifu katika Methali za Kiswahili- Mtazamo wa Nadharia ya Uhusiano*. Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.

Geeraerts, D. (2006). *Cognitive Linguistics: Basic Readings*. New York: Mouton deGruyter.

Geeraerts, D., & Kristiansen G. (2012). *Cognitive Linguistics and Language Variation*. Jeannette Little & John Taylor.

Gichuru, M. T. (2020). *Mabadiliko ya Maana za Leksia za Kiswahili: Mtazamo Linganishi wa Kikale na Kisasa*. Tasinifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Jeffers, G., R., & Lehiste, I. (1979). *Principles and Methods for Historical Linguistics*. Cambridge: MIT Press.

Kitundu, G. J., & Malangwa, P. S. (2020). Ujenzi wa Maana katika Sitiari na Tashibiha za Kiswahili. *Kioo cha Lugha*, 17(1).

Lakoff, G. (1987). *Women, Fire and Dangerous Things*. Chicago: University of Chicago Press.

Lakoff, G., & Johnson, M. (1980). *Metaphor We Live By*. Chicago: Chicago University Press.

Leech, G. N. (1981). *Semantics*. Harlow: Penguin.

Lemmens, M. (2017). 'Cognitive Semantics' in *Routledge Handbook of Semantics*. Editor Nick Riemer. London and New York: Routledge.

- Löbner, S. (2013). *Understanding Semantics*. New York: Routledge.
- Mbatiah, M. (2001). *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Standard Textbooks, Graphics and Publishing.
- Milroy, A. L. (1987). *Observing and Analysing Natural Languages*. Oxford: Basil Blackwell Ltd.
- Muna, E. O. (2017). *Vitendo Sogezi katika Kiswahili Sanifu*. Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Mwakio, L. W. (2016). *Matumizi ya Tashbiha, Sitiari na Taashira katika Damu Nyekusi na Hadithi Nyingine*. Tansifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Mwita, L. M., & Malangwa, P. S. (2019). *Semantiki*. Nairobi: Longhorn Publishers PLC.
- Onish, K. H., & Murphy, G. L. (1993). Metaphoric Reference: When Metaphors are Not Understood as Easily as Literal Expressions. *Memory & Cognition*, 21(6), 763-772.
- Sapir, E. (1912). Language and Environment. *American Anthropologist*, 14(2), 226-242.
- Ullmann, S. (1967). *Semantics: An Introduction to the Science of Meaning*. London: Oxford Basil Blackwell.
- Vyvyan, E. (2006). Lexical Concepts, Cognitive Models and Meaning-Construction. 17(4), 491 - 534.

Utelezi wa Uainishaji wa baadhi ya Maneno ya Kiswahili: Kigezo cha Kimofosintaksia

Elishafati J. Ndumiwe

Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agustino, Tanzania

ndumiweelisha@gmail.com

Ikisiri

Makala hii imechunguza utelezi wa uainishaji wa baadhi ya maneno ya Kiswahili kwa kurejelea kigezo cha kimofosintaksia. Data za msingi za makala hii zimekusanywa kwa kutumia mbinu ya upitiaji nyaraka. Nyaraka zilizochunguzwa ni *Kivuli Kinaishi* na magazeti ya Ijumaa na Mwananchi. Mbinu ya uteuzi lengwa ilitumika kupata tamthiliya na magazeti yaliyolengwa. Katika uchanganuzi wa data tumetumia msingi wa taarifa za kileksika na za kiuamilifu pamoja na msingi wa muundo wa vishiriki vya kitenzi wa nadharia ya Sarufi Leksia Amilifu. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa baadhi ya maneno yanabadilika kutoka aina moja kwenda nyingine. Kwa mfano, vivumishi, vielezi vya wakati na vya mahali vinaweza kuwa nomino. Kiwakilishi kinaweza kuwa kibainishi na kitenzi-jina kinaweza kuwa kitenzi au nomino. Pia, kihusishi kinaweza kuwa kiunganishi. Makala hii inapendekeza kuwa, kigezo cha kimofosintaksia kinaweza kuwa suluhisho la uainishaji wa aina za maneno katika Kiswahili kuliko vigezo vya kimofolojia na kisemantiki.

Istilahi za Msingi: Uainishaji wa maneno, kimofosintaksia, sarufi leksia amilifu, utelezi na mwarobaini.

1.0 Utangulizi

Neno ‘utelezi’ limetokana na kitenzi ‘teleza’ linalomaanisha kuserereka kutoka sehemu moja kwenda nyingine (TUKI, 2013). Katika makala hii neno utelezi limetumika kurejelea hali ya neno kutokea katika kategoria zaidi ya moja. Kimsingi, yapo maneno ya Kiswahili yanayotokea katika kategoria zaidi moja. Basha (1996:1) anatoa mfano ufuatao:

MAKALA HALISI

HISTORIA YA

MAKALA

Kupokelewa: 07 Machi

2022

Kurekebishwa: 13 Julai

2022

Kukubaliwa: 29 Julai

2022

Kuchapishwa: 20

Septemba 2022

ISSN: 2799 – 2187

Juzuu 1,

Toleo 1,

uk.92 – 104.

NUKUU

Ndumiwe, E. J. (2022). Utelezi wa Uainishaji wa Baadhi ya Maneno ya Kiswahili: Kigezo cha Kimofosintaksia. *Jarida la Fahari ya Kiswahili*, 1(1), 92 – 104.

1. (a) Watoto wanacheza na **kuimba**.
- (b) **Kuimba** kwao kumewafurahisha watu wengi.

Linganisha:

2. (a) Watoto wanacheza na **wanaimba**.
- (b) **Chakula** chao kimewashibisha watu wengi.

Wanafunzi wengi wa sarufi hupata ugumu wa kuainisha aina ya neno “kuimba” katika sentensi 1 (a) na (b) kwa sababu yapo maelezo ya kinadharia yanayoeleza kuwa kiambishi {ku-} kinapopachikwa mwanzoni mwa kitenzi hubadili kitenzi kuwa nomino (Ndumiwe, 2020). Pia, yapo maelezo ya kinadharia yanayoeleza kuwa neno linapotokea mwanzoni mwa sentensi huwa ni nomino au kiwakilishi. Pia, Stom (2015) ameonisha kuwa yapo maneno ya Kiswahili yanayoainishwa kutegemeana na mazingira yake katika sentensi. Kwa mfano, maneno ‘hodari’ na ‘nyumbani’ huweza kuwa kivumishi, nomino, kielezi au nomino kama ilivyo katika mifano hii:

3. (a) Mwanafunzi **hodari** ni mwepesi wa kuelewa.
- (b) Hamisa ni **hodari** wa kucheza ngoma.
4. (a) Wageni walifika **nyumbani** mapema.
- (b) **Nyumbani** kwetu kuna mti mrefu.

Wanasarufi hupata ugumu wa kuainisha maneno yaliyokolezwa katika tungo 3 (a) na (b) na 4 (a) na (b). Katika mifano hiyo, neno *hodari* katika sentensi 3 (a) ni kivumishi, ilhali katika sentensi 3 (b) ni nomino. Pia, neno *nyumbani* katika sentensi 4 (a) ni kielezi, ilhali katika sentensi 4 (b) ni nomino. Ugumu huo umetokana na maelezo ya kinadharia yanayoeleza kuwa neno linalotokea baada ya nomino au kiwakilishi hufanya kazi ya kutoa sifa kuhusu nomino. Neno linalotokea baada ya kitenzi kishirikishi huwa ni nomino; na linalotokea baada ya kitenzi kikuu huwa ni kielezi (Matinde, 2012). Uainishaji wa neno kwa kuzingatia dhana ya neno hilo hautoshi kusema kwa uhakika kuwa ni aina hii ya neno.

Wanaisimu wa lugha ya Kiswahili wanatofautiana kuhusu idadi ya aina za maneno katika lugha ya Kiswahili. Katika utofauti huo, yapo makundi manne yanayoonesha idadi tofautitofauti ya maneno ya Kiswahili. Kundi la kwanza, linaeleza kwamba, zipo aina saba za maneno ambazo ni nomino, kitenzi,

kivumishi, kiingizi, kiwakilishi, kielezi na kiunganishi au kihusishi (Nkwera, 1978; Kapinga, 1983 na Mohamed, 1986). Kundi hili linabainisha kiunganishi na kihusishi kama aina moja ya neno. Jambo hilo siyo sahihi kwa sababu kiunganishi na kihusishi ni maneno ambayo hayana uhusiano kabisa wa kiumbo na kidhima katika tungo.

Kundi la pili linaeleza kuwa kuna aina nane za maneno ambazo ni nomino, kitenzi, kivumishi, kiwakilishi, kielezi, kiunganishi, kihusishi, na kiingizi (Mdee, 1988; Msokile, 1992; Mgullu, 1999; Mbaabu, 2000; Rubanza, 2003; Matinde, 2012). Kundi hili limetofautisha kihusishi na kiunganishi kwa kuonesha kuwa hizi ni aina mbili za maneno zinazotofautiana kama ilivyofafanuliwa katika mifano ifuatayo:

5. (a) Kazi hiyo imefanywa **na** mfanyakazi hodari.
- (b) Zawadi ni mfupi **kama** mama yake.
- (c) Jane hajarudia tendo hilo **tangu** aonywe na wazazi wake.
- (d) Wageni walioalikwa **na** wasioalikwa walihudhuria hafla hiyo (**Chanzo**: Matei, 2008).

Tukirejea mfano 5 (a) - (c) maneno yaliyokolezwa ni vihusishi kwa sababu yanaonesha uhusiano wa nomino na vipashio vingine katika sentensi. Mfano 5 (d) neno lililokolezwa ni kiunganishi kwa sababu huunganisha vipashio viwili vyenye hadhi sawa. Hivyo, kihusishi ni kategoria inayojitegemea tofauti na wanamapokeo walioianisha kama kiunganishi.

Kundi la tatu linaeleza kwamba kuna aina tisa za maneno ambazo ni nomino, kitenzi, kielezi, kivumishi, kibainishi, kiunganishi, kihusishi, kihisishi na kiwakilishi (Philipo, 2012; Wesana-Chomi, 2013). Kundi hili limeonesha kuwa kibainishi ni aina ya neno linalojitegemea tofauti na watangulizi wao waliochukulia kuwa kibainishi ni aina mojawapo ya kivumishi au kiwakilishi. Kwa mfano:

6. (a) **Yule** ni mwanangu.
- (b) Wanafunzi **wawili** warefu wamefika.
- (c) Kijana **hodari** ni mcheshi.
- (d) Mtoto **yule** ni mwanangu (**Chanzo**: Philipo, 2012).

Tukirejea mfano wa 6 (a), neno lililokolezwa ni kiwakilishi kwa sababu husimama badala ya nomino. Katika mfano 6 (b) neno *wawili* ni kibainishi cha namba kwa sababu linapambanua idadi ya wanafunzi. Pia, katika 6 (d) neno *yule* ni kibainishi kwa sababu huonesha umbali wa mtoto anayerejelewa. Katika 6 (c) neno *hodari* ni kivumishi kwa sababu inaonesha sifa ya kijana anayehusika. Kwa hiyo, kibainishi ni aina inayojitegemea tofauti na wanamapokeo wanaoianisha kama kiwakilishi au kivumishi.

Kundi la mwisho, wanaeleza kwamba, kuna aina kumi za maneno katika lugha ya Kiswahili ambazo ni nomino, kitenzi, kivumishi, kiwakilishi, kielezi, kiunganishi, kihusishi, kihisishi, kionyeshi na kibainishi (Habwe na Karanja, 2004). Hata hivyo, kundi hili limeonesha kioneshi na kibainishi kuwa ni kategoria mbili tofauti. Jambo hilo si sahihi kwa sababu kioneshi ni aina mojawapo ya kibainishi. Kwa hiyo, madai haya yanatufanya tuone kuwa ni aina tisa wala siyo kumi.

Utofauti wa uainishaji wa maneno ya Kiswahili unasababishwa na mambo kadhaa. Kwanza, vigezo vya uainishaji vinavyotumika. Kwa mfano, wanapooanisha aina 7 hutumia kigezo cha kimofolojia bila kuliweka katika muktadha wa tungo. Pia, wanaoanisha aina 8 wanatumia kigezo cha kisintaksia kwa kuangalia muundo wa tungo. Wanaoanisha aina 9 na 10 wanatumia kigezo cha kimofosintaksia. Pili, mkabala wa kisarufi unaotumika wakati wa uainishaji. Wanasarufi mapokeo huainisha aina 7. Wanamuundo huainisha aina 8 na wanasarufi zalishi huainisha aina 9 na 10. Wanamapokeo walifungwa na kanuni elekezi tofauti na wanasarufi zalishi wanaoshughulikia lugha kama inavyotumiwa na jamii.

Makala hii inatambua kategoria 9 za kileksika katika lugha ya Kiswahili. Kategoria hizo ni nomino, kitenzi, kielezi, kivumishi, kibainishi, kiunganishi, kihusishi, kihisishi na kiwakilishi. Uwekaji wa maneno katika kategoria fulani si jambo jepesi kwa kuwa kuna baadhi ya maneno huwa katika kategoria zaidi ya moja. Kwa mfano, ‘meza’ ni kitenzi pia ni nomino, ‘tupa’ ni kitenzi pia ni nomino, ‘wake’ ni nomino pia ni kibainishi. Kwa hiyo, mifano hiyo inathibitisha kuwa uainishaji wa maneno siyo jambo jepesi kwani yanajidhihirisha katika kategoria tofautitofauti licha ya kuwa na mofolojia inayofanana. Makala hii imeshughulikia aina za maneno ambazo zinatokea

katika aina zaidi ya moja. Aina hizo ni nomino, vivumishi, vibainishi, vihusishi na vielezi.

2.0 Mbinu za Utafiti na Nadharia

Makala hii imechunguza utelezi wa uainishaji wa baadhi ya maneno ya Kiswahili kwa kurejelea kigezo cha kimofosintaksia. Data za msingi za makala hii zimekusanywa kwa kutumia mbinu ya upitiaji nyaraka. Nyaraka zilizochunguzwa ni tamthiliya ya *Kivuli Kinaishi* (Mohamed, 1990) na magazeti ya *Ijumaa* (2020, Julai 31-Agosti 6), *Ijumaa* (2020, Agosti 24 - 30) na *Mwananchi* (2020, Agosti 5). Mbinu ya uteuzi lengwa ilitumika kupata tamthiliya na magazeti yaliyolengwa. Uchambuzi wa data umeongozwa na Nadharia ya Sarufi Leksia Amilifu ya Bresnan na Kaplan (1982). Nadharia hii ilipendekezwa kwa ajili ya kuchambua data za lugha kwa kutumia taarifa za kiuamilifu na za kileksika za viambajengo vya tungo. Msingi wa taarifa za kileksika na za kiuamilifu pamoja na msingi wa muundo wa vishiriki vya kitenzi umetusaidia kubainisha na kufafanua aina za maneno pindi zinapotokea katika sentensi. Nadharia imetumika kupambanua aina za maneno kwa kuzingatia muundo wa sentensi, taarifa za kileksika na za kiuamilifu za maneno linalohusika katika sentensi.

3.0 Matokeo ya Utafiti

Sentensi za Kiswahili huundwa na aina mbalimbali za maneno. Kuna aina tisa za maneno ya Kiswahili kama tulivyoona hapo awali. Aina hizo ni nomino, kitenzi, kielezi, kivumishi, kibainishi, kiunganishi, kihusishi, kihisishi na kiwakilishi. Baadhi ya maneno ya Kiswahili huingia katika aina zaidi ya moja pindi yanapojitokeza katika sentensi za Kiswahili. Utafiti huu unaonesha kuwa neno moja linaweza kuwa la aina fulani, lakini katika mazingira mengine likawa la aina nyingine. Kivumishi kinaweza kuwa nomino, kielezi kinaweza kuwa nomino, na kiwakilishi kinaweza kuwa kibainishi. Katika sehemu hii tumefafanua utokeaji wa aina hizo katika sentensi za Kiswahili.

3.1 Utelezi wa Kielezi Kuwa Nomino

Kielezi ni neno lenye uamilifu wa kuonesha jinsi kitenzi, kivumishi au kielezi kingine kilivyotokea au kilivyo (Kihore na wenzake, 2012). Kuna aina mbalimbali za vielezi katika lugha ya Kiswahili. Kwa mfano, vielezi vya mahali, namna na wakati (Wesana-Chomi, 2017). Baadhi ya wanaisimu wa

lugha ya Kiswahili wanaeleza kuwa nomino za kawaida zinapoongezewa kiambishi {ni} mwishoni huwa ni kielezi cha mahali. Vielezi hivyo vinaonesha mahali tendo lilipofanyikia, linapofanyika au litakapofanyikia. Hata hivyo, si wakati wote kwa sababu lugha ya Kiswahili ina mpangilio wa vipashio wa Kiima-Kitenzi-Yambwa (Vitale, 1981 & Mwamzandi, 2014). Kiambajengo kinachotokea mwanzoni mwa sentensi za Kiswahili mara nyingi ni nomino au kiwakilishi chake (Ndung'u, 2015). Kwa mfano:

7. (a) Baba na mama wanaenda **nyumbani**.
(b) Jana tulienda **mnadani** kwa basi la shule.
(c) Watoto wetu wamekwenda **sokoni**.
8. (a) **Nyumbani** kwetu kuna basi la zamani.
(b) **Mnadani** kuna bidhaa za bei ndogo.
(c) **Sokoni** pamebomolewa jana asubuhi.

Tukichunguza mfano 7 (a) - (c) kategoria zilizokolezwa zimejitokeza kama vielezi vya mahali kwa sababu zinatoa taarifa zaidi kuhusu mahali tendo lilipofanyika, linapofanyika au litakapofanyika. Hata hivyo, kategoria hizo hizo zimejitokeza kama nomino katika mfano wa 8 (a)–(c) kutokana na kutokea mwanzoni mwa sentensi.

Baadhi ya vielezi vya wakati hubadilika na kuwa nomino pindi vinapojitokeza mwanzoni mwa sentensi za lugha ya Kiswahili. Vielezi vya wakati hueleza wakati ambao tendo lilifanyika, linafanyika au litafanyika. Hata hivyo, si katika mazingira yote vielezi hivi hubaki kuwa vielezi. Yapo mazingira mengine ya kuwepo katika sentensi za Kiswahili hubadilika kuwa nomino. Kwa mfano:

9. (a) Watazamaji wengi watakuja **kesho**.
(b) Mvua ya mawe ilinyesha **asubuhi** kabla Mtolewa hajaingia Giningi.
(c) Mchezaji wetu aliwasili **janajioni** na kupokelewa na mashabiki wengi.
10. (a) **Kesho** ni siku ya utambulisho wa wasanii wapya WCB.
(b) **Usiku** wa leo Arsenal na Chelsea zitapambana katika mchezo wa fainali.
(c) **Leo** pana shughuli mbili ndani ya moja
(**Chanzo:** *Ijuma*, 2020, Julai 31-Agosti 6) na *Mohamed* (1990).

Tukichunguza tungo 9 (a) - (c) aina za maneno zilizokolezwa zimejitokeza kama vielezi vya wakati kwa sababu zinatoa taarifa kuhusu wakati tendo lilipofanyika au litakapofanyika. Hata hivyo, aina za maneno zilizokolezwa katika 10 (a) - (c) zimejitokeza kama nomino kutokana na kutokea kwake mwanzoni mwa sentensi za Kiswahili. Aidha, ukiigawa sentensi ya 10 (a) katika KN na KT, KN itakuwa ni *kesho* na KT itaanzia katika *ni siku ya utambulisho wa wasanii wapya WCB*.

3.2 Utelezi wa Kivumishi na Nomino

Kivumishi ni neno linalotoa taarifa zaidi kuhusu nomino au kiwakilishi cha nomino (Massamba, 2016). Kihore na wenzake (2012) wanaeleza kuwa taarifa hizo zinahusu namna nomino hiyo inavyoonekana au inavyofikiriwa. Hata hivyo, fasili ya Massamba (2016) ina dosari kidogo kwa sababu kivumishi huweza pia kutoa taarifa zaidi kuhusu kiwakilishi. Kivumishi ni neno au maneno yanayotoa taarifa zaidi kuhusu nomino au kiwakilishi. Kuna mkanganyiko unaojitokeza miongoni mwa wanaisimu wa lugha kuhusu aina za vivumishi kutokana na mtazamo wa kuwepo kwa kategoria ya kibainishi ulioibuka hivi karibuni (Philipo, 2012). Msimamo wa makala hii ni kuwa kuna aina moja tu ya kivumishi cha sifa. Maelezo haya yana maana kuwa vivumishi vyote hutoa sifa za nomino. Vivumishi hivi mara nyingi hutokea mbele ya nomino na huwa na kiambishi kipatanishi cha ngeli kinachotokana na ngeli husika ya nomino. Hata hivyo, katika mazingira mengine vivumishi hivi hubadilika kuwa nomino kutokana na kujitokeza kwake katika sentensi. Kwa mfano:

11. (a) Msani **mzuri** husaidia wasiojiweza.
(b) Mchezaji **hodari** amesajiliwa Simba.
(c) Mti **mrefu** umeanguka uwanjani.
12. (a) Hamisa Mabeto ni **mzuri** wa sura.
(b) Diamond ni **hodari** wa kuimba nyimbo za mapenzi.
(c) Kipusa huyo alionekana **mrembo** wa kuvutia.

Tukichunguza mfano wa 11 (a) - (c) aina za maneno zilizokolezwa zimejitokeza kama vivumishi vya sifa kwa sababu vinajitokeza baada ya nomino kueleza sifa za nomino hiyo. Hata hivyo, katika mfano 12 (a) - (c) aina za maneno zilizokolezwa haziwezi kuwa vivumishi kwa sababu zimetokea baada ya

nomino. Pia, haziwezi kuwa vielezi kwa sababu kielezi hakiwezi kutokea mbele ya kitenzi kishirikishi. Kitenzi kishirikishi hufuatwa na nomino wala siyo kivumishi. Kategoria hizo husimama kama nomino zinapotokea katika mazingira hayo. Kwa hiyo, nomino zingine zinaweza kukaa katika nafasi hizo.

3.3 Uainishaji wa Kitenzi-jina

Kitenzi-jina ni nomino zinatotokana na kitenzi ambazo huambikwa kiambishi {ku-} mwanzoni (Matinde, 2012). Vitenzi shina (mzizi+kiambishi tamati maana) ndivyo mara nyingi huwa na sifa ya kuambikwa kiambishi {ku-} na kupata sifa ya kuwa nomino. Vitenzi-jina ni nomino kwani katika uaininishaji wa ngeli kimofolojia nomino hizi huwekwa katika ngeli ya 15 (Ku) (Philipo, 2012). Matinde (2012) anatoa ukomo wa nomino hizo kuwa zinaendelea kuwa nomino pindi tu zinapojitokeza mwanzoni mwa sentensi. Kitenzi-jina hakiwezi kuwa nomino kinapojitokeza kwenye kirai kitenzi cha sentensi inayohusika. Pia, mawazo ya namna hiyo yanajitokeza kwa Kihore na wenzake (2012) katika mifano ya vitenzi visaidizi ifuatao:

13. (a) **alikuwa** analala.
 - (b) **tunapenda** kula.
 - (c) **alikuwa anataka** kunisalimu.
- (Chanzo: Kihore na wenzake, 2012).

Katika mfano 13 (a) - (c) maneno yaliyokolezwa ni vitenzi visaidizi na hufuatiwa na vitenzi vikuu. Kuna utata unajitokeza katika 13 (b) na (c) kwa sababu vitenzi visaidizi vinaweza kufutwa katika sentensi na maana lengwa-ikaendelea kuwepo. Mfano 13 (a) tunaweza kusema *mtoto analala* badala ya *mtoto alikuwa analala*. Pia, 13 (b) tukiondoa neno *tunapenda* ikabaki *kula* maana lengwa inapotea. Mfano wa 13 (b) tukisema *sisi tunapenda kula* inaleta maana, lakini tukisema *sisi kula* haileti maana. Nafasi ya utokeaji wa vitenzi-jina katika mfano 13 (b) na (c) kunaweza kutokea nomino yoyote ile. Katika 13 (b) tunaweza kusema *tunapenda nyimbo* na ikaleta maana. Pia, mfano 13 (c) tunaweza kusema *alikuwa anataka simu* na ikaleta maana. Makala hii imebaini kuwa kitenzi-jina huendelea kuwa nomino hata pale kinapojitokeza katika kirai kitenzi cha sentensi. Kwa mfano:

14. (a) **Kuenea** kwa ugonjwa huo kumethibitiwa nchini.
(b) **Kujifunza** teknolojia mpya ni chachu ya kuongeza tija kwa wahitimu wetu.
(c) **Kupatiakana** kwa mafuta hayo ndiyo ajenda mhimu katika kikao hiki.

15. (a) Chama kimewezak**usimama** imara.
(b) Wahitimu wawe wepesi wa **kutafuta** ajira nje ya nchi.
(c) Sisi tunaomba **kupita**.
(**Chanzo:** *Ijumaa* 2020, Agosti 24 – 30 na *Mwananchi*2020, Agosti 5).

Tukirejea mfano wa 14 (a)–(c) maneno yaliyokolezwa ni vitenzi-jina na hubainishwa kama nomino kwa sababu hutokea mwanzoni. Vitenzi-jina hivyo huendelea kujitokeza kama nomino katika 15 (a)–(c) kwa sababu ya uamilifu wake na mfuatano wa kategoria zingine katika sentensi. Katika 13 (a) nafasi hiyo inaweza kukalikwa na nomino nyingine. Katika 15 (c) hatuwezi kuwa na vitenzi vikuu viwili vinavyofuatana. Kimpangilio, kitenzi kisadizi hufuatiwa na kitenzi kikuu na kitenzi kikuu hakiwezi kuondolewa bila kuathiri maana. Kwa mfano, katika 15 (c) neno *tunaomba* haliwezi kuondolewa bila kuathiri maana. Pia, kitenzi kikuu hakiwezi kutokea pamoja na kitenzi kishirikishi. Kwa mfano, katika 15 (b) neno *kutafuta* haliwezi kuwa kitenzi kwa sababu katika kirai kitenzi kimoja kitenzi kikuu hakiwezi kutokea pamoja na kitenzi kishirikishi.

3.4 Uainishaji wa Kihusishi

Kihusishi ni kategoria yenye uamilifu wa kuonyesha uhusano wa vitu viwili au zaidi au watu wawili au zaidi katika tungo au sentensi (Matei, 2008). Kihusishi huweza kutokea kwenye kirai nomino au kirai kitenzi na mara zote huwa na muundo sahili. Tukiwa tunabainisha vihusishi vikiwa pwekepweke tunaweza kuvichanganya na kategoria ya kiunganishi. Mukadha mzuri wa ukategorishaji wa vihusishi katika lugha ya Kiswahili ni kutumia sentensi. Mifano ifuatayo inaweza kurejelewa:

16. (a) Baba **na** mama wamerudi nyumbani.
- (b) Mtoto ameondoka **na** mama yake.
- (c) Mafuta hayo yalikuwa **na** bei **ya** juu.
- (d) Kiliniki ni huduma muhimu **kwa** mtoto.
- (e) Yale mafuta yalinunuliwa **kwa** bei **ya** Dola 560 **kwa** tani.
- (f) Wezi **wa** mahindi wamevamia **katika** shamba.
- (g) Kivuli chako kinaishi **mpaka** leo.

Mfano wa 16 (a) neno *na* limejitokeza kama kiunganishi kwa sababu linaunganisha nomino na nomino kuunda kirai nomino *baba na maama*. Hata hivyo, katika mfano 16 (b) - (g) maneno yaliyokolezwa yametokea kama kihusishi kwa sababu yanaonesha uhusiano wa vitu au tendo na kitu. Kihusishi katika sentensi hubainika kiurahisi kwa kuangalia kategoria inayofuatia kihusishi hicho. Mara zote kihusishi hufuatwa na nomino licha ya kutanguliwa na nomino au kitenzi.

3.5 Uainishaji wa Kibainishi

Kirai kibainishi ni kipashio cha kimuundo ambacho kiini chake ni kubainisha ukomo wa maana ya nomino. Richards na Schmidt (2002) wanaeleza kuwa kibainishi ni neno ambalo hutumika pamoja na nomino kuonyesha ukomo wa maana ya nomino. Pia, Massamba (2016) anaeleza kuwa kibainishi ni kipashio kinachotumika kuonesha umahsusi wa nomino. Kwa hiyo, kibainishi huipambanua nomino kiumiliki, kiidadi na kimwonekano. Kibainishi katika lugha ya Kiswahili kinaweza kutokea baada au kabla ya nomino. Kwa mfano, *yule mtoto mzuri* na *mtoto yule mzuri*. Katika sentensi hizi *yule* ni kibainishi licha ya kutokea kabla ya nomino au baada ya nomino. Hata hivyo, kibainishi kikiwa pwekepweke huweza kutokea kama kiwakilishi na hata wakati mwingine kikianza katika sentensi bila kuwa na nomino huweza kuwa kiwakilishi. Kwa mfano:

17. (a) **Huu** ni uamuzi mgumu kabisa.
 - (b) **Kile** ni kisima cha Giningi.
 - (c) **Wawili** watapelekwa kwa Malkia siku ya kesho.
18. (a) **Yule** mtoto ni wangu.
 - (b) Mtoto **yule** ni wangu.
 - (c) Jibu lako linaonyesha ulijitayarisha vema
 - (d) Askari **wawili** walipita kwa Bawabu kwa hongo.

Chanzo cha data ni Mohamed (1990) na Mwananchi (2020, Agosti 5).Kategoria zilizokolezwa katika 17(a) - (c) zinajitokeza kama viwakilishi kwa sababu husimama badala ya nomino. Hata hivyo, kategoria zilizokolezwa katika 18(a) - (d) zimejitokeza kama vibainishi kwa sababu zimeandamana na nomino kuonesha umahususi wa nomino zinazorejelewa katika sentensi.

4.0 Hitimisho

Makala hii inaonesha umuhimu wa taaluma ya sintaksia na mofolojia katika uanishaji wa maneno ya Kiswahili. Hali hii ni tofauti na kigezo cha kimofolojia ambapo huangalia umbo la neno linalohusika na kuliweka neno katika aina fulani. Maneno yanayoingia katika aina fulani huwa yana maumbo yanayoelezwa kimofolojia. Kwa mfano, maneno yenye viambishi ngeli huwa ni nomino. Pia, kigezo cha kimofosintaksia kinatofautiana na kigezo cha kisemantiki ambacho huangalia dhana inayobebwa na kundi na neno. Maneno yanayodokeza tendo huitwa vitenzi. Kigezo cha kimofosintaksia huangalia namna maneno yanavyotokea katika sentensi pamoja na athari za maumbo ya maneno katika muundo wa sentensi. Uainishaji wa kategoria fulani katika sentensi mara nyingi huamuriwa na mfuatano na kategoria nyingine katika sentensi.

Marejeleo

- Besha, R. M. (1996). “Nomino za Kiswahili: Misingi ya Uainishaji”. *Kioo cha Lugha*, 2:1-14.
- Bresnan, J., & Kaplan, R. M. (1982). “Introduction: Grammars as Mental Representation of Language”. Katika, M. Bresnan (Mh.) *Mental Representation of Grammatical Relations*, 173-281. Cambridge: The MIT Press.
- Habwe, J., & Karanja, P. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- Kapinga, M. C. (1983). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: TUKI.
- Kihore, Y. M., Massamba, D. P. B., & Msanjila, Y.P. (2012). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: TUKI.
- Massamba, D. P. B. (2016). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha* (Toleo la 2).

Dar es Salaam: TUKI.

Matei, A. K. (20087). *Darubini ya Sarufi: Ufafanuzi Kamili wa Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Matinde, R. S. (2012). *Dafina ya Lugha, Isimu na Nadharia Sekondari Vyu vya Kati na Vyu Vikuu*. Mwanza: Serengeti Educational Publisher (T) Ltd.

Mbaabu, I. (2000). *Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Longorn.

Mdee, J. S. (1988). *Sarufi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Education Service Centre.

Mgullu, R. S. (1999). *Mtalaa wa Isimu*. Nairobi: Longman.

Mohamed, A. M. (1986). *Sarufi Mpya*. Nairobi: Foundation Publishers.

Mohamed, S. (1990). *Kivuli Kinaishi*. Nairobi: Oxford University Press.

Msokile, M. (1992). *Kunga za Fasihi na Lugha*. Dar es Salaam: Educational Publishers and Distributors Ltd.

Mwamzandi, M. Y. (2014). Swahili Word Order Choices: Insights from Information Structure. *Tasinifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Texas*.

Ndumiwe, E. J. (2020). *Kurunzi ya Isimu na Muundo wa Kiswahili*. Mwanza: Tridax Africa Company Limited.

Ndung'u, N. M. (2015). 'Information Structure in Kiswahili'. *International Journal of Education and Research*, 3 (3):309-320.

Nkwera, F. (1978). *Sarufi na Fasihi: Sekondari na Vyu*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

Philipo, Z. T. (2012). "Tofauti Baina ya Vivumishi na Vibainishi katika Lugha ya Kiswahili". *Kioo cha Lugha*, (13): 125-143.

Radford, A. (2004). *English Syntax: An introduction*. Cambridge: Cambridge University Press.

Richards, J. C., & Schmidt, R. (2002). *Longman Dictionary of Language Teaching and Applied Linguistics*. London: Pearson Education Limited.

Strom, E. B. (2015). The Word Order in Swahili Adnominal Constructions with Locative Demonstrative. *Nordic Journal of African Studies*, 24 (2): 118-145.

TUKI, (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.

Vitale, A. J. (1981). *Swahili Syntax*. Cinnamison: N.J. Foris Publishers.

Wesana-Chomi, E. (2013). *Kitangulizi cha Mofolojia ya Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.

Wesana-Chomi, E. (2017). *Kitangulizi cha Muundo Viambajengo wa Sentensi za Kiswahili*. Dar es Salaam: TATAKI.

Utandawazi wa Kiswahili: Kuimarika na Kulegalega kama Lugha Rasmi ya Afrika

Mohamed Omary Maguo
Chuo Kikuu Huria cha Tanzania
omarymohamed36@gmail.com

Ikisiri

Makala hii imechunguza utandawazi wa Kiswahili, kuimarika na kulegalega kwake kama lugha rasmi ya Afrika. Data za msingi katika makala hii zilipatikana maktabani kwa kudurusu nyaraka zinazohusiana na mada teule. Data za upili zilizotumika kuthibitisha data za msingi zilipatikana maktabani kwa mbinu ya usomaji makini. Matokeo ya utafiti uliozaa makala hii yameonesha historia, maendeleo na kuimarika kwa utandawazi wa Kiswahili Barani Afrika. Pia, imeonesha sababu za kihistoria, kisera na kisaikolojia zinazosababisha kulegalega kwa Kiswahili kama lugha rasmi ya Afrika. Baadhi ya mataifa yanadai kuwa lugha za kikoloni ni vigezo muhimu vya kupima hadhi ya taifa kiuchumi, kisayansi na kiteknolojia. Muelekeo huu unaangukia katika kuzienzi lugha za Kikoloni na unaambatana na jitihada za kupuuza lugha za asili za Kiafrika kwa kuziona katika uchanga usioweza kumudu mahitaji ya utandawazi. Makala hii inapendekeza kuwa ni wakati muafaka kwa mataifa ya Afrika kuunda sera ya lugha itakayohusisha mataifa yote na itakayotekeleza kwa vitendo. Kwa kufanya hivyo, lugha ya Kiswahili itakuwa alama ya Uafrika na lugha rasmi ya Afrika.

Istilahi za Msingi: Utandawazi, Kiswahili, lugha rasmi, kuimarika na kulegalega.

1.0 Utangulizi

Mtazamo wa kuimarika na kutoimarika kwa lugha, kwa upana wake, ni ukadiriaji wowote wa kihisia, kiufahamu na kitabia kuhusu mwitikio wa wazungumzaji wa lugha inayohusika. Jambo linalosisitizwa katika ufafanuzi wa mitazamo kuhusu lugha ni ile hali ya kuwa tayari kiakili na kuitumia katika

MAKALA HALISI HISTORIA YA MAKALA

Kupokelewa: 02 Machi
2022

Kurekebishwa: 30 Juni
2022

Kukubaliwa: 29 Julai
2022

Kuchapishwa: 20
Septemba 2022

ISSN: 2799 – 2187

Juzuu 1,

Toleo 1,

uk.105 – 114.

NUKUU

Maguo, M. O. (2022). Utandawazi wa Kiswahili: Kuimarika na Kulegalega kama Lugha Rasmi ya Afrika. *Jarida la Fahari ya Kiswahili*, 1(1), 105 – 114.

nyanja zote za kijamii (Ryan na wenzake, 1982). Mitazamo huonesha hisia za kupenda au kutopenda kitu fulani. Kuimarika na kutoimarika kwa lugha ya Kiswahili kunatokana na mitazamo ya wazungumzaji wa lugha inayohusika.

Mitazamo ya lugha hujumuisha umuhimu wa kijamii unaoambatishwa na lugha, pamoja na namna mbalimbali za matumizi ya lugha katika jamii. Umuhimu wa lugha ni miongoni mwa mambo yanayochangia mitazamo ya lugha. Lugha yenye watu wengi katika shughuli nyingi na muhimu, watu huipa umuhimu wa kujenga mitazamo chanya kwake. Kwa kawaida, lugha iliyo na hadhi, iliyopata maenezi mapana, itakuwa na mtazamo chanya inapolinganishwa na lugha nyingine ndogo kimatumizi (Edwards, 1982). Kwa mfano, lugha ya Kinyakyusa ina hadhi ndogo inapolinganishwa na lugha ya Kiswahili. Pia, lugha ya Kiswahili ina hadhi ndogo inapolinganishwa na Kiingereza. Hoja hii ndiyo inayoibua mitazamo chanya na hasi kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili kama lugha rasmi ya Afrika.

Licha ya hadhi, umuhimu wa lugha huchangiwa pia na wazungumzaji wa asasi zinazoiunga mkono. Hadhi ya lugha hujumuisha nguvu za kiuchumi, kisiasa na kijamii, pamoja na matumizi katika viwango mbalimbali vya elimu, idara za serikali kitaifa, kimaeneo na katika biashara, uchapishaji na matumizi mapana katika vyombo vya habari (Triands, 1971). Kwa hiyo, ipo mitazamo ya kuimarika na kusita kwa lugha ya Kiswahili Barani Afrika katika kipindi hiki cha utandawazi.

Kiswahili ndio lugha yenye ukubalifu wa kimataifa kuliko nyingine Barani Afrika kwa sababu ina usilimisho unaorahisisha kujifunza na kuitumia. Pia, inaweza kuzimudu teknolojia mpya zinazoibuka kupitia uundaji wa maneno (Ryanga, 2002). Nchi nyingi zinazoinuka kiuchumi tayari zimeanza kwa dhati kutandawazisha lugha zao za kiasili ili zinufaike kikamilifu katika mfumo wa utandawazi. Baadhi ya mataifa hayo ni Israel, China, Japan na Korea. Bara la Afrika linapaswa kuiga mataifa haya na kuanza kutandawazisha kwa vitendo lugha zake za asili ili kuukabili utandawazi. Chachage (2003) anasisitiza kuwa Bara la Afrika litaingia katika utandawazi kupitia juhudi pana za kujitegemea na kuondoa umelea wa kutegemea lugha za kigeni kimsamiati na katika nyanja zote za kijamii.

Ipo haja ya kubadilisha mitazamo hasi kuhusu lugha za Kiafrika, ikiwemo lugha ya Kiswahili iliyoteuliwa kuwa lugha rasmi ya Afrika tangu mwaka 1986 na kuanza kutumika mwaka 2004. Hakuna taifa lililopiga hatua katika nyanja za kiteknolojia na kiuchumi kwa kutumia lugha ya kuazima. Mataifa ya Afrika yana wajibu wa kuikuza na kuipanua kijiografia na kimatumizi lugha ya Kiswahili. Hata hivyo, Pono (2001) anatoa angalizo kuwa siyo lazima tuu matumizi ya lugha za kigeni ili tukuze Kiswahili kama lugha rasmi ya Afrika. Makala hii imechunguza utandawazi wa Kiswahili, kuimarika na kulegalega kama lugha rasmi ya Afrika.

2.0 Mbinu za Utafiti

Suala la nafasi na dhima ya Kiswahili katika muktadha wa Afrika limewashughulisha wanazuoni wengi wa ndani na nje ya Afrika kwa mitazamo na misukumo mbalimbali. Baadhi ya wataalamu hao ni Msanjila (1997), Mekacha (2000), Qorro (2000), Rono (2001) na Chachage (2003). Tafiti za wanazuoni hao zinaonesha kuwa lugha ya Kiswahili ina ukubalifu wa kimataifa kuliko nyingine Barani Afrika kwa kuwa ina usilimisho unaorahisisha kujifunza na kuitumia. Makala hii imechunguza utandawazi wa Kiswahili, kuimarika na kulegalega kwake kama lugha rasmi ya Afrika. Data za msingi katika makala hii zilipatikana maktabani kwa kudurusu nyaraka zinazohusiana na mada teule. Data za upili zilizotumika kufafanua na kujaziliza data za msingi zilipatikana maktabani kwa mbinu ya usomaji makini.

3.0 Kuimarika kwa Utandawazi wa Kiswahili

Lugha ya Kiswahili, kama ilivyo lugha nyingine za kimataifa kama vile Kiingereza, Kijerumani na Kiarabu imepiga hatua kubwa ya kuwa moja ya lugha za kimataifa kwa minajili ya kupanua na kuimarisha uhusiano katika nyanja zote za kijamii. Hatua za kuendelea kukua na kupanuka kwa lugha ya Kiswahili kimatumizi na kijiografia ni mojawapo ya jitihada kubwa za kutozitenga nchi za Kiafrika katika jamii za kimataifa. Kwa kuwa utandawazi unahusika na uunganishaji wa mataifa mbalimbali, Afrika inahitaji lugha moja yenye asili ya Kiafrika ili kuusambaza na kuukabili utandawazi (Sullivan, 1994). Lugha ya Kiswahili ni mfano mzuri wa lugha zenye historia ndefu na zinazoendelea kukua kwa kasi Barani Afrika.

Utandawazi ni dhana inayolenga kupunguza na hata kuondoa mamlaka ya dola katika nchi kwa kuzidisha mamlaka ya mashirika ya kimataifa ili kudhibiti uwezo wa mashirika ya kitaifa. Utandawazi una dhamira ya kuondoa vikwazo vyote vya kijiografia na kisiasa ili kuruhusu mtiririko huru wa nguvu kazi baina ya mataifa (Little, 1996). Pia, unatumiwa kuelezea mikabala ya kiutamaduni, kielimu na kisiasa inayosisitiza maungano na mahusiano yanayokiuka mipaka ya taifa moja na jingine, pamoja na kuenea na kusambaza tamaduni kutoka sehemu moja hadi nyingine. Pia, husambazwa kupitia itikadi, teknolojia na lugha (Amatubi, 2002). Lugha ndicho chombo muhimu zaidi katika usambazaji wa utamaduni. Maelezo haya yametumika kama msingi wa kupima nguvu na mtiririko wa lugha ya Kiswahili kama lugha ya utandawazi katika Bara la Afrika.

Hapana shaka kuwa utandawazi unaenea kwa kasi Barani Afrika kupitia lugha za kigeni, zikiwemo za Kiingereza na Kifaransa. Hali hii yafaa kutupiliwa mbali iwapo Bara la Afrika linatarajiwa kunufaika kikamilifu kutokana na utandawazi (Njihia, 2005). Afrika inahitaji lugha moja yenye asili ya Kiafrika kama lugha ya kuusambaza utandawazi. Mathalani, lugha ya Kiswahili ina historia ndefu kwa kuwa ilianza kuwa lugha ya kimataifa na iliwekwa katika ramani ya utandawazi kupitia biashara ya watumwa baina ya jamii za Afrika Mashariki, Uarabuni na Ulaya.

Lugha ya Kiswahili ilianza kuwa ya utandawazi kabla na baada ya kuteuliwa mwaka 1925 kuwa lugha rasmi ya nchi za Afrika Mashariki za wakati huo za Uganda, Tanganyika, Zanzibar na Kenya. Uteuzi huo uliambatana na zoezi la usanifishwaji wake (Mbaabu, 2007). Utandawazi wa Kiswahili unajipambanua katika historia na asili yake iliyofungamana na nadharia za kiisimu na kihistoria ambazo zinathibitisha utandawazi wa lugha hii kupitia Ubantu na mwingiliano wa muda mrefu baina ya jamii za ndani na nje ya Afrika Mashariki (Guthrie, 1948). Matokeo yake, lugha ya Kiswahili ilivunja mipaka ya kijiografia, kimatumizi na kimsamiati hata kabla ya ujio wa wakoloni kutoka Ulaya.

Ujio wa Wamisionari katika nchi za Afrika Mashariki ulisaidia sana kutandawazisha lugha ya Kiswahili. Wamisionari walianza kuifundisha lugha ya Kiswahili katika mataifa ya Magharibi. Pia, walikuwa waasisi wa somo la Kiswahili katika vyuo vikuu katika nchi za Magharibi kama vile Leiden nchini

Ujerumani. Pia, shughuli za vyombo vya habari zimechangia sana kuisambaza lugha ya Kiswahili ulimwenguni kote kutokana na kuwepo kwa idhaa mashuhuri za utangazaji duniani, kama vile BBC (London) na VoA (Marekani). Aidha, zipo redio, magazeti na majarida yanayochapishwa kwa lugha ya Kiswahili katika mataifa ya Magharibi na Mashariki (Sapir, 1958).

Jambo lingine linalothibitisha utandawazi wa lugha ya Kiswahili ni namna inavyowianishwa na lugha nyingine Barani Afrika. Kwa mfano, hapa ulimwenguni, Bara la Afrika linafikiriwa kuwa na lugha nyingi kuliko mabara mengine. Linakadiliwa kuwa na lugha kati ya 800 na 1140 (Bourhis, 1982). Katika lugha hizo, Kiswahili, Kihansa na Kiarabu, ndizo zenye wasemaji wengi kuzidi hata baadhi ya lugha za kigeni kama vile Kijerumani, Kireno na Kifaransa. Lugha ya Kiswahili imevuka mipaka ya utaifa wa mataifa ya Afrika Mashariki, kiasi cha kuteuliwa kuwa lugha rasmi ya Umoja wa Afrika tangu mwaka 1986 na mwaka 2004 ilianza kutumika rasmi. Kuchelewa kwa utekelezaji wa azimio hilo pengine kumetokana na kukosekana kwa Sera ya Lugha inayolenga kuikuza na kuiendeleza kwa vitendo, kisheria na kikatiba (Mekacha, 2000). Lugha ndicho chombo mahususi cha kuwaunganisha watu katika kutekeleza majukumu yao katika nyanja zote za kijamii.

4.0 Kulegalega kwa Lugha ya Kiswahili kama Lugha Rasmi ya Afrika

Kusita kwa ukubalifu wa lugha ya Kiswahili kama lugha rasmi ya Afrika kunatokana na sababu mbalimbali za kihistoria zilizosababisha kwa kiasi fulani kuwepo kwa mielekeo ya lugha. Tangu tupate uhuru, kuna mivutano katika mataifa ya Kiafrika kuhusu hali na hadhi ya matumizi ya lugha zao. Kwa mfano, kuna wale wanaodai kuwa lugha za kikoloni ni vigezo muhimu vya kupima hadhi ya mtu kijamii, kiuchumi na kitaifa. Muelekeo huu unaangukia katika kuzieni lugha za kikoloni na unaambatana na jitihada za kuzipuuza lugha za asili za Kiafrika kwa kuziona katika uchanga usioweza kumudu mahitaji ya utandawazi (Bourhis, 1982). Pamoja na jitihada zao za kibinafsi, lugha hizo zimesalia kuwa za watu wachache. Sehemu inayofuata imechunguza sababu za kulegalega kwa Kiswahili kama lugha rasmi ya Afrika.

4.1 Taathira ya Kisaikolojia

Wasomi wa bara la Afrika wameathirika kisaikolojia kutokana na kukomaa kwa kasumba za kigeni. Athari kubwa ya tatizo la kisaikolojia ni kutojiamini. Suala

la kutojiamini ndilo linalosababisha baadhi ya wasomi kufikiri kuwa lugha za kiasili za Kiafrika hazina maana wala mchango wowote katika ulimwengu wa kisasa (Ansre, 1977). Pia, wanaona kuwa kuziendeleza lugha za asili ni mojawapo ya matokeo ya hatua ya kurudi nyuma. Wengi wao wanaamini kama utamaduni wa jamii zao za Kiafrika una hitilafu. Mitazamo yao inaonesha kuwa maendeleo ya sayansi na teknolojia ni mambo ya mataifa ya Kimagharibi. Kwao, ili kupata teknolojia ya haraka, hatuna budi kuiga kwa kutumia lugha zilizoendelea kisayansi na kiteknolojia. Crystal (1992) anaukosoa mtazamo huo, kwa kueleza kwamba, waneni wa lugha ya kwanza hujihisi kuwa salama na hujivunia lugha zao.

Kasumba za Kikoloni zimeambatana na baadhi ya wasomi wanaoamini kuwa Kiingereza ni lugha ya sayansi na teknolojia na ni alama ya usomi (Qorro, 2002). Mwelekeo huu ndio unaozifanya lugha za Kiafrika kuonekana kama haiwezi kumudu mahitaji katika elimu ya juu, sayansi na teknolojia za kigeni. Teknolojia hizo zinaendelea kubaki nje ya utamaduni wa jamii za Kiafrika kwa sababu lugha zinazotumika kufundishia hazieleweki kwa walimu, wanafunzi na wananchi walio wengi. Katika kutathmini kwa usahihi sababu za kuanguka kwa lugha za asili hapa nchini, ni lazima lugha ya Kiingereza iangaliwe kama pingamizi la uelewa wa maarifa. Bara la Afrika halina budi kutumia lugha zake za asili ili kuepuka utegemezi wa lugha za kigeni usio na tija kwa maendeleo na ustawi wake.

Hali ya kutojiamini inasababisha kuwa na mijadala inayopuuza harakati za Kiswahili kutumika kufundishia katika fani mbalimbali za elimu ya juu. Kuhusiana na hili, Birgit Brock-Utne (2000) anaeleza kwamba lipo tatizo la kuziona lugha za Kiafrika kama zenye upungufu badala ya kuziona kama rasilimali. Jambo hili ni kinyume na matakwa ya maisha ya ulimwengu wa kitandawazi. Matokeo ya hali hiyo ni kudumaa kwa utamaduni wa Kiafrika. Lugha za asili za Kiafrika na fasihi yake zimenyamazishwa na mahali pake kuchukuliwa na lugha za kigeni. Tuisahau kuwa mataifa ya Ulaya yalipokea sayansi na teknolojia kutoka katika utamaduni wa Wayunani, Wamisri na Wagiriki wa kale (La Ponce, 1984). Upokezi wake uliambatana na matumizi ya lugha zao za asili. Haya yanawezekana kwa kutumia lugha ya Kiswahili kama lugha rasmi ya Afrika.

4.2 Matokeo ya Sera ya Lugha

Kukosekana kwa sera ya lugha ndio msingi mkuu wa kusuasua kwa hadhi ya Kiswahili kama lugha rasmi Barani Afrika. Licha ya Kiswahili kuteuliwa kuwa lugha rasmi ya Afrika mwaka 1986 na kuanza kutekelezwa mwaka 2004, mpaka sasa, hakuna sera zinazolenga kuikuza na kuiendeleza (Msanjila na wenzake, 2009). Sera kama mwongozo wa mpango na utekelezaji, ni muhimu kuandaliwa, kuidhinishwa na kutumika kisheria. Kiswahili kama lugha rasmi ya Afrika haiwezi kustawi na kuhimili harakati za utandawazi bila kuwepo kwa sera ya lugha inayolihusisha bara zima. Uundaji upya wa sera za lugha katika nchi za Kiafrika unafaa kujumuisha lugha za Kiafrika kutokana na mahitaji ya kimataifa (Msanjila, 1997). Katika muktadha wa Afrika, Kiswahili ndiyo lugha rasmi. Msimamo wa pamoja kuhusu chaguo la lugha kimaeneo utachochea mtazamo endelevu katika kila nchi ili kufanikisha malengo ya Kiswahili kama lugha rasmi ya Afrika.

4.3 Asasi za Kutandawazisha Kiswahili

Kukosekana kwa chombo imara cha Kanda nzima ya Afrika kumechangia kulegalega kwa Kiswahili kama lugha rasi ya Afrika. Mpaka sasa, hakuna chombo madhubuti kilichoundwa ili kusimamia ukuzaji wa Kiswahili barani Afrika. Baadhi ya vyombo kama vile TATAKI, BAKITA, BAKIZA na TAKILUKI, vyote vya Tanzania, vipo kijiografia zaidi (Masebo na Nyangwine, 2004). Uzoefu unaonesha havijafanikiwa kutekeleza wajibu wao kikamilifu kwa sababu vinatazamwa kama vyombo vya kitaifa na kikanda. Pia, ukuzaji wa lugha katika uwanja wa maarifa mapana na ya kina unahitaji vitendea kazi vinavyokidhi matumizi kwa kuzingatia mawanda yake kijiografia. Barani Afrika, upatikanaji wa vitendea kazi ni tatizo linalotokana na utegemezi kutoka nje. Baadhi yake vimeandaliwa kwa ajili ya mazingira yao.

Pia, ipo mikakati na hatua za makusudi zinazofanywa na mashirika ya kimataifa kama vile Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa kutotoa huduma, iwapo Kiswahili kitatumika. Mathalani, shirika la misaada la Uingereza lilitoa msaada wa ukuzaji na uimarishaji wa Kiingereza nchini Tanzania na Uganda kwa masharti maalumu. Uganda ilitishiwa kusitishiwa misaada iwapo nchi hiyo ingeruhusu lugha ya Kiswahili kuwa miongoni mwa lugha za kufundishia (IMF, 1997). Katiba ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (2000: kifungu 137) inaeleza kuwa Kiingereza ndiyo itakayokuwa lugha rasmi ya Jumuiya na Kiswahili

kitakuzwa kama lugha ya mawasiliano mapana. Hali hii inavunja nguvu za msukumo wa kuimarisha matumizi ya Kiswahili kama lugha rasmi ya Afrika. Matatizo haya yanatokana na mwelekeo wa kisiasa na kasumba ya kutawaliwa (Mhina, 1977). Mitazamo chanya ya mabadiliko kama hayo ikitokea, Kiswahili kama lugha za asili za Kiafrika zitapewa nafasi zinazostahili.

5.0 Hitimisho

Mataifa ya Kiafrika yanatumia lugha za kigeni na yanatofautiana kisiasa kutegemea watawala wanaozitawala nchi hizi. Utamaduni wa mataifa ya Afrika hauna uwiano wa kufikia kuwa na sera ya lugha moja. Hata hivyo, ikumbukwe kwamba, hakuna nchi iliyoendelea bila kutumia lugha yake. Waafrika hawapendi lugha zao. Mapinduzi ya kiuchumi, kisayansi na kiteknolojia katika mataifa yanayoendelea na yaliyoendelea kama vile Japani, China, Urusi, Marekani, Uingereza, India, Ufaransa na Ujerumani yanahusishwa moja kwa moja na matumizi ya lugha zao za asili. Kwa hiyo, ni wakati muafaka kwa mataifa ya Afrika kuunda sera ya lugha itakayotekeleza kwa vitendo itakayohusisha mataifa yote. Kwa kufanya hivyo, lugha ya Kiswahili itakuwa alama ya Uafrika na lugha rasmi ya Afrika.

Marelejeo

Ansre, G. (1977). Four Rationalizations for Maintaining the European Language in Education in Africa. *In Kiswahili*, 47/2:55 – 61.

Brock-Utne, B. (2000). *Who's Education for All? The Recolonization of the African Mind*. New York: Falmer.

Bourhis, R. Y. (1982). Language Policy and Language Attitudes katika Ryan, E. B., and Giles, H. (1982). *Attitudes towards Language Variation*. London: Edward Arnold.

Chachage, S. C. (2003). Kiswahili katika Mukadha wa Utandawazi. BAKITA

Crystal, D. (1992). *An Encyclopedic Dictionary of Language and Language*. Cambridge: MA: Blackwell.

Edwards, J. R. (1982). *Language, Society and Identity*. Oxford: Basil Blackwell.

Edwards, J. R. (1985). 'Language Attitudes and their Implications among English Speakers'. Katika: Ryan, E. B. and Giles, H. (1982). *Attitudes*

towards Language Variation, Social and Applied Contexts. London: Edward Arnold.

- Guthrie, A. (1948). *The Classification of the Bantu Languages.* London: O.U.P.
- International Monetary Fund, (1997). *World Economic. I. M. F, Outlook.*
- La Ponce, J. A. (1984). *Language and Their Territories.* Toronto: Toronto University Press.
- Little, A. (1996). Globalization and Education Research: Whose Context Counts? *International Journal of Development* Vol.16, No.4. Ok. 427 – 438.
- Masebo, J., na Nyangwine, N. (2004). *Nadharia ya Lugha Kiswahili 1.* Dar es Salaam: Afroplus Industries Ltd.
- Mbaabu, I. (2007). *Historia ya Usanifishaji wa Kiswahili.* TUKI.
- Mekacha, R. D. K. (2000). *Isimujamii: Nadharia na Mktadha wa Kiswahili.* Osaka University of Foreign Studies.
- Mhina, G. (1977). The Tanzania Experience in the Use of Kiswahili in Education. *In Kiswahili*, 47/2:6 – 69.
- Msanjila, Y. P., na wenzake, (2009). *Isimujamii.* TUKI.
- Msanjila, Y. P. (1997). ‘Towards a Policy On the Use of Kiswahili in Africa’ katika *Kiswahili Juzuu la 60*, TUKI.
- Msokile, M. (1992). *Kunga za Fasihi na Lugha.* Kibaha: Educational Publisher and Distributors Ltd.
- Njihia, S. K. (2005). Kiswahili na Utandawazi, katika Insha za Jubilei 2005, Utandawazi na Umoja wa Afrika. TUKI.
- Qorro, M. (2000). Mjadala wa lugha ya kufundishishia: sababu zinazotolewa kupitia atumizi ya Kiswahili kama lugha ya kufundishia. *Katika J. S. Mdee na H. J. M. Mwansoko (Wahariri), Kiswahili 2000 Proceedings.* TUKI.
- Rono, M. (2001). *We should Arise and Save Kiswahili: Nairobi: The People.*

- Ryan, E. B. (et.al) (1982). 'An Intergrative Perspective for the Study of Language' katika *Attitudes towards Language Variation*. London: Edward Arnold.
- Ryanga, S. (2002). "The African Union in the Wake of Globalization: The Forgotten Language Dimension". Katika *Kiswahili Juzuu 65*. Dar es Salaam, TUKI, UK. 1-15.
- Roy-Campbell and Qorro, M. (1997). *The Language Crisis in Tanzania: The Myth of English versus Education*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota.
- Sullivan, T. (1994). *Key Concepts in Communication and Cultural Studies*. Canada: Routledge Press

**Mapungufu ya Kiutamaduni Yanavyoathiri
Ustawi wa Mwanamke katika Jamii: Mifano
Kutoka Riwaya ya Sikujua**

Ndimyake Mwakanjuki
Chuo Kikuu Katoliki Ruaha
ndimmyake@gmail.com

Ikisiri

Makala hii imechunguza mapungufu ya kiutamaduni yanavyoathiri ustawi wa mwanamke katika jamii kwa kurejelea riwaya ya *Sikujua*. Data za msingi zilipatikana katika riwaya ya *Sikujua* kwa mbinu ya usomaji makini. Mbinu ya uteuzi lengwa ilitumika kupata riwaya teule. Data za upili kwa ajili ya kufafanua na kuthibitisha data za msingi zilipatikana kwa mbinu ya usomaji wa nyaraka mbalimbali. Makala yamebainisha kuwa utamaduni ni asasi mojawapo ya iliyosheheni taarifa na sheria zilizoeleza uhusiano usio sawa baina ya mwanamke na mwanamke katika jamii. Mwanamke amekuwa mhanga wa kasoro zinazoendelea kumdhalilisha na kumdunisha mwanamke. Makala haya yanapendekeza kuwa jamii haina budi kubadilika kwa kuacha utamaduni unaomdhulumu mwanamke. Serikali na taasisi zisizo za kiserikali zinapaswa kuendelea kukemea kisheria hali yoyote inayonuia kumdhalilisha mwanamke kwa kurejelea misingi ya mila na desturi zilizopo katika jamii.

Istilahi za Msingi: Mapungufu, Utamaduni, Mwanamke, Riwaya na Ufeministi.

1.0 Utangulizi

Historia ya kudhalilishwa kwa mwanamke ni ndefu kwa kuwa inarudi nyuma tangu jamii ya watu ilipoanza kugawanyika katika matabaka. Baadhi ya jamii

**MAKALA HALISI
HISTORIA YA
MAKALA**

***Kupokelewa:* 09 Machi
2022**

***Kurekebishwa:* 22 Juni
2022**

***Kukubaliwa:* 29 Julai
2022**

***Kuchapishwa:* 20
Septemba 2022**

ISSN: 2799 – 2187

Juzuu 1,

Toleo 1,

uk.115 – 130.

NUKUU

Mwakanjuki, N. (2022). Mapungufu ya Kiutamaduni Yanavyoathiri Ustawi wa Mwanamke katika Jamii: Mifano Kutoka Riwaya ya *Sikujua*. *Jarida la Fahari ya Kiswahili*, 1(1), 115 – 130.

zimepitia vipindi vya kihistoria ambapo wanawake walitawala kiuchumi na kisiasa (Fakih, 2017). Mgawanyiko uliendelea na kuimarika zaidi baadhi ya watu walipoanza kumiliki njia za uzalishaji mali na uchumi. Katika kipindi hicho, mwanaume alianza kuwakilisha nguvu za uchumi na kuzitumia kufanya lolote dhidi ya mwanamke. Uhusiano huo ulizidi kukuzwa na taasisi mbalimbali za kijamii, zikiwemo za kidini na kindoa zilizoambatana na utoaji wa mahari. Suala la mahari lilichunguzwa katika misingi ya kumnunua mwanamke hali inayoendelea kumpa mwanaume nafasi pana ya kumtumia kwa namna anavyotaka.

Suala la harakati za wanawake linaangukia katika mikabala mbalimbali iliyopo katika jamii (Sungi, 2011). Upo mkabala unaozitamama harakati za wanawake za kutetea haki zao kama sehemu tu ya fujo za dunia. Mtazamo huu hauwezi kutupatia uzito unaopaswa kwa kuwa hautusaidii kulingana na hali halisi ya maisha iliyopo katika jamii. Mkabala wa mwingine unaeleza kuwa suala la ukombozi wa mwanamke ni ule uhuru wa kurudi nyumbani kutoka kazini, kukaa na kusoma gazeti na kushiriki katika mijadala mizito ya kijamii. Mtazamo huu unataka kutumia mbinu ya kuheshimiana kama kisingizio cha kuhalalisha kuonewa kwa mwanamke. Suala hili linachunguzwa kwa wepesi bila kupewa mtazamo sahihi wa namna ya kulishugulikia kwa kurejelea misingi ya ukweli wa kihistoria.

Wahakiki wengi wa fasihi za Kiafrika wanakumbana na wanawake katika miktadha mingi, lakini wanakwepa kuhakiki uhusika wao kutokana na kuwepo kwa sura mbalimbali. Baadhi yao wamemtazama mwanamke kama mfungwa anayewekwa ndani muda wote pasipo kupewa ruhusa ya kutoka nje. Hali hiyo inamfanya mwanamke kukosa haki zake na uhuru wa kutembea kutoka eneo moja kwenda eneo jingine. Mtazamo huu ulimfanya Chaligha (2011) kuwatazama wanawake kama kundi la watu ambalo limekandamizwa na kutengwa kwa muda mrefu bila kushirikishwa katika kumiliki mali. Miundo iliyopo katika jamii pamoja na asasi zake inashirikiana kumkandamiza mwanamke.

Vipo viashiria vya kuwepo kwa usawa kati ya mwanaume na mwanamke katika jamii. Jambo hilo linadokeza kama jamii imeanza kuweka misingi ya usawa katika jamii. Pia, huwafanya wanawake kupata nguvu na sauti katika maeneo

mengi. Hata hivyo, suala la utamaduni linatazamwa kama mhimiri mkuu unaosababisha kumdunisha mwanamke. Mifumo yake imechangia kuwepo kwa mapungufu yanayochangia athari katika maisha na maendeleo ya mwanamke (Lyatuu, 2011). Kwa hiyo, makala hii imechunguza mapungufu ya kiutamaduni yanavyoathiri ustawi wa mwanamke katika jamii kwa kurejelea riwaya ya *Sikujua*.

2.0 Nadharia na Mbinu za Utafiti

Wahakiki wengi wameshughulikia suala la nafasi ya mwanamke kwa mitazamo inayohitilafiana katika fasihi ya Kiswahili. Baadhi yao ni An (2013), Aburima (2014), Maganga (2015), Ruto (2015) na Massoud (2018). Wataalamu hawa wote kama wawakilishi wa wengine, wameonesha athari za mapungufu ya kiutamaduni katika ustawi wa mwanamke katika jamii. Makala hii imelishughulikia pengo hilo kwa kurejelea riwaya ya *Sikujua* (2022). Data za msingi zilipatikana kwa mbinu ya usomaji makini. Riwaya teule ilichaguliwa kwa kuwa ina mawanda mapana kushughulikia mada iliyolengwa. Data za upili zilizotumika kufafanua na kuthibitisha data za msingi zilipatikana kwa mbinu za usomaji wa nyaraka.

Nadharia ya Ufeministi ina historia ndefu duniani. Msingi wake mkuu ni kuliangaza suala la haki na ukombozi wa wanawake (Wamitila, 2002). Chimbuko la ukandamizaji wa mwanamke linatokana na uroho wa tamaa ya mwanaume ya kutaka kumdhambi na kumtawala mwanamke. Agenda ya Ufeministi inalenga kumaliza utawala wa mwanaume dhidi ya mwanamke (Khatibu, 2011). Ili kufanikiwa, wanawake wanahitaji kubomoa miundo ya mihimili ya utamaduni iliyojengeka katika sanaa, dini, sheria na kaya zinazodhibitiwa na mfumo wa kibaba na taswira zote za asasi zinazomwona mwanamke kama mtu dhaifu. Uhakiki wake ulishika nguvu miaka ya 1960 na kuendelea kukua na kuimarika zaidi miaka ya hivi karibuni.

Mtafiti alichunguza nadharia ya Ufeministi kwa kurejelea nguvu za kijamii zinavyohusiana na nguvu za kisanaa kwa kuwa fasihi inadhibitiwa na miundo iliyopo katika jamii. Pia, hutazamwa kama usawiri mkamilifu ambao huyasawiri maisha kwa undani na huyachunguza kwa mtazamo mpana (Selden na wenzake, 2005). Riwaya teule ya *Sikujua* imechunguza namna suala la mwanamke linavyoaminika na kukubalika katika jamii ya wakati wake. Nafasi ya

mwanamke imehakikiwa kwa kuchunguza uhusiano wa moja kwa moja uliopo baina yake na jamii. Hali hii inatokana na ukweli kwamba riwaya teule ni zao la jamii iliyomkuza na kumlea mwandishi. Uchunguzi kuhusu mapungufu ya kiutamaduni yanavyoathiri ustawi wa mwanamke ulijengwa katika misingi ya nadharia teule kwa kurejelea riwaya ya *Sikujua*.

3.0 Mapungufu ya Kiutamaduni Yanavyoathiri Ustawi wa Mwanamke katika Jamii

Riwaya ya Kiswahili imejengwa katika uwanja mpana unaohakiki hali na harakati za maisha ya kila siku ya jamii. Kupitia utanzu huo, maisha ya mwanamke yametazamwa katika sura mbalimbali. Kila sura katika maisha yake ina harakati zake. Hali hii inatokana na ukweli kwamba kila jamii ina vikwazo vyake, miiko yake na masharti yake yanayomwongoza mwanamke. Kanuni za jamii humfunga mwanamke na kuingilia matakwa na shughuli zake za kujiendeleza kimaisha na kimtazamo. Katika harakati hizo wanawamke wana matatizo yao, matakwa yao na maslahi yao. Suala la mapungufu ya kiutamaduni yanavyoathiri ustawi wa mwanamke katika jamii limebainishwa katika sehemu inayofuata.

3.1 Mwanamke Kubidhaishwa

Katika mfumo wa biashara nchini, wanawake wengi wao hawana uwezo wa kuendesha biashara zao katika kiwango kinachofaa kutokana na kukosekana kwa mitaji inayokidhi harakati zao za msingi. Wengi wao hawakopesheki katika taasisi zinazojihusisha na masuala ya kifedha kutokana kutowafanya biashara zao kisasa pamoja na ukosefu wa mitaji yenye tija. Upungufu unaobainishwa huwafanya wanawake wengi kutokuwa na sauti katika maeneo ya kiuchumi, kiutamaduni na kisiasa (Kauti, 2013). Pia, wanakosa fursa pana ya kushiriki katika shughuli mbalimbali za kijamii kutokana na kutoshirikishwa kikamilifu katika shughuli za kisiasa, kiuchumi na kijamii. Matokeo yake ni kushindwa kusimama imara katika kila fani ya maendeleo katika jamii.

Licha ya kuwepo kwa upungufu uliopo kuhusu hali na hadhi ya mwanamke katika sekta mbalimbali za kijamii, riwaya teule inaonesha namna mwanamke anavyodhalilishwa kwa kubidhaishwa kupitia misingi ya mahari. Sikujua akiwa darasa la sita alikwishatambua mapungufu kadha wa kadha katika mifumo ya kijamii. Kwa kiasi kikubwa, wanawake ni wahanga wa mapungufu hayo. Hali

hii ilimpa Sikujua kiu na nguvu ya kutaka kuwa kiongozi atakayetetea haki za wanawake kwa siku za usoni. Wazo lake liliota mbawa kwa kuwa lilikuwa kama mbio za sakafuni kuishia ukingoni. Wazazi wake walipokea mahari akiwa katika umri mdogo. Jambo hilo lilifanyika kwa kurejelea mila na desturi zilizoimarika katika jamii yake. Katika jamii yake, watoto wa kike walitazamwa kama kiinua mgongo cha mwanaume na ilikuwa fahari kwa waliojaliwa mabinti wengi katika uzao wao. Kwa mfano, mahari iliyopangwa kumuoza Sikujua ilikuwa kubwa mno:

Mzee Jumbe alieleza kwamba, kwanza, mnatakiwa kutoa debe sita za pombe. Pili, majembe manne, mashuka mawili kwa ajili ya baba na mama. Mtatoa mbuzi watano na kuku wanane, ng'ombe arobaini, madume ishirini na mbili na majike kumi na nane (Wanka, 2022: 31).

Maelezo haya yanaonesha kuwa suala la kuwepo kwa mahari kubwa linachochea watoto wa kike kuozwa kabla kukomaa kikamilifu kama ilivyokuwa kwa Sikujua. Suala la mahari linafanyika kwa kurejelea mila na desturi zilizopo katika jamii inayohusika (Silau, 2013). Kila familia ina vigezo na namna yake ya kupanga mahari kama mzee Jumbe anavyotoa msimamo wake kuwa sisi hapa ndio wenye mamlaka, sisi ndio mahakama na sisi ndio bunge. Tunachokipanga na kuamua hicho ndicho sheria, kule tunawasilisha tu na kukaa pembeni tukisubiri utekelezaji na sio mjadala tena (uk. 30).

Pia, suala la mahari lilitazamwa kama mbinu na chanzo kimojawapo cha kupambana na umaskini. Inawezekana jambo hili lilifanyika bila kuzingatia elimu na umri wa binti anayeposwa. Jamii lazima isimame kidete ili kuwalinda na kuwaepusha wasichana dhidi ya madhira yanayowaangukia kutokana na kuwepo kwa mapungufu yaliyopo katika jamii. Wanawake wapambane kwa sauti zao wenyewe na kuacha kuwategemea wanaume wanaodhulumu haki wanazopigania (Seif, 2011). Pia, hawana budi kupigania haki zao ili kupinga udhalilishaji wa mahari kuhalalisha mabinti kuozwa katika umri mdogo. Sikujua aliposwa akiwa darasa la sita. Barua inaeleza:

Kwako mzee matata Mashilingi,

Ni matumaini yetu kuwa u mzima na bikheri wa afya, wewe pamoja na familia yako. Dhumuni la barua hii ni kuunganisha ukoo wako pamoja na ukoo wa mzee Maganga Mabula kupitia binti yako Sikujua Matata na kijana wetu Magesa Mabula. Ni matumaini yetu kuwa ombi letu litapokelewa vizuri.

Wako,

Mzee Maganga Mabula (Wanka, 19).

Baada ya Bi Vumilia, mama yake Sikujua, baada ya kusoma barua, hakuwa na la kufanya zaidi ya kutii matakwa ya mumewe aliyeipokea posa ya binti yao kwa mikono miwili. Hivi ndivyo haki na ndoto za matarajio ya msingi ya watoto wa kike zinavyosiginwa na kuzikwa katika kaburi la sahu. Mojawapo ya matokeo yake ni kwamba mabinti wengi wanaingia katika majukumu ya umama wangali watoto. Pia, kuna ongezeko kubwa la watoto wanaoyakimbia makazi ya wazazi na walezi wao kutokana na kuwepo kwa vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia (Kajeza, 2016). Kwa mfano, baada ya mzee Matata kuipokea posa ya binti yake, mawazo ya Sikujua yaliyoambatana na kilio, machozi na uchungu. Mwandishi anaeleza:

Sikujua, licha ya umri wake mdogo, moyo wake ulipatwa ganzi, alitamani kufa dakika tano halafu arudi kuanza upya maisha yake ya duniani suala ambalo halikuwezekana. Sikujua akikumbuka ndoto aliyokuwa nayo, nafsi yake ilikatishwa kabla hakujapambazuka. Hali hii ilimfanya ajenge chuki dhidi ya baba yake. Alishindwa wa kumweleza kwani watu katika jamii yake hulichukulia suala hilo kama la kifakari (Wanka, 23).

Maelezo hayo yanaonesha mfaidhaiko wa kimaisha na kisaikolojia uliompata Sikujua baada ya baba yake kupokea posa. Suala hili madhara makubwa yanayowapa mabinti wanaotendewa. Inawezekana mwitikio huo unatokana na kukosekana kwa elimu kuhusu madhara ya ndoa za utotoni pamoja na kuimarika kwa mila nadesturi zisizo na tija katika jamii. Jamii inapaswa kubadilika na kuchukua hatua za msingi za kuwanusuru kwa kutunga sheria kali zinazotekelezeka kwa vitendo (Senzighe, 2004). Serikali haina budi kuwalinda watoto kisheria ili kujenga taifa lenye kizazi imara na endelevu. Kwa mfano, mzee Jumbe alihalalisha posa kwa Sikujua kwa kumtaka mzee Matata asiwe na mashaka kwa kuwa mabinti zake wawili wa darasa la tano na mwingine la

darasa la sita waliozwa bila matatizo wala kusumbuliwa na mamlaka. Pia, alimtoa wasiwasi alipoonesha hofu ya kuchukuliwa hatua za kisheria kutokana na serikali kuwekeza hisa zake kwa watoto wa kike. Mzee Jumbe anaeleza:

Wewe ni zuzu kweli. Mtoto wako halafu unaikabidhi serikali? Tangu lini serikali ikazaa? Serikali ina mke au mume? Ukiwa na mke pamoja na watoto, hasa wa kike ni lazima upate kiinua mgongo. Hiyo ndio fahari ya mwanaume aliyejaliwa mabinti katika uzao wake. Changamka acha kuzubaa (Wanka, 23).

Maelezo haya yanaonesha jinsi wanaume wanavyohalalisha suala la ndoa katika umri mdogo. Baadhi ya mapungufu yanayowakumba wanawake yanachochewa na wanawake wenyewe kutokana na kuimarika kwa mfumo wa mila na desturi zilizopo na kuimarika katika jamii (Seleman, 2008). Mama yake Sikujua alishindwa kutafuta njia sahihi za kumnusurika binti yake kwa kuficha ukweli kuhusu dhumuni la barua ya posa. Kwa mfano, Sikujua alipomuuliza mama yake kuhusu dhumuni la barua iliyoletwa na wazee. Mama yake alieleza:

Bi Vumilia anasita kusema kitu chochote kwa sekunde kadhaa, kisha anaguna na kutabasamu bila hata kujua kama ametabasamu. Anajaribu kuyafanya yote hayo ili kumshawishi binti yake kuwa yupo sawa. Ah! Si unajua tena mambo ya baba yako; ile haikuwa barua ila hati ya kuuziana kiwanja, ila ndio hivyo shuleni hakutia mguu (Wanka, 26).

Ufafanuzi huu unaonesha jinsi Bi Vumilia alishindwa kumweleza ukweli binti yake kuhusu barua ya kumposa. Mama anaamua kumdanganya ili kumfariji. Alimficha ili Sikujua asivurugike akili yake kwa kuwa bado umri wake ulikuwa mdogo kuhimiri vishindo vizito vya maisha vilivyotokea katika familia yake. Alichokisikia kwa mama yake, kinampa Sikujua picha kamili kuwa umdhaniye kumbe kumbe siye. Sikujua alitegemea mama yake angemwambia ukweli ili wajaribu kutafuta suluhu kwa pamoja, lakini mambo hayakwenda hivyo. Usilolijua ni kama usiku wa kiza. Wazazi na walezi wengi wamejikuta wakiwatumbikiza watoto wao katika matatizo ili kulinda heshima, utamaduni na matarajio yao.

3.2 Mwanamke Kudhalilishwa

Licha ya kuwepo kwa kanuni na sheria zinazolenga kumtetea mwanamke, kwa kiasi kikubwa, hazitekelezeki kwa kuwa wanawake hawana taarifa za kutosha kuhusu namna bora ya kuumudu utamaduni unaowadhulumu kutokana na kuwepo kwa mianya ya mapungufu iliyopo katika jamii. Wanawake wengi hawana habari hiyo kama inavyoelezwa katika katiba kifungu namba 13 cha ya ndoa cha mwaka 1971 kama kilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2000 (Mtandao wa Jinsia Tanzania, 2001). Wengi wao wanaishia kukandamizwa na baadhi ya mila na desturi zilizoshamiri katika jamii zao. Kwa mfano, katika riwaya teule ya Sikujua, mwandishi ameanesha madhara ya wasichana kuozwa akiwa katika umri mdogo. Sikujua aliamua kukimbilia mjini ili kuyakwepa madhira ya kuolewa katika umri mdogo. Kinyume na matarajio yake, mji ulimtumbukiza katika matatizo makubwa ya kukosa chakula, malezi na shughuli sahihi na halali ya kufanya kulingana na umri wake. Ghafla, Sikujua aliangukia katika kundi la watoto wa mitaani lenye matokeo yasiyoridhisha katika jamii.

Miongoni mwa masuala yanayowasibu wanawake ni kushamiri kwa suala la ubakaji katika jamii. Sikujua alivamiwa na kubakwa akiwa amelala na wenzake kwenye veranda. Mwandishi anaeleza namna mbakaji alivyomtupia katika bega la kulia kama tingo anavyofanya wakati wa kupakua mzigo katika shehena bandarini. Sikujua alifikishwa katika jumba bovu ambako mwindaji haramu alikuwa akingojewa na waliomgoja malishoni. Baada ya hapo, shughuli pevu ikaendelea awamu kwa awamu. Sikujua alilia sana, alilia vilivyo, akalia hadi kilio cha mwisho. Hakuwahi kukutana wala kumjua mwanaume tangu aletwe duniani. Kitendo cha kuwabeba watu watatu walioshiba na uchu uliojaa hadi kumwangukia, ulikuwa ni msiba wa roho yake. Kwa umri aliokuwa nao, mzigo uliotua utosi wake uliashiria mwisho wa maisha yake katika dunia iliyojaa mateso na dhuruma. Mwandishi anaeleza:

Baada ya Sikujua kubakwa, mwili wake ulibadilika na kuwa nyumba ya watesi na wahuni badala ya kuwa hekalu la Mungu. Nafsi yake ilivuja jasho na akili yake kuvurugika. Mwili mzima ulitapakaa damu ambayo haikuwa kikwazo kwa wawindaji wenye uchu mkuu usio na chembe ya huruma dhidi ya mtoto wa binadamu mwenzao. Roho zao ziligeuka

kutoka ubinadamu hadi kufikia unyama. Unyama ulimfanya Sikujua kuwa nusu mtu nusu mfu, nusu duniani, nusu peponi. Mateso yaliuzidi mwili na roho (Wanka, 44).

Maelezo haya yanaonesha kuwepo kwa udhalilishaji wa wanawake kutokana na kushamiri kwa suala la ubakaji katika jamii. Matukio hayo yanapaswa kutokomezwa kwa kuwa yana athari katika maisha na saikolojia ya wanaohusika. Pia, ubakaji unaweza kusababisha vifo na maambukizi ya maradhi yanayotokana na ngono. Mwanamke amejikuta akiogelea katika bahari kuu ya kupuuzwa, kuonewa, kunyanyaswa, kukandamizwa na kulazimishwa kuolewa kabla ya kukomaa kwa mujibu wa sheria za nchi (Oyeronke, 2005). Kuwepo kwa hali ya utamaduni unaomtaka mwanamke awe mnyenyekevu na mtiifu kwa mumewe, kumemfanya mwanamke aendelea kunyanyasika na kudhalilishwa katika jamii.

Suala la ubakaji linatokana na kuimarika kwa mitindo ya maisha inayotumika kama sheria zinaendelea kuonesha nafasi na majukumu ya mwanamke na mwanaume katika jamii. Kipengele cha utamaduni kinatengeneza mazingira ya kumkandamiza mwanamke. Wanaume hawaamini kama wanaweza kuongoza vizuri na kuyatimiza maamuzi ya wanaume na wanawake kwa usawa (Mugane, 2012). Matokeo yake wanawake wanaishia kuwekwa pembeni na kuendelea kuwa watazamaji kwa kila kinachotokea katika jamii zao. Maelezo haya yanaonesha nafasi duni aliyonayo mwanamke katika jamii. Mama yake Sikujua (Bi Vumilia) alikosa nafasi ya kumpinga mumewe baada ya kupokea posa ya binti yao akiwa katika umri mdogo. Jambo hili lilimfanya Sikujua akose msaada kutoka kwa mama yake aliyekuwa muumini wa mila na desturi zinazosisitiza kumtii mume bila kuhoji uhalali wa matakwa na maamuzi yake.

Mapambano ya ukombozi wa mwanawake uwe huru na wa kujitegemea, yasifanye kazi ndani ya matakwa ya mwanaume. Mwanaume asiwepo kabisa katika jitihada za ukombozi wa mwanamke. Ufanisi wa mapambano ya mwanamke dhidi utamaduni usio rafiki unashindikana kwa kuwa mfumo wa kibaba uliasisiwa na wanaume ili kuwatawala wanawake (Abdun, 2000). Utamaduni wa kibaba na mtazamo mkuu wa ustaarabu unaotawaliwa na kuongozwa na wanaume, ndio umewafanya wanawake kuwa wasaidizi wa wanaume katika nyanja za utamaduni, dini, familia, siasa, uchumi, sheria na

sanaa. Mfumo huu unatazamwa kwa jicho la kawaida na jumuiya ya wanawake, wakiwemo wanaishi vijijini ambako mwamko wa kupata elimu inayotetea haki zao, bado ni mdogo sana ikilinganishwa na harakati zilizopo sehemu za mji. Jitihada za wanawake kutaka kujikomboa hazitafua dafu kama mti wa utamaduni wa kibaba hautavunjwa na kung'oa mizizi yake yote.

Mapungufu yaliyopo katika jamii yamechangia kumdhalilisha na kumweka nyuma mwanamke kutokana na sababu za kimila, zikiwemo zinazoruhusu kuolewa katika umri mdogo. Jambo hilo linatokana na baadhi ya wazazi kukosa mwamko wa kuwasomesha watoto wa kike kwa sababu ya kuwepo kwa fikira potofu, pamoja na msukumo mdogo wa uchumi. Sababu hizo hazina budi kuvunjwa kwa kuwa wanawake wanastahili kupata haki za msingi kama ilivyo kwa wanaume. Wanawake wanahamasishwa kusoma kwa bidii hadi elimu ya juu ili kujikomboa kiutamaduni na kimaisha. Jamii inapaswa kuunda sheria zinazotekelezeka zinazolenga kuondoa mianya inayomdhulumu na kudhalilisha mwanamke katika kijamii.

3.3 Mwanamke katika Mimba za Umri Mdogo

Suala la malezi sahihi kwa watoto linapaswa kuimarishwa kuanzia ngazi ya familia katika jamii. Wazazi hawana budi kushirikiana kwa hali na mali ili kuwalea, kuwatunza na kuwajenga watoto katika misingi imara ya kimaadili, kimalezi na kimaisha ili kuwamudu kimahitaji. Wazazi na walezi wanapaswa kushirikiana kikamilifu. Katika baadhi ya jamii, mwanamke anatazamwa kama mhimili thabiti wa uzazi, makuzi na malezi ya familia. Pia, hutegemewa kuijenga familia yake katika misingi imara ya kimaadili. Mwanamke ni nguzo muhimu katika kujenga maadili na malezi ya familia (Kitundu, 2012). Mtazamo huu unamchukulia mwanawake kama chuo cha malezi kinachopaswa kuwekewa mikakati imara ya kuwajengea nguvu na misingi ya kudumu inayolenga kuzimudu harakati zao za kimalezi katika jamii.

Suala la kuwatelekeza watoto ni jambo linalopigwa vita na wanajamii takribani wote katika jamii, pamoja na taasisi za serikali na zisizo za serikali hapa nchini. Hali hiyo inatokana na baadhi ya wasichana wanaopata mimba zisizotarajiwa kutokana na kuwepo kwa sababu mbalimbali, zikiwemo za kubakwa. Wengi wao huwatelekeza watoto wao mara tu baada ya kujifungua. Wengi huyakwepa majukumu yao kama wazazi kutokana na hali ngumu ya maisha na malezi.

Watoto wanaotelekezwa hukosa malezi bora kwa kuwa wengi wao hulelewa na bibi zao ambao nguvu za kiuchumi na kiumri zimewatupa mkono (Mmbogo, 2008). Jambo hilo husababisha baadhi ya watoto kuteteleka kiafya na hata kupoteza maisha. Wasichana hawana budi kujitunza na kuwalea watoto wao kikamilifu mara tu wanapojaliwa.

Mojawapo ya madhara wanayopata watoto wa mitaani ni kubakwa wakiwa katika umri mdogo kama ilivyokuwa kwa Sikujua. Sikujua ni miongoni mwa watu waliyoyaaga makazi yao mapema. Mwandishi ameonesha namna maisha ya mitaani yalimkuza na kumvusha Sikujua hatua moja katika makuzi yake, kutoka utoto hadi kuwa mama baada ya kubakwa. Tumbo lake halikufichika tena, kila mtu sasa akawa anatambua. Sikujua akawa mama mtarajiwa, muda si muda tena. Mtaa utapata mjukuu, mtoto wa mtaa akijifungua. Mungu hamtupi mja wake, Sikujua kajifungua kitoto cha kiume, kiunzi cha kwanza kakivuka, kitendawili mbele kakiwaza, kuishi kwake mtihani, yeye peke yake. Sasa si peke yake tena, pana mwana wake. Chakula, malazi na mavazi, Mungu atamhurumia. Sasa fumbo jipya kafumbiwa, ni vipi atafumbua. Chakula si tu maziwa, kesho atakua atahitaji kwenda shule, matibabu na kupata mahitaji mengine ya msingi. Maelezo haya yanaonesha hali wanayoipitia wabinti waliopata watoto katika umri mdogo. Mwandishi anaeleza:

Maisha ya Sikujua hakuwa salama kwake na mtoto mchanga kumudu harakati za mitaani. Sikujua aliamua kumtelekeza mtoto wake baada ya kuelemeza kimaisha na kimalezi. Mtoto alitelekezwa karibu na geti la hospitali ya wilaya. Kwa bahati njema, mtoto aliokotwa akiwa hai na kulelewa na Bi Chakupewa, mtumishi mmojawapo katika hospitali ya wilaya akihudumu kama daktari bingwa katika kitngo cha watoto (Wanka, 53).

Suala la watoto kutelekezwa lina athari kubwa katika jamii. Watoto walelewe kulingana na maadili bora yaliyozoeleka katika jamii. Wasichana waache tabia kuwatelekeza na kuwatupa watoto wao. Matukio haya yamechangia baadhi ya watoto wanaotelekezwa kupoteza maisha yao. Wazazi na walezi wanapaswa kuwapa msaada mabinti wanaopata mimba kabla ya umri sahihi na kuwajenga kisaikolojia. Watoto watunzwe kwa manufaa ya ustawi na uendelevu wa kizazi

kilichopo na kijacho. Hatua kali za kimaadili na kisheria zichukuliwe kwa wabakaji na utelekezaji wa watoto katika jamii.

Malezi bora yana mchango mkubwa katika kuimarisha misingi ya kimaadili inayotakiwa katika jamii. Kila mwanadamu hutengenezwa na maadili yaliyopo katika jamii yake iliyomkuza na kumlea. Kila hatua ya maisha ya binadamu ina athari zake katika jamii. Kushamiri kwa vitendo ubakaji, kupata mimba katika umri mdogo na kutekeleza watoto katika jamii ni zao la mmomonyoko mkubwa na kudhoofika kwa misingi ya maadili ya kiasili katika jamii (Sanga, 2013). Wajibu wa jamii ni kujenga misingi imara itakayoziba mianya inayosababisha kuporomoka kwa maadili ya kiasili katika jamii.

3.4 Mwanamke katika Biashara ya Ngoni

Suala la kuwepo kwa taasisi za biashara ya ngoni limeshamiri katika jamii nyingi, hasa katika sehemu za miji na miji mikuu hapa nchini. Wahanga wakubwa katika biashara hizo ni wanawake, wakiwemo mabinti wadogo. Baadhi yao wanaingizwa katika biashara hizo bila kutegemea kwa kurubuniwa na wengine kushawishiwa kwa kupewa pesa nono. Katika riwaya teule ya Sikujua, mama Mipango alianzisha taasisi iliyofanya biashara haramu ya ngoni. Aliwakusanya mabinti wenye umri kati ya miaka 16 hadi 20 na kuwafanyisha biashara haramu ya ngoni. Sikujua hakujua, nyavuni kaingia na asione pa kutokea. Pesa anazitaka ndio! Kazi anaitaka ndio! Kazi imekuwa kazi, kazi ina walakini. Kuna muda anaona ni bora angebaki alikokuwa, akiendelea kupambana na masufuria mgahawani, lakini akizitazama noti, kwa kiasi fulani, zinamshawishi nyavuni kubakia. Mama Mipango anasema:

Mwanangu! Kwanza, unisamehe kama nitakuwa nimekukwaza, lakini pole kwa kazi nzito na pevu. Unajua lazima utashangaa kidogo kutokana na kile kilichotokea. Ili dhahabu ing'ae lazima ipite kwenye moto. Nimekuja hapa na kiasi kidogo cha fedha kama kifuta jasho kutokana na shughuli ya jana. Alitoa noti mbili za elfu kumi, kumi na kumkabidhi Sikujua. Kisha, akaaga na kuondoka zake (Wanka, 59).

Ufafanuzi huu unaonesha jinsi baadhi ya mabinti wanavyotumbukia katika biashara ya ngono bila kutegemea. Mama Mipango anadhihirisha suala hilo kama anavyojitetea na kuomba radhi kwa kumpa Sikujua kiasi kidogo cha fedha kama kifuta jasho kutokana na shughuli ya jana. Sikujua na wenzake waliokuwa katika vyumba vilivyo katika umbo la U wakiwa kama vitega uchumi katika taasisi ya Mama Mipango. Mama Mipango walinadi kwa wanaume kama bidhaa ili kujiingizia fedha kupitia mabinti. Mwandishi anaeleza:

Leo nina mali safi sana. Mali mbichi kutoka kwenye maganda yake. Yaani hunielezi chochote, hunizikilizishi lolote bilawekundu watano utaishia kula kwa macho. Mama Mipango anajigamba kwa mchuuzi wake aliyefika ofosini mwake kupata huduma ya kijamii. Hasara roho pesa makaratasi. Sema chumba namba ngapi nikafungue dimba kabla mafisi hayajanusa. Mchuuzi anaeleza huku akirusha noti tano za elfu kumi kumi juu ya meza ya mama Mipango (Wanka, 58).

Maelezo haya yanaonesha namna mama Mipango alivyokuwa akiwatumikisha mabinti katika biashara haramu ya ngono kwa manufaa yake. Licha ya biashara hiyo kumdhaliisha na kumdunisha mwanamke kimaadili, pia inaweza kumwathiri mhusika kiafya na kisaikolojia na kusababisha vifo kutokana na kuwepo kwa maradhi ya kuambukizwa. Biashara hiyo, iliendelezwa pia Rose na Sikujua waliondoka katika taasisi ya Mama Mipango na kuanzisha taasisi yao yenye madhumuni kama ile ya Mama Mipango. Chumba chao kimoja kilitosha kukidhi haja zao. Siku mbili tu zilitosha kutokana na maumbo yao waliyojaaliwa. Walifungua mtandao kupitia *facebook* na *instagram* wenye jina la wakubwa tu ili kulinda hadhi ya ofisi yao. Watu walijiunga kwa kulipa ada ya kiingilio kulingana na uzito wa maudhui yaliyomo. Jamii haina budi kushirikiana na serikali ili kupinga biashara haramu ya ngono inamdhalilisha mwanamke.

4.0 Hitimisho

Makala hii imechunguza athari za mapungufu ya kiutamaduni katika ustawi wa mwanamke katika jamii kwa kurejelea riwaya ya *Sikujua*. Makala yamebainisha kuwa utamaduni ni asasi mojawapo ya iliyosheheni taarifa na sheria zilizoeleza uhusiano usio sawa baina ya mwanamke na mwanamke katika jamii.

Mwanamke amekuwa mhanga wa kasoro zinazoendelea kumdhalilisha na kumdunisha mwanamke. Makala haya yanapendekeza kuwa jamii haina budi kubadilika kwa kuacha utamaduni unaomdhulumu mwanamke. Serikali na taasisi zisizo za kiserikali zinapaswa kuendelea kukemea kisheria hali yoyote inayonua kumdhalilisha mwanamke kwa kurejelea misingi ya mila na desturi zilizopo katika jamii.

Marejeleo

- Abdun, N. H. (2000). *Ukombozi wa Mwanamke*. Morogoro: Mzumbe Book Project.
- Aburima, A. E. A. (2014). Kutathmini Nafasi ya Mwanamke katika Mashairi ya Kiswahili: Uchunguzi wa Mashairi ya Shaaban Robert na Mathias Mnyampala. Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Ann, S. S. (2013). Usasa na Usasa wa Kisasa katika *Nyuso za Mwanamke* ya Said A. Mohamed. Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Challigha, N. E. (2011). Usawiri wa Mwanamke na Mgawanyo wa Majukumu Kijinsia katika Fasihi Picha ya Katuni Mnato za Kiswahili. Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Fakih, S. (2017). Kutathimini Mabadiliko ya Usawiri wa Mwanamke katika Riwaya ya *Utengano na Kamwe si Mbali Tena*: Utafiti Linganishi. Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Kajeza, R. T. (2016). Usawiri wa Mwanamke katika Fasihi Andishi: Mifano Kutoka katika riwaya ya *Machizi na Damu* ya E. Shigongo (2005). Tasinifu ya Shahada ya Kwanza. Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira.
- Kauti, J. (2013). Mabadiliko ya Dhamira katika Nyimbo za Mwanamke wa Kiyao. Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Dar es Salaam.
- Khatibu, M. S. (2011). *Chanjo, Matakwa ya Mwanaume Katika Mwili wa Mwanamke: Ulinganisho wa Ushairi wa Muyaka na Shaaban Robert*. Dar es Salaam: Taaluma ya Taasisi za Kiswahili.

- Kitundu, N, J. (2012). Usawiri wa Wahusika Wanawake Katika Ngano za Kinyiramba. Tasinifu ya Uzamili, Chuo cha Kikuu cha Dar es Salaam.
- Lyatuu, J. (2011). Usawiri wa Wanawake katika Fasihi ya Kiswahili: Ulinganifu wa Waandishi wa Kike na Kiume: Uchaguzi katika Riwaya Teule. Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Maganga, M. (2015). Usawiri wa Mwanamke katika Riwaya ya *Pesa Zako Zinanuka*. Tasinifu ya Shahada ya kwanza. Chuo Kikuu cha Tumain Makumira.
- Massoud, H. S. (2018). Kutathimini Usawiri wa Mwanamke katika Riwaya ya *Mfadhili*. Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.
- Mmbogo, N. (2008). Mabadiliko ya Kimaudhui na Kiwakati katika Nyimbo za Harusi za Jamii ya Waembu. Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Dar es Salaam.
- Mtandao wa Jinsia Tanzania (2001). 'Kuelekea Kwenye Usawa: Taswira ya Mwanamke Tanzania'. Dar es Salaam: SARDC.
- Mugane, D. (2012). Nafasi ya Mwanamke katika Jamii. USA: Harvard Univesity Press.
- Oyeronke, O. (ed) (2005). *African Gender Studies*. New York: Palgrave MacMillan.
- Ruto, M. C. (2015). Matatizo ya Mwanamke katika Kidagaa Kimemwozea na Nyuso za Mwanamke. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Sanga, A. (2013). 'Wanawake na Injili katika Ujasiriamali'. Dar es Salaam: Ujuzi Education Publishers Limited.
- Selden, R., & Wenzake. (2005). *A Reader's Guide to Contemporary Literary Theory*. Great Britain.

Seleman, H. J. (2008). Ujamiishaji wa Kijinsia katika Nyimbo za Harusi za Kihaya. Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dodoma.

Senzighe, R. (2004). *Usawiri wa Mwanamke katika Methali za Wapare*: Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Silau, G. K. (2013). Kutathmini Dhima ya Nyimbo katika Kukuza na Kuimarisha Malezi: Mfano wa Kabila La Wakaguru. Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Sungi, N. A. (2011). Ruwaza ya Shujaa Mwanamke wa Kiutendi katika Jamii ya Wanyanyembe wa Tabora. Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Phoenix Published Ltd.

Wanka, A. J. (2022). *Sikujua*. Iringa: Gredo Company Ltd.

WAANDISHI WA MAKALA

- Athumani S. Ponera** Mhadhiri Mwandamizi,
Chuo Kikuu chaKumbukumbu ya Mwalimu Nyerere,
Kampasi ya Karume Zanzibar, Tanzania.
- Birigitha N. John** Mhadhiri Msaidizi,
Chuo cha Uhasibu Arusha,
Mwanagenzi wa Uzamivu,
Chuo Kikuu cha Dodoma, Tanzania.
- Charles Mbiu** Mhadhiri Msaidizi,
Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Sebastian Kolowa,
Wanagenzi wa Uzamivu,
Chuo Kikuu Huria chaTanzania.
- Deus Gracewelll Seif** Wanagenzi wa Uzamivu,
Idara ya Lugha na Fasihi,
Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Elishafati J. Ndumiwe** Mhadhiri Msaidizi,
Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agustino Tanzania,
Mwanagenzi wa Uzamivu,
Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania.
- Hassan R. Hassan** Mhadhiri Msaidizi,
Idara ya Lugha na Fasihi,
Chuo Kikuu cha Waislamu Morogoro, Tanzania.
- Majuto K. Manyuka** Mwanagenzi wa Umahiri,
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania.
- Mofart O. Ayiega** Mhadhiri Msaidizi,
Chuo Kikuu cha Kenyatta, Kenya.
- Mohamed O. Maguo** Mhadhiri,
Idara ya Lugha na Fasihi,
Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Ndimyake Mwakanjuki** Mhadhiri Msaidizi,
Chuo Kikuu Katoliki Ruaha
Mwanagenzi wa Uzamivu,
Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.